**29 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 29 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. FESTO SANGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Raymond.

Na. 446

**Walimu wa Masomo ya Sayansi Katika Shule za Msingi na Sekondari**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza: -

Je, kuna walimu wangapi wa masomo ya hisabati na sayansi na kuna ziada au upungufu wa walimu wangapi katika shule za msingi na sekondari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya upungufu wa walimu katika shule za msingi na sekondari. Serikali imekuwa ikiajiri walimu wa kada mbalimbali ikiwemo walimu wa masomo ya sayansi kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya walimu wa masomo ya sayansi na hisabati ni 47,354, waliopo ni 30,044 na upungufu ni walimu 17,312. Aidha, mahitaji ya walimu kwa shule za msingi ni 298,687 waliopo ni 173,861 na upungufu ni 124,826.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri walimu wakiwemo walimu wa masomo ya sayansi kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa upungufu ni mkubwa sana unaokaribia nusu, hadi sasa wanafunzi wengi wameelekea kuikataa sayansi, je, Serikali haioni kwamba jambo hilo ni la kufanyiwa ufumbuzi haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa mabinti wengi au wanafunzi wengi wa kike wangependa sana kujifunza sayansi na shule zinaendelea kujengwa kila mkoa hasa za *high school,* lakini upungufu ndiyo kama ilivyoelezwa kwenye swali la msingi, je, ni athari gani ambazo zinaenda kutokea katika jambo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Shally Raymond ambaye amekuwa akifanya ufuatiliaji wa hali ya juu kuhusiana na masuala ya sekta ya elimu na hususan sekta hii ya elimu msingi na sekondari. Ninaomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafahamu kwamba kuna uhitaji wa kuendelea kupata walimu kwa ajili ya kufundisha wanafuzi wetu, na matokeo haya yote yanatokana na sababu ya msingi kabisa ya hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali ya kutoa elimu bila malipo na udahili wa wanafunzi umeongezeka maradufu, na umetengeneza mazingira ambayo tunahitaji kupata walimu zaidi kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuajiri walimu. Walimu wote, pia kwa kuzingatia uhitaji wa walimu wa masomo ya sayansi, katika Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi hiki cha miaka minne walimu 45,742 tayari wameajiriwa na mpaka wakati huu tayari kimetoka kibali kingine cha kuendelea kuajiri walimu

wengine zaidi ya 9,000. Miongoni mwa walimu hao wanaoajiriwa wapo Walimu wa Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa sana katika kuhakikisha inaweka kipaumbele katika masomo ya sayansi. Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba anatambua jitihada ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujenga shule za sayansi za bweni za wasichana kila Mkoa. Shule hizi zimepelekewa shilingi bilioni 4.45 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kunafanyika uwekezaji katika upande wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea na jitihada hizi zote kuhakikisha kwamba walimu wanapatikana wa wa masomo yote pia kwa kuzingatia uhitaji wa Walimu wa Sayansi watapatikana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, wanawafundisha watoto wetu na elimu inakuwa ni bora. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Ulenge kwa niaba Mheshimiwa Shangazi.

Na. 447

**Kufanya Matengenezo Barabara za Mkoa wa Tanga**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa kuzitengeneza barabara za Mkoa wa Tanga zilizopo *TARURA* zilizofunguliwa kwa fedha za tozo na fedha zilizopelekwa Jimboni?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza bajeti Mkoa wa Tanga kutoka shilingi bilioni 12.4 hadi shilingi bilioni 37.1 ambapo kupitia fedha hizi, baadhi ya barabara zimeweza kufunguliwa, kujengwa kutoka changarawe hadi lami, na barabara za udongo kuwa changarawe. Aidha, barabara zilizosajiliwa ndizo zenye

uhalali wa kufanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha zinazotolewa na Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza barabara za lami kutoka kilomita 124.078 hadi kilomita 165.68 na kuongeza barabara za changarawe kilomita 2,104.25, ambapo kati ya hizo zipo ambazo zilikuwa zimesajiliwa na zinaendelea kufanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa, takribani kilomita 1,486.4 za barabara ambazo hazijasajiliwa, tayari Serikali imeshaanza mchakato wa kuzisajili ili zitambulike na kuweza kutengewa fedha kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara *(Routine Maintenance)* kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja ya Mkoa wa Tanga kwa kujenga, kukarabati na kutengeneza kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikupongeze kwa jitihada hizi kubwa za kuifikisha Bajeti ya Barabara za Vijijini kufikia hizo shilingi bilioni 37 kwa Mkoa wa Tanga, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Hii programu ya kupeleka lami hasa katika Miji Midogo imekuwa ikienda hasa kwa kusuasua na kujenga kilomita moja ama mbili. Je, Serikali ipo tayari kuongeza fedha ili angalau katika ile Miji Midogo lami iweze kujengwa angalau kwa kiwango cha kilometa tano mpaka 10?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Barabara nyingi ambazo zimefunguliwa vijijini, bado zinahitaji uboreshaji hasa kwa

maeneo ya kalavati na pia kujengea sehemu ambazo ni za mifereji hasa katika Wilaya ya Lushoto ambayo maeneo mengi ni ya milima. Je, Serikali ipo tayari sasa kuongeza bajeti katika barabara hizo mpya zilizofunguliwa ili ziweze kupitika kwa mwaka mzima? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye amekuwa akifuatilia na kuweka msukumo wa maendeleo katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza ninaomba kumpata taarifa Mheshimiwa Rashid Shangazi kwamba, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali Awamu ya Sita, utaona dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi za zinazohudumiwa na *TARURA* za ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya shilingi bilioni 100 zimetumika katika Mkoa wa Tanga kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara hizi. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hata katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa maana ya mwaka wa bajeti unaofuata tayari fedha inatarajiwa kutumika bajeti imetengwa shilingi bilioni 37.1 kwa ajili ya kwenda kuimarisha miundombinu ya barabara hizi katika Mkoa wa Tanga, ikiwemo katika maeneo ya Miji Midogo ili lami ziweze kujengwa na barabara hizi ziweze kuwanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na barabara hizi ambazo zimefunguliwa za vijijini ambazo zinauhitaji wa kalavati, mifereji ikiwemo katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge la Lushoto, ninaomba nimtaarifu kwamba katika bajeti hiyo ya shilingi bilioni 37.3 ya mwaka wa fedha ujao, tayari kuna mipango ambayo ipo ya kujenga kalavati 33, mifereji ya maji kilometa 1,020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ataona dhamira ya dhati kabisa ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuimarisha miundombinu hii muhimu kabisa ya barabara katika Mkoa wa Tanga na Jimbo lako hili la Lushoto, ndiyo maana utaona Mkoa wa Tanga ulikuwa una bajeti kila mwaka shilingi bilioni 12.4, lakini sasa tunazungumzia mwaka wa fedha 2025/2027, bajeti itakuwa ni shilingi bilioni 37.1. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo hamna maswali ya nyongeza? Haya, Mheshimiwa Ally Juma Makoa. *(Makofi)*

Na. 448

**Kuongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari - Kondoa**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Jimbo la Kondoa Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Kondoa Mji ina mahitaji ya walimu 674 (msingi 414 na sekondari 260), waliopo ni 450 (msingi 266 na sekondari 184) na upungufu ni walimu 224 (msingi 148 na sekondari 76).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024/2025 Serikali imeajiri walimu 15,925 wa shule za msingi na shule za sekondari ambapo Halmashauri ya Kondoa Mji ilipangiwa walimu 33 (msingi saba na sekondari 26).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri walimu na kuwapangia vituo vya kazi katika maeneo yenye uhitaji mkubwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru Serikali kwa kutupatia hawa walimu wapya 33. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uwiano wa walimu wetu kustaafu, kuhama na kwenda kujiendeleza kimasomo na sababu nyingine zinazopelekea kuweka upungufu wa walimu katika Majimbo yetu, unakuwa ni mkubwa kuliko wale wanaoajiriwa, je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inakabiliana na jambo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni upi mkakati wa Serikali wa muda mfupi wa kuongeza walimu hasa ukizingatia kasi kubwa ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kujenga shule mpya pamoja na kuongeza miundombinu, pia ongezeko la wanafunzi katika shule zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni upi mkakati sasa wa muda mfupi wa Serikali kuhakikisha inakabiliana na upungufu mkubwa wa walimu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ally Juma Makoa kwa swali lake hili zuri kabisa linalolenga kuboresha sekta ya elimu ya msingi na sekondari katika Jimbo lake la Kondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumjibu swali lake la kwanza kuhusiana na kasi ya walimu kuhama kutoka kwenye maeneo wanayopangiwa kutoa huduma hii muhimu ya elimu. Ninaomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ili kukabialiana na changamoto hii ambayo unakuta walimu wanapangwa katika vituo na wanaanza kuhama na kutengeneza mazingira ambayo kunakuwa sasa na upungufu wa walimu katika maeneo hususan kule vijijini katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mwongozo uliotolewa na Wizara ya Utumishi, imetoa maelekezo kwamba mtumishi anapopangwa katika kituo cha kazi, hatakuwa na sifa ya kuhama kwenye kituo hicho cha kazi mpaka awe ametimiza miaka mitatu na kuendelea. Kwa hiyo, huo ni mkakati mmoja ambao unatumika kwa ajili ya kuhakikisha inapunguza ile kasi ya watumishi ikiwemo walimu kuhama kutoka katika maeneo na hususan haya ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na hasa katika maeneo ya pembezoni, ili walimu waweze kupata utulivu na waweze kuridhika katika mazingira ya kazi wanayokuwa wamepangiwa na wasiweze kuhama na kusababisha upungufu ambao Mheshimiwa Mbunge anazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mkakati wa muda mfupi wa Serikali wa kuendelea kuongeza walimu na hasa ukizingatia utekelezaji wa Mpango wa Elimu Bila Malipo ambao umetengeneza mazingira ya udahili, sasa udahili umeongezeka na Serikali ya Awamu ya Sita imetumia zaidi ya trilioni 5.1 kwa ajili ya kuimarisha hii sekta ya elimu, kwa kujenga madarasa na shule nyingi kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunahitaji pia kuongeza nguvu katika upande wa upatikanaji wa walimu. Serikali kwanza inaajiri kama nilivyotangulia kusema, kwamba katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita (kipindi cha miaka minne) tayari walimu 45,742 wameajiriwa na kupangwa katika maeneo mbalimbali katika shule zetu hizi. Pia, mpaka wakati huu kimetoka kibali kingine cha walimu zaidi ya 9,000 ambao na wenyewe wataajiriwa kwa ajili ya kupangwa katika maeneo tofauti kwenda kuwafundisha wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna mikakati mingine kwa mfano ya kutumia teknolojia ya TEHAMA kutumia madarasa janja, kwa ufundishaji mubashara, kuajiri kwa mikataba, mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kupitia mapato ya ndani inaajiri walimu hawa kwa mikataba ya muda na kutumia walimu wanaojitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea na taratibu hizi, itaendelea kuongeza nguvu ili ile dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuendelea kuimarisha sekta muhimu ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari iweze kutimia, tupate walimu wa kutosha kwa ajili ya kutoa elimu bora kwa wanafunzi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya msingi uliyojibu umesema kutakuwa kuna ajira mpya takribani 9,000. Hamwoni sasa umuhimu wa kuangalia wale wanaojitolea ili waweze kupata hiyo nafasi ya kuendelea kufundisha, hasa katika Wilaya ya Rungwe, Shule ya Ikuti kuna walimu zaidi ya tisa wanaojitolea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kwa kweli amekuwa akifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye masuala muhimu ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kutaka walimu wale wanaojitolea wapewe kipaumbele katika ajira hizi za walimu. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala hilo tayari lilichukuliwa na Wizara ya Utumishi na tayari linatengenezewa utaratibu wa kuanza kutengeneza kanzidata ya kutunza taarifa na kumbukumbu muhimu za walimu hawa wanaojitolea. Mwisho wa siku, dhamira ni kwamba hawa walimu wanaojitolea waweze kuwa na sifa ya ziada katika kupata ajira hizi ambazo zinatoka katika kila mwaka wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata walimu wako hawa tisa katika Shule hii ya Rungwe aliowataja, ninadhani na wenyewe watakuwa wanufaika wa mipango na mikakati hii ya Serikali ya kuwatazama walimu wetu wanaojitolea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa vibali kwa ajili ya kuajiri walimu. Kwa kuwa katika ajira hii kutakuwa na walimu wa kike na wa kiume, Wilaya ya Nyang'hwale ina upungufu mkubwa sana wa walimu wa kike kwenye shule zetu za sekondari na msingi. Je, Serikali inajipangaje kutupatia walimu wa kike wengi kwenye Wilaya ya Nyang'hwale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Hussein Amar, amekuwa akiuliza maswali mengi ya kuendelea kuweka msukumo katika kuboresha Sekta hii muhimu ya Elimu Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inaendelea na mkakati wake wa kuajiri walimu na kila mwaka wa bajeti fedha zinatengwa kwa ajili ya kuendelea kuajiri walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne hii ya Serikali ya Awamu ya Sita, tayari walimu 45,742 wameajiriwa na sasa kimetoka kibali kingine katika mwaka huu wa bajeti kwa ajili ya kuajiri walimu wengine zaidi ya 9,000. Serikali inaajiri walimu hawa wote kwa kuzingatia jinsia zote (walimu wanawake na walimu wanaume).

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maombi mahususi kabisa kutoka kwako Mheshimiwa Mbunge kwamba unahitaji walimu wanawake katika shule zako za msingi na sekondari katika Wilaya ya Nyang'hwale na nimeyapokea na tutayaweka katika kipaumbele ili walimu wanapoajiriwa naye aweze kupata mgao wa walimu wanaume na pia walimu wanawake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na changamoto kubwa sana ya walimu kuhama kuliko kuhamia hasa wilaya za pembezoni kama ilivyokuwa Tunduru. Je, Serikali haioni haja sasa ya kutoa ajira ama kuajiri walimu ambao wako karibu na maeneo yale ili kuondoa changamoto hizi za walimu kuhama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Hassan Kungu kwa swali lake hili muhimu sana. Kama nilivyotangulia kusema, yanatokea mazingira ambayo watumishi wetu wa kada zote, lakini hapa nitazungumzia wa kada hii ya elimu wanaoomba uhamisho na mara nyingi inatokana na mazingira ya watumishi kupenda vituo vya mijini kuliko vituo vya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali wa kwanza kwa maelekezo yaliyotoka Wizara ya Utumishi ni kwamba mtumishi anapopangwa kwenye kituo hatakuwa na sifa ya kuhama kwenye kituo hicho cha kazi mpaka atimize miaka mitatu. Kwa hiyo, hiyo ni njia moja ya kudhibiti walimu kuhama.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ni kuboresha mazingira ya kazi ya walimu wetu, na ndiyo maana Serikali inajenga nyumba za walimu, lakini inapeleka huduma za umeme kupitia *REA*. Pia, unaona inapeleka huduma za maji, inaboresha miundombinu na huduma za msingi kabisa za kijamii ili walimu wetu wapate amani ya kufundisha katika vituo ambavyo viko pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ni kuhamisha watumishi ikiwemo hawa walimu kwa kutumia namna ya kubadilishana vituo kwamba mwalimu anapotaka kuhama kutoka kwenye kituo kimoja awe amepata mwenzake wa kubadilishana naye kituo, wabadilishane ili kutengeneza uwiano

na kupunguza ule ukali wa walimu kuhama kutoka katika maeneo ya vijijini au tuseme pembezoni kwenda mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inaendelea na jitihada ya kutengeneza haya mazingira ambayo maeneo ya pembezoni yasikose walimu kwa sababu walimu wanakuwa wanahama.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa leo Kiti kinatafuta maswali ya nyongeza, sioni mtu. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa upungufu wa walimu ni mkubwa, je, Serikali ina mpango gani wa kuleta walimu katika Jimbo la Mbulu Vijijini ambako walimu wengi ni wanaume tu, na tuna upungufu wa walimu wa kike? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Flatei Massay kwa swali lake hili zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuajiri walimu kila mwaka wa bajeti. Inapoajiri walimu hawa huwa wanaajiriwa kwa jinsia zote, wanawake na wanaume. Kwa hiyo, haya ni maombi ya Mheshimiwa Mbunge, anatamani kupata walimu hawa wa jinsia, yaani wapate walimu wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imemsikia na katika ajira hizi za walimu zinazotangazwa, Serikali itazingatia na kuweka kipaumbele katika kumletea walimu ikiwemo walimu wanaume na walimu wanawake ili waweze kufundisha katika shule katika Jimbo lake la Mbulu Vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tarime Vijijini kwenye shule nyingi za sekondari hakuna walimu wa kike, lakini imetokea shida nyingine kwamba wale walimu wa masomo ya *arts* wa sekondari wameelekezwa kwenda kufundisha shule za msingi. Sasa ni nini mpango wa Serikali kuondoa changamoto hizo mbili katika Jimbo la Tarime Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waitara ambaye amekuwa akiuliza maswali mengi katika upande huu na kufanya ufuatiliaji katika upande huu wa elimu msingi na hasa kwa maana ya kutaka kuona ustawi wa Sekta hii muhimu katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali inaendelea kuajiri walimu na Serikali inaajiri walimu kwa jinsia zote kwa sababu mchakato huu wa ajira ni wa ushindanishi, yaani walimu *graduate,* wanaomba ajira hizi kwa sifa zao, na wanapatiwa ajira hizi kutokana na kuwa wamefaulu ile michakato ya kuwapata kwa maana ya usaili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea na utaratibu huo kupata walimu wanaume na walimu wanawake na itahakikisha kwamba inaendelea kuwapanga katika vituo mbalimbali. Pia, itazingatia haya maombi mahususi kabisa ya Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na walimu hawa wa sekondari kwenda katika shule za msingi, Serikali ina wajibu wa msingi wa kutengeneza uwiano kufanya msawazo. Kuna maeneo ambayo yana uhitaji zaidi wa walimu na walimu hao wa sekondari wana sifa pia za kufundisha katika masomo ya shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea na mikakati mbalimbali lakini itapunguza changamoto hizo unazozitaja Mheshimiwa Mbunge. Baada ya kujibu maswali haya,

tutakaa, tutazungumza ili tuone umahususi wa changamoto hii katika Jimbo lako ili tuweze kuifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Salma.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa yetu ya Kusini na hasa Mtwara na Lindi kuna tatizo la walimu na watumishi wengine, lakini kikubwa zaidi, watumishi wanapopangiwa katika maeneo yetu ya kazi kabla ya muda wa kuhama, wanataka kuondoka, yaani wanakuja kuchukua *check number* na wakishazipata hizo *check number* wanaondoka. Nini tamko au kauli ya Serikali kwa watumishi hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Salma Kikwete kwa swali lake hili zuri kabisa lenye maslahi mapana kwa siyo tu kwa mikoa ya kusini (Mtwara na Lindi), lakini kwa nchi nzima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa yanatokea mazingira ambayo watumishi na hususan hapa tunazungumzia walimu ambao wakipangwa katika vituo vya kazi na hasa katika mikoa ya pembezoni, wanakuwa wana hamu ya kuhama na kuhamia katika maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ili kukabiliana na changamoto hii ambayo inatengeneza mazingira ya kuwa na upungufu wa watumishi (upungufu wa walimu katika maeneo ya pembezoni) ilishatoa maelekezo kupitia Wizara ya Utumishi kwamba mtumishi hatakuwa na sifa ya kuhama katika kituo cha kazi alichopangiwa mpaka awe ametimiza angalau miaka mitatu katika utumishi kwenye kituo hicho cha kazi na Serikali inazingatia maelekezo hayo yaliyotolewa na Wizara ya Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuendelea

kuwasisitiza Wakurugenzi wote wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa na Makatibu Tawala wa Mikoa waweze kuzingatia mwongozo huu. Hata hivyo, kwa sababu uhamisho unafanyika katika mifumo, Serikali inazingatia maelekezo haya yaliyotolewa na Wizara ya Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna nyingine ambayo Serikali inatumia kukabiliana na hii changamoto ya watumishi kuhama sana kutoka kwenye maeneo ya pembezoni na kutengeneza upungufu endelevu wa walimu ni kutumia namna ya walimu kubadilishana vituo kwamba mwalimu akitaka kuhama kutoka katika kituo kimoja awe amepata mwenzake wa kituo kingine waweze kubadilishana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea na jitihada mbalimbali kwanza za kuendelea kuajiri walimu wawe wengi watosheleze kuwafundisha wanafunzi wetu. Pia, itazingatia misingi ambayo imewekwa ya kudhibiti uhamisho kutoka katika vituo vya pembezoni kwenda mijini ili maeneo ya pembezoni yapate walimu wa kutosha wa kuwafundisha wanafunzi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kila kata ina mwalimu. Kwa nini msiwatumie hawa vilevile kusaidia kupunguza ukwasi wa walimu kwenye shule zetu? Kwenye kila kata kuna Maafisa wa Elimu ambao wako *stationed* kwa Mtendaji wa Kata, wanafanya kazi zao pale, hawaendi kwenye madarasa. Kwa nini msiwatumie hawa nao kusaidia kupunguza kero ya upungufu wa walimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea maelekezo yako, tutayafanyia kazi kama Serikali, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

Na. 449

**Hitaji la Umeme Songea Pori na Nindi - Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, hatua gani imefikiwa kupeleka umeme Kitongoji cha Songea Pori na Nindi vinavyopakana na Msumbiji kama ilivyoahidiwa na Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitongoji cha Songea Pori kilichopo katika Kijiji cha Lunyele, Kata ya Mpepo na Kitongoji cha Nindi kilichopo Kijiji cha Konganywita, Kata ya Mipotopoto vilifanyiwa upembuzi yakinifu na kubaini kwamba, vinahitaji kuwekewa njia za kusambaza umeme za msongo wa kati kwa umbali wa kilometa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatarajia kuvipelekea umeme vitongoji hivi kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Pili "B" ambao utekelezaji wake utaanza mwaka huu wa fedha 2025/2026. Kwa sasa taratibu za kuwapata wakandarasi zinaendelea, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu haya mazuri ya matumaini. Katika miradi hii ya vitongoji inayoendelea kama ambavyo niliongelea mara ya mwisho kwenye swali langu la nyongeza, kasi yake bado ni ndogo sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba umetoa maelekezo na wakandarasi, nimeona sasa wameanza kuripoti lakini kasi yao ni ndogo sana. Nini jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba wakandarasi hao wanaongeza makundi ya kutosha

kuweza kukabili ule muda walioupoteza ili watu waweze kupata umeme katika Wilaya ya Nyasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa wakati unaenda Nindi utakipita Kitongoji cha Magugu kwanza, je, Serikali itasaidia kukifanya na hicho kitongoji nacho kipate umeme wakati huo tunapeleka Nindi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake na pia ninamshukuru kwa maswali haya mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kasi ndogo ya mkandarasi ni kweli mkandarasi ambaye anatekeleza mradi huu katika Jimbo la Nyasa anaitwa *MF*. Pia, ni kweli kasi yake ni ndogo kwa sababu hatekelezi tu katika Jimbo la Nyasa, lakini pamoja na majimbo mengine vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshakaa na mkandarasi kwa siku ya juzi na tumeshakubaliana kwamba aweke wakandarasi wadogo *(sub-contractors)* watatu ili waweze kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi katika maeneo ambayo amepewa mkandarasi ikiwemo Jimbo la Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumeshachukua hatua za ziada za kumtaka mkandarasi aongeze kasi kupitia kuweka ma-*sub-contractor* hawa ambao kwa kweli tutawasimamia kwa weledi mkubwa sana kuhakikisha kasi ya miradi katika Jimbo la Nyasa inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kitongoji cha Magugu, katika mradi huu ambao unakuja kupeleka umeme katika vitongoji, Jimbo la Nyasa litapelekewa takribani vitongoji 91. Kwa hiyo, tutaangalia katika orodha ile kama Kitongoji cha Magugu pia hakipo, basi tutaangalia kwa hatua zinazofuata

namna ya kuwafikishia na Wananchi wa Kitongoji cha Magugu umeme ili na wenyewe waweze kunufaika na kuongeza tija katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Mkandarasi aliyepewa kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vinavyozunguka Ziwa Tanganyika, mradi huo umekuwa unasuasua sana. Nini kauli ya Serikali ili wananchi waweze kupata huduma hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wetu wa miradi ya vitongoji, kwanza tumehakikisha tunawapata wakandarasi wenye weledi. Hata hivyo, kwa mara zote kwa wakandarasi ambao wamesuasua Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu amekuwa akiwaagiza mamlaka ambazo zinasimamia ikiwemo Wakala wetu wa Nishati Vijijini kuhakikisha wakandarasi hawa wanaendeleza kazi katika vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa suala hili la mkandarasi huyu ambaye anapeleka umeme katika vitongoji vilivyomo pembezoni mwa Ziwa Tanganyika, ninaomba kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu nimwelekeze Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Nishati Vijijini achukue jambo hilo alifanyie kazi kwa haraka, amsimamie mkandarasi na kufanya jitihada za ziada pamoja na mkandarasi kuhakikisha mradi huu unatekelezeka kwa kasi na wananchi ambao wanazunguka Ziwa Tanganyika ambao wako katika wigo wa mradi huu wanufaike na mradi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kwa kuwa jiografia ya Wilaya ya Simanjiro, umbali kutoka kitongoji kimoja kwenda kingine, upo uwezekano ikawa ni zaidi ya kilometa

10 katika vijiji vingi vya wilaya hiyo, je, Serikali inaweka mpango gani kuhakikisha kwamba maeneo ya vijiji na vitongoji ambavyo viko mbali kutoka kimoja kwenda kingine na vyenyewe vinapata huduma ya umeme huu wa vitongoji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru pia kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Kwa miradi hii ya sasa ya vitongoji, tumeenda kwa vigezo vya ziada, ndiyo maana kile kigezo cha kwamba tunatoa sawasawa katika kila jimbo katika miradi hii hatujafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza tumeangalia ukubwa wa jimbo husika na vilevile tumeangalia ukubwa wa vitongoji katika jimbo husika pamoja na mahitaji ya kiuchumi na kijamii katika jimbo husika vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mtaona utofauti katika miradi hii inayokuja ya vitongoji kwa sababu tumeangalia vigezo vya ziada kutokana na mahitaji ya jimbo husika na ndiyo maana kuna majimbo makubwa yatapata vitongoji vingi zaidi na yale ambayo hata miradi yao imetekelezwa sana kuliko majimbo mengine, basi tutapunguza idadi ya vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuhakikisha kila jimbo linakuwa na vitongoji vingi zaidi ambavyo vina umeme ili kuweza kuweka usawa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imechukua hatua za ziada katika miradi hii ya vitongoji inayokuja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa niaba yake Mheshimiwa Jesca.

Na. 450

**Ujenzi wa Chuo cha CBE – Kilolo**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU K.n.y. MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza: -

Je ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha *CBE* katika Kata ya Lugalo – Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kilikabidhiwa eneo rasmi, Hati ya umiliki wa eneo la Chuo, Wilaya ya Kilolo mnamo tarehe 8 Julai, 2024 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *CBE* inaandaa Mpango Kabambe *(Master Plan)* kwa ajili ya uendelezwaji wa kudumu wa Kampasi hiyo. Aidha, baada ya kukamilika kwa mpango kabambe, ujenzi wa Chuo kwa Kampasi ya Iringa iliyopo Kata ya Lugalo katika Wilaya ya Kilolo utaanza rasmi 2025/2026 kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua pia katika huo mpango kabambe; je, mme-*consider* jiografia ya Wilaya ya Kilolo kwa kuwa pia jiografia yake ni kubwa na tungehitaji kwamba wanafunzi wote wanaolala katika hicho chuo wawe wa bweni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, kwani alipambania sana kuhakikisha Chuo cha *CBE* kinajengwa katika Mkoa wa Iringa na mahsusi Jimbo la Kilolo na tayari kama nilivyosema tumepata eneo pale na tulishakabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambaye Jimbo lake liko karibu sana na tunapojenga Chuo hiki cha *CBE*. Kwa hiyo, maana yake wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini watafaidika sana kuliko hata Wanakilolo kwa maana ya jiografia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake sasa ni kweli; moja ya mazingatio ambayo tumefanya ni kuhakikisha tunakuwa na mabweni kwa ajili ya wanachuo, kulala hapo ili kuhakikisha wanafunzi wote wanaendelea kusoma vizuri zaidi. Kwa kuwa Mkoa wa Iringa ni mkubwa na Nyanda za Juu Kusini, kwa hiyo, ni lazima kuwe na mabweni na miundombinu mingine stahiki ili waweze kusoma kwa usalama na kwa tija zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Alfred James Kimea, kwa niaba ya Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo mwenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Upo mwenyewe! Haya basi, endelea.

Na. 451

**TANROADS Kuweka Taa za Barabarani Korogwe**

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza: -

Je, lini *TANROADS* itamalizia kuweka taa za barabarani katikati ya Mji wa Korogwe, kwenye Barabara Kuu itokayo Dar es Salaam hadi Arusha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la uwekaji wa taa za barabarani ni endelevu. Hadi sasa jumla ya taa 89 zimewekwa Mji wa Korogwe kwenye urefu wa jumla ya kilometa 2.67. Kwa sehemu iliyobaki ya kilometa 2.0, uwekaji wa taa utaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kimea.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninaomba Waziri afahamu kwamba, Korogwe ni kati ya miji inayokua kwa kasi sana. Kutokuwepo kwa taa za barabarani, kwa baadhi ya maeneo, kunaleta changamoto kubwa. Je, wanatuambia ni lini taa hizo zitakamilika kwenye Mji wa Korogwe mzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba suala la zoezi la kuweka taa ni endelevu, kwa sababu pia, miji imeendelea kukua. Kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu huo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata katika mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026 tumepanga kuendelea kuweka taa katika miji, ukiwepo na Mji wa Korogwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Wilaya ya Lushoto, kwa mujibu wa hali ya hewa, ina ukungu sana, hasa kipindi hiki cha mwezi wa Tano, wa Sita mpaka wa Nane. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka taa katika Miji ya Wilaya ya Lushoto, kama Mlola, Lukozi na Mtae, ili kupunguza ukungu unaosababisha giza zito wakati wa matumizi ya barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe tu maelezo kwamba, kwa sasa katika barabara zote mpya tunazojenga kwenye miji, tunaweka taa, lakini kwa miji ambayo ipo na haipo kwenye miradi, kwanza katika bajeti tumehakikisha kwamba, kila mkoa utatengewa taa zake ambazo zitakuwa ni sehemu ya matengenezo, siyo chini ya taa 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuliwaomba mameneja wa mikoa walete mahitaji ya taa katika miji ambayo imekua. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba, katika miji yote ambayo imekua itawekewa taa. Pia, tutapeleka taa 200 katika kila mkoa ambao wataamua taa zipi zimeharibika na wapi tuweze kuweka ili tuhakikishe miji yetu inapendeza, ukiwepo Mji wa Lushoto, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ni lini Serikali itakamilisha uwekaji wa taa katika Mji Mdogo wa Katoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuweka taa katika Mji wa Katoro na tunakwenda sambamba kuongeza taa upande wa Buseresere. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumepanga na tutaendelea kuziwekea taa katika mwaka huu, lakini tumepanga pia kuendelea kuweka taa pande zote, Buseresere na Katoro. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Mkundi.

Na. 452

**Hitaji la Chuo cha Uuguzi na Uganga, Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Tawi la Chuo cha Uuguzi na Uganga - Ukerewe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli. Bado kuna mahitaji ya vyuo katika maeneo mbalimbali ya nchi, ila kwa sasa Serikali inajenga hospitali yenye hadhi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa katika Wilaya ya Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ujenzi huo, Serikali itaendelea kufanya upembuzi yakinifu kuona kama eneo hilo litahitaji kuwa na Chuo cha Uuguzi mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru sana Serikali kwa kuridhia na kutoa pesa, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa kwa ngazi ya mkoa, Jimboni Ukerewe. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, sasa tunakamilisha majengo mapya ya halmashauri yetu ya wilaya, na yale majengo yaliyokuwa yanatumika zamani yatakuwa matupu, Serikali sasa iko tayari kuja kufanya tathmini ya majengo yale na kama itaridhika, basi ianze kuyatumia, kwa ajili ya mafunzo ya wanafunzi wa uganga na uuguzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kama ambavyo Wizara ya Afya, mimi, yeye, pamoja na Waziri wa Afya tumekuwa tukifanya kazi, hasa kwenye eneo la hospitali, ambayo inajengwa kwenye Wilaya yake ya Ukerewe. Pia ninamwomba sasa aje, halafu Wizara itampa wataalamu kwenda Ukerewe na kuangalia hayo majengo, ili waweze kuleta ripoti. Kama inawezekana tukaanzisha chuo kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha msingi kabla ya kuanzisha chuo ni lazima pawepo na hospitali ambayo itaweza kutumika kama sehemu ya kufundishia kwa sababu, majengo ni jambo moja na hospitali ambayo inaweza ikatumika kwa ajili ya kuhakikisha tunawafundisha wataalamu masomo kwa vitendo, ni muhimu kuwepo katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Bakar Bakar.

Na. 453

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi, Chakechake**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza: -

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Chakechake itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Chakechake imetoa kiwanja Na. 61 chenye ukubwa wa mita za mraba 1,429, eneo la vitongoji, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi, Daraja “B”, cha Wilaya ya Chakechake. Ujenzi wa kituo hicho utagharimu kiasi cha shilingi 802,926,788. Fedha hizo

zitatengwa kwenye Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ahadi ya ujenzi wa Kituo hiki cha Wilaya ya Chakechake ni ahadi ya muda mrefu sasa. Ninataka nifahamu ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, fedha hizi, shilingi milioni 800, zinapatikana kwa ajili ya kwenda kujenga kituo hiki? Pia, nyumba za Askari na Maafisa mbalimbali wa pale Madungu, Chakechake, ni chakavu na ni za muda mrefu sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuko kwenye kipindi cha bajeti. Ninaomba sana muwe watulivu ndani ya Bunge. Swali Waziri halisikii, meza haikusikii, na hata *Hansard* watashindwa kuandika haya mahojiano ambayo yako ndani.

Mheshimiwa Waziri.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninakwenda kwenye swali la pili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umeelewa swali lake? Jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, ahadi hiyo aliyoisema Mheshimiwa Mbunge ni ya muda mrefu, lakini kwanza tuliongeza kituo hicho kwenye mpango, na sasa, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, tunatenga fedha kwenye mwaka wa fedha 2026/2027 tayari, kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la uchakavu wa nyumba za Askari, ni kweli nyumba hizo ni chakavu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwanza tutatuma wataalamu wetu wakafanye tathmini kuhakikisha kwamba, je, tunafanya ukarabati au kujenga upya nyumba hizo? Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali italifanyia kazi suala hilo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Komanya.

Na. 454

**Adha ya Maji Chumvi Vijiji vya Lukale na Mwabagimu, Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Bwawa katika Kijiji cha Lukale na Mwabagimu Wilayani Meatu ili kuondakana na adha ya maji ya chumvi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, viongozi wote wa Serikali, chama, Bunge lako Tukufu, ukiwepo wewe pamoja na Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Wananchi wa Jimbo la Pangani na Watumishi wote wa Wizara ya Maji. Tumepitia kipindi kigumu cha kuondokewa na mdogo wangu kipenzi, Ally Hamidu Aweso, nikiwa katika shughuli zangu za Bunge. Mungu anasema, "Yapaswa kushukuru kwa kila jambo." Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa mtihani huu mzito, lakini Mungu ailaze mahali pema Peponi roho ya Marehemu. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mfupi, Serikali imekamilisha ujenzi wa bwawa dogo katika Kijiji cha Lukale, Wilayani Meatu, ambapo kupitia bwawa hilo, wananchi wanapata huduma ya maji kwa kutumia pampu ya mkono. Aidha, katika hatua nyingine, Serikali imeanza hatua za awali za ujenzi wa mabwawa ya maji katika Vijiji vya Lukale na Mwabagimu, ambapo kazi zinazofanyika kwa sasa ni utafiti wa udongo na upembuzi yakinifu ili utekelezaji wake uweze kuanza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kazi kubwa imefanyika kutoka upatikanaji wa maji 40% mpaka sasa 85%. Ninaomba sasa, kwa kuwa, kuna miradi ya shilingi bilioni nne inayotekelezeka ndani ya Jimbo la Meatu, changamoto iliyopo ni upatikanaji wa fedha. Serikali iko tayari kuleta fedha ili tuweze kukamilisha miradi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa Bajeti 2024/2025 na mpango, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.1 katika mradi huu alioutaja Mheshimiwa Waziri, na tumebakiza mwezi mmoja. Je, Serikali ni lini itaanza kutekeleza mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, lakini kubwa katika eneo lake, tuna miradi sita yenye thamani ya shilingi bilioni nne, ambayo iko katika hatua mbalimbali. Ninataka nimhakikishie, Wizara ya Maji imeongezewa fedha katika bajeti yake na tunatambua utekelezaji wa miradi ya maji unategemea fedha. Tutapaleka fedha kuhakikisha miradi hii inakamilika na wananchi wake wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya swali la pili, sasa hivi tupo katika hatua ya upembuzi yakinifu. Ninataka niwahakikishie, ninapokamilisha, na hii miradi tutaianza, ili kuhakikisha kwamba inakamilika na wananchi hawa waweze kupata huduma hii muhimu sana ya maji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa kipindi cha maswali kimekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii:-

Wageni wa Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, Ndugu Daniel Mussa, Mwandishi wa Habari wa Kampuni ya Uchimbaji Madini ya *Soya One Limited* na mgeni mwingine wa Mheshimiwa

Naibu Spika, Ndugu Mohamed Bawaziri, Mwenyekiti wa CCM, Kata ya Jangwani.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika; hao ni wageni wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mhandisi Anthony Sanga, Katibu Mkuu; Ndugu Lucy Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Zidikher Mndeme, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wathamini; Ndugu Lucas Mwaisaka, Mwenyekiti wa Bodi ya Mipango Miji; Dkt. Lucy Shule, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Tabora; na Ndugu Hamad Abdallah, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*.

Wengine ni Mheshimiwa Hamad, kwanza wewe na wenzako ninawapongeza kwa kazi nzuri, lakini kuna shida sana ya nyumba za bei nafuu kwa wananchi. Muwe na mkakati sasa wa kujenga nyumba *affordable*. Watanzania wanapaswa kuishi kwenye nyumba bora, salama na safi. Ninajua kuna watu wamekuja ofisini kwako kutaka kukusaidia kwenye suala hili, kwa hiyo, lifanyieni kazi, wekeni *Samia Affordable House,* sawa? Hongereni tena.

Waheshimiwa Wabunge, pia, yupo Ndugu Joseph Mafuru, Mkurugenzi Mkuu Tume ya Matumizi ya Ardhi; Ndugu Minja Jeremiah, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora; Ndugu Evelyne Mugasha, Mthamini Mkuu wa Serikali; Ndugu Thom Munkondya, Mshauri na Mtaalam wa Masuala ya Ardhi kutoka *Lapex Properties.*

Wengine ni Ndugu Stella Tullo, Msajili Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; Ndugu Oscar Mgaya, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya *Refinance* ya Mikopo ya Nyumba Tanzania; Ndugu Janeth Mayanja, Mkuu wa Wilaya Chamwino; Ndugu Rebeca Nsemwa, Mkuu wa Wilaya Kilolo; na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mbunge Mstaafu, Jimbo la Chamwino.

Waheshimiwa Wabunge, vilevile kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Ndejembi. Hawa ni familia yake kutoka Jijini Dodoma; Ndugu Subira Rajabu, mke wa Mheshimiwa Waziri;

Ndugu Joram Ndejembi, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; na Ndugu Edna Ndejembi, dada wa Mheshimiwa Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Shangazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, huyo ni shangazi yake.

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ndugu Silas Ilumba, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, na Ndugu Sharifa Hamad, mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri. Pia yupo Ndugu Eva Pinda, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri na Ndugu Peter Pinda. Sasa familia mliokuja, hii kazi ni kubwa sana. Baada ya kazi, chai ya maziwa jioni. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi kutoka Jijini Dar es Salaam. Ndg. Baraka Shangazi – mtoto wake; na Ndugu Athumani Wakanai, mtoto wake. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Naibu Waziri wa Afya ambao ni wawakilishi wa Chama cha Kimataifa cha Madaktari na Wauguzi wa Kikristo Ulimwenguni. *(Makofi)*

Wapo wageni 17 wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, ambao ni walimu kutoka Mkoa wa Rukwa; na wageni 20 wa Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri, Afrika Mashariki, ambao ni walimu wa Shule ya Msingi Mafiga kutoka, Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile yupo mgeni wa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, ambaye ni *Makofi* Hamisi Jumanne, Mwekezaji wa Sekta ya Kilimo cha Choya na usindikaji wa zao la choya kutoka Bukoba Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam; na

wageni watatu wa Mheshimiwa Juma Othman Hija, ambao ni viongozi wa Jimbo la Tumbatu kutoka Kaskazini Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, ambao ni makada wa CCM wakiongozwa na Mjumbe wa Halmashauli Kuu ya CCM Ndugu Leonard Mahenda. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Haji Amour Haji, viongozi wa Kamati ya Siasa Jimbo la Pangawe Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, viongozi wa CCM Jimbo la Amani kutoka Mjini Magharibi Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 101 na walimu nane wa Shule ya Sekondari Canossa kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Ndugu Aziza Ng'amilo mpiga picha wa *Ng'amilo Production* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wanafunzi 57 na walimu sita wa Shule ya Awali na Msingi Corradini kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Taasisi ya *International Peace and Security Summits and Awards* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokaa jukwaa la Spika, ni wageni wa Mheshimiwa Waziri Ndejembi, ambaye ni Ndugu Nathaniel Nhonge Kamishna wa Ardhi. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) Bunge lipokee na kujadili Taarifa ya Utakelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu namba 03 kwa mwaka 2024/2025. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Mbili ambao ni mahususi kwa ajili ya kujadili mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamwahidi kuwa kwa kushirikiana na viongozi na watumishi wote wa Wizara, nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa uadilifu na weledi mkubwa ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma katika

sekta ya ardhi kwa ustawi wa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi mahiri katika kudumisha amani, umoja na mshikamano nchini. Miongoni mwa mambo makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwenye sekta ya ardhi katika kipindi cha uongozi wake ni pamoja na kuwezesha ukamilishaji wa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ambayo imetoa mwelekeo mpya wa usimamizi wa ardhi nchini na maboresho ya mifumo ya TEHAMA ambayo imeongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mheshimiwa Rais amewezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, kukwamua miradi ya ujenzi ya Shirika la Nyumba la Taifa na ongezeko la tengeo la Bajeti kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ambalo limeongeza kasi ya upangaji wa matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Daktari Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu. Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi mahiri katika kusimamia ustawi wa wananchi wa Zanzibar na kuendelea kudumisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto

Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kipekee kabisa kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Dkt. Hussen Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza. Hatua hii inadhihirisha imani ya wana CCM kwa viongozi hawa kutokana na uongozi wao makini unaozingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Tulia Ackson, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge letu na zile za Umoja wa Mabunge Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kipekee ninakupongeza wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza shughuli za Bunge. Ni imani yangu kuwa wananchi wa Jimbo la Uyole Mkoani Mbeya pamoja na wananchi wa Jimbo la Ilala Mkoani Dar es Salaam watawachagua kwa kura nyingi ili mwendelee kuwatumikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa

Njombe Mjini ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisimamia na kuongoza shughuli za Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi kupitia Mhimili huu wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imefafanua na kubainisha utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2024/2025 na mwelekeo wa shughuli za Serikali zitakazotekelezwa katika mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya ardhi, hotuba hiyo pamoja na mambo mengine, imeweka msisitizo katika kuongeza kasi ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na urasimishaji wa makazi yasiyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi mahiri kabisa wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava Mbunge wa Korogwe Vijijini, pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitoe shukrani na pongezi za dhati kwa wajumbe wote wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge kwa kutoa ushauri, miongozo na maelekezo mbalimbali yanayoweza kutusaidia katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie fursa hii kuzishukuru Kamati za Kudumu za Bunge za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Hesabu za Serikali; Bajeti; Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Kamati zote za Kudumu za Bunge. Michango na ushirikiano wao ambao wameendelea kutupatia katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Wizara umekuwa wa manufaa na tija kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwashukuru Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mbunge wa Jimbo la Kavuu; Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu wa Wizara; na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wa sekta ya ardhi kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Kwa hakika kila mmoja wetu ameendelea kutekeleza wajibu wake ipasavyo na hivyo kuwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kipekee kumtakia heri Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Mbunge wa Jimbo la Kavuu katika Uchanguzi Mkuu Oktoba 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani na pongezi za dhati kwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa maelekezo, miongozo, ushauri na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru wasaidizi wangu wote jimboni na wananchi wa Jimbo la Chamwino kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Niwaambie kwamba mwaka huu Mungu akijalia bado tupo pamoja na Wanajimbo wa Chamwino.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninapenda kuishukuru familia yangu na hasa mke wangu Bi. Subira Rajabu, na wanangu wote kwa upendo, ushauri, uvumilivu na kunitia moyo wakati wote nikiwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, ninawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zimeendelea kunipa nguvu katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba mzito wa Mheshimiwa Cleopa David Msuya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliotokea tarehe 7 Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam. Aidha, itakumbukwa

Hayati Msuya aliwahi kuhudumu kama Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makazi na Maendeleo ya Maji kati ya mwaka 1965 - 1967.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 27 Novemba, 2024, Bunge lako Tukufu lilipata pigo kwa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Ukanda wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge na kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, wapo viongozi na Watanzania wenzetu waliofikwa na ajali, majanga na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka Watanzania wenzetu waliojeruhiwa ili waweze kupona na kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ambayo ni rasilimali ya msingi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii imeendelea kuwa sekta wezeshi kwa sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, ujenzi, mifugo, uvuvi, maliasili, nishati, madini na miundombinu. Aidha, sekta ya ardhi imesaidia katika kuongeza uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi na pato la Taifa. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma bora za ardhi kwa kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA, hasa mfumo wa e-Ardhi. Mfumo huo utawezesha wananchi kupata huduma za ardhi kwa wakati pamoja na kupunguza gharama na urasimu. Ni matarajio ya Wizara kwamba, usambazaji wa mfumo huu katika

ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri zote nchini utakamilika ifikapo mwaka 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile huduma za ardhi zimeendelea kutolewa karibu zaidi na wananchi kupitia Kliniki za Ardhi ambazo zimeendelea kuendeshwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kadhalika, Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi *(LTIP)*; Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK); na Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani *(LDI)* ambayo inalenga kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za sekta ya ardhi zinatekelezwa katika ngazi ya Wizara, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mfumo huu wa usimamizi wa sekta uliopo sasa umesababisha kuwepo kwa changamoto katika utekelezaji wa majukumu kutokana na kukosekana kwa mfumo wa uratibu wa pamoja baina ya mamlaka zinazohusika, hivyo kutokuwepo kwa uwajibikaji katika usimamizi wa sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalan, uwepo wa mamlaka tofauti katika utekelezaji wa masuala yanayohusu uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya kiutawala; usimamizi na udhibiti wa uendelezaji ardhi na utwaaji ardhi umesababisha mkanganyiko katika utekelezaji wa majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa changamoto hiyo, Wizara inakusudia kuanzisha Kamisheni ya Ardhi *(Land Commission)* ambayo pamoja na mambo mengine itaweka mfumo mmoja wa usimamizi na utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi katika ngazi zote, hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ramani za msingi zilizopo nchini zimeandaliwa kati ya mwaka 1960 na 1970 na hivyo zimepitwa na wakati kutokana na mabadiliko mengi ikiwemo ya teknolojia

katika mifumo ya upimaji, uoto wa asili na matumizi ya ardhi kama vile uendelezaji wa makazi na ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia changamoto hii, Wizara kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani, itapiga picha za anga kwa kutumia ndege zenye rubani na zisizo na rubani (ndege nyuki *au drones)*. Kazi ya kupiga picha za anga na kuandaa ramani za msingi kwa nchi nzima zenye taarifa za kijiografia zinazosababisha na kubainisha hali halisi ya sasa itakamilika ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya katikati ya miji hayatumiki kikamilifu, na baadhi ya majengo yameanza kuchakaa na hivyo kuhitaji kuendelezwa upya. Ili kukabiliana na hali hii, Wizara imeandaa programu maalum ya uendelezaji upya maeneo yaliyochakaa katika miji mbalimbali nchini. Utekelezaji wa programu hii utahusisha ushirikishwaji wa wananchi na wadau mbalimbali, uondoaji wa majengo chakavu na ujenzi wa majengo ya kisasa yenye miundombinu na huduma katika majiji na miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, imelenga kuboresha taswira na huduma za msingi katika maeneo hayo, kuboresha maisha ya wakazi, kuongeza fursa za kiuchumi na kuhakikisha kuwa miji inakuwa endelevu na himilivu na hivyo kuchangia ipasavyo katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 na hivyo kuwa na Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi ninaomba nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2024/2025, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele yatakayotiliwa mkazo na Wizara katika mwaka 2025/2026 ili kufikia malengo yaliyowekwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na katika maeneo ya kimkakati; pili, kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma, na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na mengine yote yapo katika hotuba niliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 250 kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 Wizara imekusanya shilingi bilioni 136.88 sawa na 54.75% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kukusanya shilingi bilioni 265 kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusisha sekta ya ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kuendelea kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Azma ya Wizara ni kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinachangia katika pato la Taifa kupitia kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi imepanga kukusanya shilingi milioni 18 kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Hadi kufikia 15 Mei, 2025 Tume imekusanya shilingi milioni 15.25 sawa na 84.72%. Aidha, Tume ilitarajia kupokea michango kutoka kwa wadau wa kimkakati kiasi cha shilingi bilioni 1.0 ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2025, shilingi milioni 673.89 zimepokelewa sawa na 67.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa 2025/2026 Tume imekadiria kukusanya shilingi milioni 18 kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo Mkoani Tabora, Vilevile Tume itahamasisha wadau wa kimkakati kuchangia shilingi bilioni moja kwa ajili ya shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 12.17. Aidha, wakati wa utekelezaji wa bajeti Tume ilipata nyongeza ya fedha kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Ongezeko hili limefanya bajeti ya Tume kuongezeka na kufikia shilingi bilioni 17. 17. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.89 ni mishahara, shilingi bilioni 3.24 matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 10.04 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nenda kwenye shukurani, hitimisha, omba pesa, toa hoja; au nenda kwenye maombi ya pesa kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wa maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na sekta ya ardhi. Washirika hao ni pamoja na: Benki ya Dunia; Benki ya *Exim* ya Korea Kusini; *UN habitat, Shelter Afrique; African Union Boarder Program; Regional Centre for Mapping and Resource for Development;* Benki ya Maendeleo ya Afrika; Benki Kuu ya Tanzania; *Tanzania Mortgage Refinancing Compang;* Watumishi *Housing Investment;* Taasisi za Fedha za Ndani; Asasi za Kiraia sekta binafsi; na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kutoa shukrani kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano waliotupatia katika kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi, hakika wanahabari wamewezesha Wizara kuwafikia wadau wengi kwa namna mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuhitimisha Hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya sekta ya ardhi kwa kuboresha huduma

zinazotolewa. Ili kutekeleza azma hiyo Wizara itazingatia vipaumbele kama vilivyoainishwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Mendeleo ya Makazi Fungu Na. 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu Na. 3 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi: mapato ya Serikali shilingi bilioni 265, matumizi ya kawaida; matumizi ya mishahara shilingi 53,820,915,000; matumizi mengineyo shilingi 37,559,123,000 na kufanya jumla ndogo kuwa shilingi 91,380,038,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya maendeleo fedha za ndani shilingi 5,732,469,000; fedha za nje shilingi 56,325,360,000 na hivyo kufanya jumla ndogo kuwa shilingi 62,057,829,000. Jumla ya matumizi ya kawaida ya maendeleo Fungu Na. 48 ni shilingi 153,437,867,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 3 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi: mapato ya Tume shilingi 18,000,000; matumizi ya kawaida ya mishahara shilingi 4,712,143,000; na matumizi mengineyo shilingi 3,475,426,000 ambapo jumla ndogo ni shilingi 8,187,569,000. Matumizi ya maendeleo shilingi 2,520,616,000, jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo Fungu Na. 3 ni shilingi 10,708,185,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla kuu ya fedha zote zinazoombwa kwa Wizara (Fungu 48 na Fungu 03) ili Bunge lako Tukufu liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi 164,146,052,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninatoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, kwa Watanzania, na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii, yameambatishwa majedwali ambayo yanafafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Wizara katika mwaka 2024/2025.

Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni www.lands.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DEOGRATIUS J. NDEJEMBI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**); Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2024/25. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2025/26.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa **19** wa Bunge la **12** ambao ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/26. Aidha, kipekee namshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamuahidi kuwa kwa kushirikiana na viongozi na watumishi wote wa Wizara, nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa uadilifu na maarifa ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta ya

ardhi kwa ustawi wa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

**SALAMU ZA PONGEZI**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, naomba nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi mahiri katika kudumisha amani, umoja na mshikamano nchini; kuimarisha utulivu wa kisiasa na diplomasia ya kiuchumi; na kuvutia uwekezaji katika sekta ya ardhi kwa kuweka misingi bora ya utawala na utendaji kazi. Miongoni mwa mambo makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwenye Sekta ya Ardhi katika kipindi cha uongozi wake ni pamoja na kuwezesha ukamilishaji wa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ambayo imetoa mwelekeo mpya wa usimamizi wa ardhi nchini na maboresho ya mifumo ya TEHAMA ambayo imeongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi. Aidha, Mheshimiwa Rais amewezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na shilingi bilioni **50** zilizotolewa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (PDRF); miradi ya ujenzi ya Shirika la Nyumba la Taifa; na ongezeko la tengeo la Bajeti kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ambalo limeongeza kasi ya upangaji wa matumizi ya ardhi nchini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu. Aidha, ninamshukuru kwa maelekezo na miongozo ambayo amekuwa akitupatia kuhusu masuala mbalimbali ya sekta ya ardhi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi mahiri katika kusimamia ustawi wa wananchi wa Zanzibar na kuendelea kudumisha Muungano wetu. Vilevile, nampongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali katika kuboresha huduma za msingi kwa jamii kama kichocheo cha kudumisha amani, umoja, upendo, mshikamano na utulivu nchini. Napenda kuwashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kipekee kabisa kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Dkt. Hussen Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza. Hatua hii inadhihirisha imani ya wana CCM kwa viongozi hawa kutokana na uongozi wao makini unaozingatia maslahi ya Taifa. Ninaamini na ninawaomba Watanzania wote kwa umoja wetu tuwaunge mkono kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kukupongeza wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge letu na zile za Umoja wa Mabunge Duniani. Aidha, nampongeza Naibu Spika, Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.) kwa kuendelea kukusaidia kwa umahiri katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisimamia na kuongoza shughuli za Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi kupitia Mhimili huu wa Bunge.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kumpongeza tena Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imefafanua na kubainisha utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2024/25 na mwelekeo wa shughuli za Serikali zitakazotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2025/26. Kwa upande wa sekta ya ardhi, hotuba hiyo pamoja na mambo mengine, imeweka msisitizo katika kuongeza kasi ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na urasimishaji wa makazi yasiyopangwa; na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za ardhi. Wizara imezingatia na inaendelea kutekeleza maelekezo na maagizo yanayohusu sekta ya ardhi ili kuimarisha usalama wa milki za ardhi nchini, kudhibiti migogoro ya ardhi, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuifanya ardhi kuwa mtaji hai kwa wananchi wetu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava (Mb.), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ardhi. Maoni na ushauri ambao wamekuwa wakiutoa mara kwa mara umesaidia kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi. Tunaahidi kuendelea kuzingatia ushauri na maelekezo ya Kamati ili kuhakikisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Ardhi zinaendelea kuboreshwa. Aidha, nitumie fursa hii kuzishukuru Kamati za Kudumu za Bunge za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Hesabu za Serikali; Bajeti; Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Kamati zote za Kudumu za Bunge. Michango yenu na ushirikiano ambao mmeendelea kutupatia katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Wizara umekuwa wa manufaa na tija.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kumpongeza Prof. Mohamed Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika. Ushindi wa Prof. Janabi unaongeza hamasa kwa wataalam wetu katika sekta

mbalimbali nchini kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na ubunifu hivyo kuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kushiriki katika soko shindani la kikanda na kimataifa. Aidha, natoa pongezi zangu kwa Dkt. Ntuli Angyelile Kapologwe kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Jumuiya ya Afya ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Tunawatakia mafanikio tele katika utekelezaji wa majukumu yao mapya tukiwa na imani kwamba wataipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani na pongezi za dhati kwa Viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa maelekezo, miongozo, ushauri na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wasaidizi wangu jimboni na wananchi wa Jimbo la Chamwino kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia kwa kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Vilevile, napenda kuishukuru familia yangu na hasa mke wangu Bi. Subira Adadi Rajabu na wanangu kwa upendo, ushauri, uvumilivu na kunitia moyo wakati wote nikiwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, nawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zimeendelea kunipa nguvu katika kutekeleza majukumu yangu.

## SALAMU ZA POLE

12. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa Cleopa David Msuya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliotokea tarehe 7 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam. Vilevile, natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, Wananchi wa Wilaya ya Mwanga na watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huu mzito. Hayati Msuya atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika kujenga misingi ya utawala bora na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, Hayati Msuya atakumbukwa kwa kuweka misingi madhubuti ya utawala na usimamizi wa sekta ya ardhi kwa kipindi alichohudumu kama Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makazi na Maendeleo ya Maji mwaka 1965 – 1967.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 27 Novemba, 2024, Bunge lako Tukufu lilipata pigo kwa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Ukanda wa Afrika. Ninatoa salamu za pole kwako wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa msiba huo. Aidha, wapo viongozi na watanzania wenzetu waliofikwa na ajali, majanga na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina**.** Aidha, Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka watanzania wenzetu waliojeruhiwa ili waweze kupona na kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa.

**MAJUKUMU YA WIZARA**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) Na. 385/2021 la tarehe 07 Mei, 2021, Wizara imekasimiwa usimamizi na uratibu wa majukumu yafuatayo:-

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi;

ii) Kusimamia Utawala wa Ardhi;

iii) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji;

iv) Kusimamia na kuwezesha upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;

v) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa hati za hakimiliki ya kimila;

vi) Kusajili hatimiliki za ardhi, miamala na nyaraka za kisheria;

vii) Kusimamia uthamini wa mali;

viii) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;

ix) Kusimamia uendelezaji milki;

x) Kusimamia utatuzi wa migogoro ya ardhi;

xi) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;

xii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za Sekta ya Ardhi; na

xiii) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake.

**HALI NA MWELEKEO WA SEKTA YA ARDHI NCHINI**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** ardhi ambayo ni rasilimali ya msingi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, imeendelea kuwa sekta wezeshi kwa sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, ujenzi, mifugo, uvuvi, maliasili, nishati, madini na miundombinu. Aidha, sekta ya ardhi imesaidia katika kuongeza uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi na pato la Taifa. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma bora za ardhi kwa kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA (e-Ardhi) pamoja na kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kuanzisha Ofisi za Ardhi za Mikoa. Aidha, huduma za ardhi zimeendelea kutolewa karibu zaidi na wananchi kupitia kliniki za ardhi ambazo zimeendelea kuendeshwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kadhalika, Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP); Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK); na Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI) ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini. Vilevile, maeneo

yaliyoendelezwa bila kupangwa yameendelea kurasimishwa. Pamoja na jitihada hizo, sekta ya ardhi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kasi ndogo ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi ikilinganishwa na mahitaji ya ardhi iliyopangwa na kupimwa; kutokuwepo kwa mfumo mmoja wa usimamizi na utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi katika ngazi zote; udhaifu katika udhibiti wa uendelezaji miji; na migogoro ya ardhi.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** azma ya Wizara ni kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya ardhi ili kuendelea kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi kwa wananchi. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na usambazaji wa Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa Huduma za Ardhi (eArdhi). Mfumo huo unawawezesha wananchi kupata huduma za ardhi kwa wakati, kupunguza gharama na urasimu. Aidha, mfumo huu umeanza kutumika katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Tanga na Mwanza. Ni matarajio ya Wizara kwamba usambazaji wa Mfumo katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri zote nchini utakamilika mwaka 2027.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za sekta ya ardhi zinatekelezwa katika ngazi ya Wizara, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo huu wa usimamizi wa sekta uliopo sasa umesababisha kuwepo kwa changamoto katika utekelezaji wa majukumu kutokana na kukosekana kwa mfumo wa uratibu wa pamoja baina ya mamlaka zinazohusika, hivyo kutokuwepo kwa ufanisi katika uwajibikaji. Mathalan, uwepo wa mamlaka tofauti katika utekelezaji wa masuala yanayohusu uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya kiutawala; usimamizi wa udhibiti wa uendelezaji ardhi; na utwaaji ardhi umesababisha mkanganyiko katika utekelezaji wa majukumu hayo. Ili kuondoa changamoto hiyo, **Wizara inakusudia kuanzisha Kamisheni ya Ardhi (Land Commission) ambayo pamoja na mambo mengine itaweka mfumo mmoja wa usimamizi na utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi katika ngazi zote hivyo, kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya sekta.**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Ramani za Msingi zilizopo nchini zimeandaliwa kati ya mwaka 1960 na 1970 na hivyo zimepitwa na wakati kutokana na mabadiliko mengi ikiwemo ya teknolojia katika mifumo ya upimaji, uoto wa asili na matumizi ya ardhi kama vile uendelezaji wa makazi na ujenzi wa miundombinu. Aidha, ramani za matumizi maalumu (*thematic maps*) zikiwemo za utawala, utalii na miundombinu haziendani na mahitaji ya sasa kwa shughuli za kiuchumi, kijamii, utawala, maamuzi na uwekezaji. Katika kushughulikia changamoto hii, Wizara imekusudia kupiga picha za anga kwa kutumia ndege yenye rubani na zisizo na rubani (drones) zitakazonunuliwa na Wizara kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani. Picha hizo zitachakatwa na kuandaa ramani za msingi kwa nchi nzima. Kazi ya kupiga picha za anga na kuandaa ramani za msingi kwa nchi nzima zenye taarifa za kijiografia zinazobainisha hali halisi itakamilika ifikapo mwaka 2030.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengi ya katikati ya miji hayatumiki kikamilifu na baadhi ya majengo yameanza kuchakaa na hivyo kuhitaji kuendelezwa upya. Ili kukabiliana na hali hii, Wizara inaandaa Programu Maalum ya Uendelezaji Upya Maeneo yaliyochakaa katika miji mbalimbali nchini. Utekelezaji wa Programu hii itahusisha ushirikishwaji wa wananchi na wadau mbalimbali, uondoaji wa majengo chakavu na ujenzi wa majengo ya kisasa yenye miundombinu na huduma. Aidha, imelenga kuboresha taswira na huduma za msingi katika maeneo hayo, kuboresha maisha ya wakazi, kuongeza fursa za kiuchumi na kuhakikisha miji inakuwa endelevu na himilivu na hivyo kuchangia ipasavyo katika pato la Taifa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na hivyo kuwa na Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023). Lengo kuu la Sera hiyo ni kuhakikisha uwepo wa mfumo madhubuti wa umiliki wa ardhi, usawa katika upatikanaji ardhi, usimamizi na matumizi ya ardhi kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Sera iliyorekebishwa imeweka mwelekeo mpya wa usimamizi na utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuwezesha utambuzi na usajili wa kila kipande cha ardhi nchini;

ardhi yote kuchangia maduhuli ya Serikali; usimamizi na uendelezaji wa maeneo nyeti na kutumia baadhi ya maeneo hayo kiuchumi; kuwa na mfumo wa uratibu wa taarifa za kijiografia miongoni mwa taasisi na wadau wengine; kudhibiti migogoro ya ardhi; kuwa na usimamizi wa ardhi unaozingatia hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na kuimarika kwa utawala bora katika usimamizi na utawala wa ardhi. Kwa sasa, Wizara inaendelea na marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazohusu sekta ya ardhi ili kuwezesha utekelezaji wa matamko ya sera.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2024/25 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu haya mawili kwa mwaka 2025/26.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Wizara imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26); Mpango Mkakati wa Wizara; Mikataba; Itifaki; Mipango na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa; Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi; na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo ya kipaumbele yatakayotiliwa mkazo na Wizara katika mwaka 2025/26 ili kufikia malengo yaliyowekwa ni kama ifuatavyo: -

i) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na katika maeneo ya kimkakati;

ii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa taarifa za ardhi na uthamini;

iii) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala na kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya;

iv) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

v) Kuimarisha mipaka ya kimataifa na kuendeleza miji ya mipakani;

vi) Kuimarisha upatikanaji wa ramani ili kuwezesha uandaaji wa mipango mbalimbali ya kitaifa na matumizi mengine; na

vii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa vipaumbele.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2024/25 NA MALENGO YA MWAKA 2025/26**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Fungu **48** -Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48**

*Mapato*

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **250** kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara imekusanya shilingi bilioni **136.88** sawa na asilimia **54.75** ya lengo (**Jedwali Na. 1A**).

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, hali ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na kodi ya pango la ardhi pamoja na tozo nyingine zinazotokana na sekta ya ardhi imeendelea kuongezeka kila mwaka. Makusanyo haya yameongezeka kutoka shilingi bilioni **121.9** mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni **138.9** mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia

**13.95** (**Jedwali Na.1B**). Ongezeko hili limechangiwa na juhudi zilizochukuliwa na Wizara ikiwemo kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato; kutuma ankara za madeni kwa njia ya jumbe fupi za simu, kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi hivyo kuongeza idadi ya walipa kodi, kukutana na wamiliki wa ardhi wenye madeni makubwa na mikakati mingine ya kuongeza makusanyo. Azma ya Wizara ni kuhakikisha kila kipande cha ardhi kinachangia katika pato la Taifa kupitia kodi, tozo na ada mbalimbali. Natumia fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. **Natoa rai kwa wamiliki wote wa ardhi nchini kuhakikisha wanalipa kodi kwa wakati ili kuepuka tozo ya adhabu au hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi yao.**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni **265** kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI katika mikakati ya ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi. Mikakati hiyo ni kama ifuatavyo: -

i) Kuhakikisha viwanja vyote vilivyopimwa vinamilikishwa kwa wahusika. Zoezi hili linaendelea kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo Kliniki za Ardhi ambazo zimekuwa na mwitikio mkubwa wa wananchi;

ii) Kuendelea kutoa elimu ya ulipaji wa kodi ya pango la ardhi kupitia mikutano ya hadhara na shughuli mbalimbali;

iii) Kuendelea kuunganisha namba za simu za wamiliki wote wa ardhi ili waweze kupata jumbe za kuwakumbusha kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati;

iv) Kuratibu usambazaji wa hati za madai na kufikisha mashauri ya kikodi Mahakamani, kufuatilia mashauri yaliyopo Mahakamani, pamoja na kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama; na

v) Kuendelea kusambaza mfumo wa e-Ardhi kwenye Halmashauri mbalimbali nchini.

*Matumizi*
29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni **157.46** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **50.16** zilikuwa kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni **36.64** kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **70.66** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni **86** kwa ajili ya kulipa madeni na hivyo kufanya bajeti ya maendeleo kuongezeka na kuwa shilingi bilioni **156.66** na jumla ya Bajeti ya Wizara kufikia shilingi bilioni **243.46.** Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara ilipokea shilingi bilioni **189.55** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia **77.86** ya bajeti. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni **37.35** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni **22.55** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni **129.65** zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 2**).

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03**
*Mapato*
30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Tume ilipanga kukusanya shilingi milioni **18** kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 Tume imekusanya shilingi milioni **15.25** sawa na asilimia **84.72**. Aidha, Tume ilipanga kupokea michango kutoka kwa wadau wa kimkakati kiasi cha shilingi bilioni **1.0** ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2025, shilingi milioni **673.89** zimepokelewa sawa na asilimia **67.4.** Kwa mwaka 2025/26, Tume imekadiria kukusanya shilingi milioni **18** kutokana na kodi ya pango ya nyumba zilizopo mkoani Tabora. Vilevile, Tume itahamasisha wadau wa kimkakati kuchangia shilingi bilioni **1.0** kwa ajili ya shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi nchini.

*Matumizi*
31. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25, Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni **12.17.** Aidha, wakati wa utekelezaji wa Bajeti, Tume ilipata nyongeza ya fedha kiasi cha

shilingi bilioni **5** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Ongezeko hili limeifanya bajeti ya Tume kuongezeka na kufikia shilingi bilioni **17.17**. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni **3.89** ni Mishahara, shilingi bilioni **3.24** Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **10.04** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Maendeleo. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Tume imepokea jumla ya shilingi bilioni **13.24** sawa na asilimia **77.1** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **2.12** ni Matumizi Mengineyo (OC), shilingi bilioni **2.91** ni Mishahara ya watumishi (PE) na shilingi bilioni **8.21** ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi bilioni **13.02** sawa na asilimia **98.3** zimetumika ambapo shilingi bilioni **2.91** ni mishahara, shilingi bilioni **1.91** ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni **8.20** kwa ajili ya mradi wa maendeleo (**Jedwali Na. 3)**.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bajeti ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi bilioni **3.9** kwa mwaka 2020/21 hadi kufikia shilingi bilioni **17.17** mwaka 2024/25. Ongezeko hili la tengeo la Bajeti limeendelea kuiwezesha Tume kuongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. **Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuongeza tengeo la fedha kwa ajili ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ili hatimaye vijiji vyote nchini viweze kuandaliwa mipango hiyo.**

## UTAWALA WA ARDHI

### Usimamizi wa Sekta ya Ardhi

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa huduma za sekta ya ardhi zinapatikana karibu na wananchi ili kuwapunguzia usumbufu na gharama za upatikanaji wa huduma. Hatua hii imehusisha uendeshaji wa zoezi la kliniki za ardhi kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo wataalam wa kada zote za ardhi wanakuwepo eneo moja kwa wakati mmoja hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma zote za ardhi papo kwa papo; kubuni

miradi ya kimkakati na kusimamia programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK). Hatua hizi zimewezesha kuboresha huduma na kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na milki salama na kuwawezesha kutumia milki hizo kijamii na kiuchumi.




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Bi. Lucy Kabyemera akishiriki katika Kliniki ya Ardhi Kilindi, Tanga*



*Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wakipata huduma za sekta ya ardhi kupitia Kliniki ya Ardhi.*

**Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera na Sheria za Ardhi, Wizara inaratibu uandaaji, usajili na utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji, Hati za Hakimiliki za Kimila na Hatimiliki za Ardhi. Azma hii inalenga kuimarisha usalama wa milki za ardhi kwa wananchi, kuongeza thamani na kudhibiti migogoro ya ardhi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuandaa na kusajili Hatimiliki **500,000**, Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000**, Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100** na Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 Wizara imeandaa na kusajili Hatimiliki **82,567** sawa na asilimia **16.51** ya lengo; Hati za Hakimiliki za Kimila **152,667** sawa na asilimia **29.36** ya lengo; Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **204** sawa na asilimia **204** ya lengo; na Hati za Sehemu ya Jengo **464** sawa na asilimia **46.4** ya lengo. Aidha, jumla ya Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **115,754** imesajiliwa sawa na asilimia **115.75** ya lengo (**Jedwali Na. 4**).



*Mhe. Deogratius Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akimkabidhi Hati ya Hakimiliki ya Kimila mmoja wa wananchi waliohamia Msomera, Wilaya ya Handeni kwa hiari kutokea eneo la Hifadhi ya Ngorongoro*

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mafanikio makubwa yamepatikana katika kuimarisha usalama wa milki za ardhi kwa wananchi na kuwawezesha kutumia hati zao katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kujiletea maendeleo. Katika kipindi hicho, Wizara imeandaa na kusajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **766** hivyo kuwa na jumla ya vijiji **10,987** vyenye Vyeti vya Ardhi ya Kijiji kati ya vijiji **12,333** vilivyopo nchini. Pia, jumla ya Hatimiliki **356,642,** Hati za Sehemu ya Jengo **1,282** na Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **444,447** zimesajiliwa katika mikoa mbalimbali nchini. Kadhalika, kumekua na ongezeko

la utoaji na usajili wa Hatimiliki kutoka Hatimiliki **67,331** katika mwaka 2020/21 hadi **99,366** mwaka 2023/24.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara imepanga kuandaa na kusajili Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000,** Hatimiliki **500,000,** Vyeti vya Ardhi ya kijiji **100** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**. Vilevile, miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria **100,000** zitasajiliwa. Ili kufikia lengo la utoaji wa Hatimiliki katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kusambaza Mfumo wa e-Ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini ili kurahisisha na kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi, kuendelea kuhimiza wananchi kuchangia gharama za urasimishaji na umilikishaji ardhi, kuziwezesha Halmashauri kutekeleza Programu za Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na kuendelea na Kliniki za ardhi ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

**Usimamizi wa Masharti ya Umiliki**

38. ***Mheshimiwa Spika***, Sheria za Ardhi zinamtaka kila mmiliki kuendeleza ardhi aliyomilikishwa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ilipanga kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba **1,000** ili kubaini hali ya uendelezaji**.** Hadi tarehe 15 Mei, 2025, jumla ya viwanja na mashamba **139** yalikaguliwa na viwanja na mashamba **28** yamependekezwa kubatilishwa kutokana na wamiliki wake kushindwa kuyaendeleza. Aidha, katika kipindi cha miaka minne, Wizara ilikagua viwanja na mashamba **1,069** ili kujiridhisha na hali ya uendelezaji wake ambapo, viwanja na mashamba **334** yalibatilishwa baada ya wamiliki wake kubainika kukiuka masharti ya umiliki. Baadhi ya viwanja na mashamba yaliyobatilishwa yameongeza hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hatua hii ya ubatilishaji wa milki imehamasisha baadhi ya wamiliki wa ardhi kuendeleza maeneo yao kwa wakati.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba **1,000** ili kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya umiliki na kuwachukulia hatua za kisheria. Aidha, ardhi ya viwanja na mashamba ambayo milki zake zitabatilishwa itakuwa sehemu ya

hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamoja na kuwapatia wananchi wenye mahitaji. **Natoa wito kwa wamiliki wa viwanja na mashamba kuyaendeleza kwa mujibu wa masharti ya umiliki ili kuepuka Serikali kubatilisha milki hizo.**

**Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji**

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu na kusimamia ardhi ya uwekezaji kwa kushirikiana na taasisi za uwekezaji nchini. Katika mwaka 2024/25 Wizara iliahidi kuwa itaendelea kuratibu na kusimamia maeneo ya ardhi ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na uhakiki wa matumizi ya ardhi iliyotolewa kwa wawekezaji na kuwa na vikao na wadau wa uwekezaji wakiwemo wawekezaji wenyewe ili kuhakikisha ardhi ya uwekezaji inaleta tija inayotarajiwa. Wizara imeendelea kupanga, kupima na kugawa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi ilipokea maombi **235** ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta **32,143.29** na kuyaidhinisha ambapo kati ya hayo, maombi **92** ni ya raia wa Tanzania na **143** ni ya wawekezaji kutoka nje ya nchi. Uwekezaji kutoka nje ya nchi una mtaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni **617.76** sawa na shilingi trilioni **1.63** (**Jedwali Na. 5**). Kwa kipindi cha miaka minne, jumla ya maombi **719** ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta **205,057.48** yaliidhinishwa kwa ajili ya uwekezaji ambapo kati ya hayo maombi **258** ni ya raia wa Tanzania na **461** ni ya wawekezaji kutoka nje ya nchi. Kwa kipindi hicho, uwekezaji kutoka nje ya nchi umekuwa na mtaji wenye thamani ya Dola za Marekani billioni **5.78** sawa na shilingi trilioni **15.57.** Katika mwaka 2025/26 Wizara inakusudia kutenga hekta **5,000** kwa ajili ya uwekezaji.

**Uhuishaji wa Kumbukumbu za Ardhi**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na kumbukumbu sahihi za wamiliki wa ardhi nchini, Wizara inaendelea kuhuisha kumbukumbu katika Mifumo ya TEHAMA inayotumika kuhifadhi kumbukumbu za ardhi. Zoezi hilo linahusisha uhakiki wa taarifa za wamiliki ili ziendane na taarifa za NIDA na mifumo ya taasisi nyingine hususan BRELA. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara imehuisha kumbukumbu za wamiliki

wa ardhi **957,407**. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi **500,000** katika Mfumo wa e-Ardhi na kuendelea na zoezi la uhakiki wa taarifa za wamiliki kupitia zoezi la ubadilishaji wa nyaraka za umiliki kutoka mfumo wa analojia kwenda mfumo wa kidijiti.

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Nchini

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutatua migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero nchini kadri inavyojitokeza. Migogoro inayohusishwa na ardhi iko katika sura mbalimbali kama mipaka ya kiutawala, madai ya fidia, uvamizi wa maeneo ya umma na binafsi, udanganyifu na utapeli kwa kutumia nyaraka za kughushi, madai ya mali za urithi au wanandoa. Vilevile, yapo malalamiko yanayotokana na wananchi kutoridhika na uamuzi wa Serikali au Mahakama, changamoto zinazotokana na zoezi la urasimishaji makazi na upimaji shirikishi wa ardhi pamoja na uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi.



*Mhe. Deogratius Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akisikiliza na kutatua migogoro ya wananchi Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga*

43. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha mwaka 2024/25, Wizara iliahidi kuendelea kushughulikia malalamiko na migogoro ya ardhi kiutawala kupitia mfumo wa kielektroniki pamoja na kushirikiana

na wadau, kuendelea kupanga matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa umma kuhusu umiliki wa ardhi na madhara ya migogoro ya ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2025 jumla ya migogoro **5,801** imetatuliwa kiutawala ikilinganishwa na lengo la kutatua migogoro **3,000**. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Wizara imepanga kushughulikia migogoro **3,000**. **Natoa rai kwa viongozi, watumishi na wananchi kwa ujumla kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na maadili ya utumishi wa umma na kuendelea kushirikiana na wananchi katika utatuzi wa migogoro na kuepuka kusababisha migogoro mipya**.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria za ardhi zimeweka utaratibu wa namna ya kushughulikia migogoro ya ardhi. Pale ambapo mgogoro unashindikana kutatuliwa kiutawala migogoro hiyo hupelekwa katika ngazi ya mahakama kutatuliwa. Kwa kipindi cha miaka minne, Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya kuzuia na kutatua migogoro kwa kushirikiana na wadau. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma, kuimarisha Kituo cha Huduma kwa Wateja, kuimarisha madawati ya malalamiko katika ofisi za ardhi za Halmashauri na Mikoa na kuendeleza programu ya '**Kliniki za Ardhi'**. Kupitia mikakati hiyo, jumla ya migogoro **18,005** ilitatuliwa kwa njia ya kiutawala katika halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 6**).

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji/Mitaa 975**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, Wizara imeratibu utekelezaji wa maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji na Mitaa 975 nchini. Katika kutekeleza uamuzi huo, tathmini imebainisha kuwa vijiji na mitaa yenye migogoro ni **1,004** (vijiji **981** na mitaa **23**) badala ya **975** kama ilivyokuwa imebainishwa hapo awali. Kwa kipindi cha miaka minne, utekelezaji wa Uamuzi wa BLM umekamilika katika vijiji/mitaa **462**. Aidha, utekelezaji unaendelea katika vijiji/mitaa **553** (**Jedwali Na. 7**). Utekelezaji huo umewezesha ardhi yenye ukubwa wa ekari milioni **2.4** kumegwa na kurejeshwa kwa wananchi ikijumuisha ekari milioni **1.65** kutoka kwenye maeneo ya hifadhi, ranchi na mashamba ya Serikali; ekari **707,962** kutoka kwenye Mapori Tengefu **12** na ekari **46,715** kutoka kwenye Hifadhi za Misitu saba (**7**). Pia, mipango ya matumizi ya ardhi

imeandaliwa katika vijiji **195** vya Halmashauri za Wilaya **29**. Vilevile, maeneo **19** kati ya **20** yalifanyiwa uthamini kwa ajili ya kuhamisha wananchi kutoka kwenye maeneo ya Hifadhi na vyanzo vya maji. Kati ya maeneo yaliyofanyiwa uthamini, wananchi wa maeneo **11** wamelipwa fidia kiasi cha shilingi bilioni **85.46** (**Jedwali Na. 8**) na kuimarisha usimamizi wa mipaka ya hifadhi ambapo vigingi **32,838** vimesimikwa na mkuza kuchongwa kuzunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa **21**, Mapori ya Akiba **29** na Hifadhi za Misitu **416**.



*Wataalam wa sekta ya Ardhi wakiwahamasisha wananchi wa Kijiji cha Ngombo, Malinyi mkoani Morogoro wakati wa zoezi la uthamini wa maeneo ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumiazi ya ardhi katika vijiji 975*

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara itaendelea kuratibu ukamilishaji wa utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri katika maeneo yaliyobakia kwa kuendelea kutoa elimu; kuweka alama za kudumu baina ya hifadhi na vijiji kwenye maeneo yaliyomegwa na kurejeshwa kwa wananchi; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na wadau; kuendelea kufanya tathmini na uthamini kwa wananchi watakaopisha shughuli za uhifadhi na kuandaa matangazo ya Serikali katika maeneo ya hifadhi

yaliyomegwa katika Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, Hifadhi za Misitu, Hifadhi za Maji, Mashamba na Ranchi.

**Uthamini wa Mali**

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu, kusimamia na kutoa huduma ya kufanya uthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika kwa madhumuni mbalimbali ikiwa ni pamoja na uthamini kwa ajili ya malipo ya fidia kupisha miradi mbalimbali ya Serikali, uthamini kwa ajili ya mizania ya hesabu za Taasisi za Serikali na Taasisi Binafsi, uthamini kwa ajili ya kuwezesha utozaji wa ushuru wa Serikali kutokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, uthamini kwa madhumuni ya rehani kwa ajili ya kupata mikopo, mirathi, kinga ya bima, utozaji wa kodi ya pango la ardhi na tozo ya mbele ya umilikishaji ardhi (premium).

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuidhinisha taarifa za uthamini **54,000** ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za uthamini zenye wafidiwa **34,000**. Pia, Wizara ilipanga kushughulikia malalamiko **100** yatokanayo na uthamini katika maeneo **30** pamoja na kuimarisha kumbukumbu za uthamini ikiwemo kukamilisha zoezi la uandaaji wa vitalu vya thamani ya ardhi katika mikoa **26**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **54,421** sawa na asilimia **100.78** ya lengo la mwaka ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,122** na taarifa za uthamini wa fidia ni **34,299**. Aidha, malalamiko **65** yalipokelewa na kushughulikiwa. Vilevile, Wizara imeandaa vitalu vya thamani ya ardhi katika Mikoa **19** sawa na asilimia **73** ya lengo la mikoa **26** ambavyo vimeingizwa katika mfumo wa e-Ardhi. Taarifa za vitalu hivyo zitatumika kufanya uthamini, kukokotoa kodi ya pango la ardhi, tozo ya mbele (premium) na kuwezesha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi. Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **97,340** na uthamini wa wafidiwa **153,358**.



*Wataalam wa fani ya Uthamini na Urasimu Ramani wakiwa katika picha ya pamoja na Mthamini Mkuu wa Serikali Bi. Evelyne Mugasha (wa nne kulia) mara baada ya mafunzo ya zoezi la uandaaji vitalu vya thamani ya ardhi (Valuation Blocks) ambayo yalifanyika jijini Dar es Salaam*



*Wathamini wakishiriki zoezi la uthamini wa fidia kwenye Mradi wa Reli ya kiwango cha Kimataifa (SGR) katika Kijiji cha Mpigwa Mkoani Tabora*

49. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi, Wizara imeendelea kuboresha matumizi

ya mfumo katika utoaji wa huduma za uthamini nchini. Taarifa za uthamini katika mikoa **19** zimeanza kuidhinishwa kupitia mfumo wa e-Ardhi. Mikoa hiyo ni Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Kigoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Singida, Manyara, Tanga, Mbeya na Kilimanjaro. Katika mwaka 2025/26, Wizara itatoa huduma za uthamini kupitia mfumo wa e-Ardhi kwa nchi nzima. **Natoa rai kwa Wathamini wote na wadau wote wa uthamini nchini kuhakikisha wanatumia mfumo katika kuwasilisha taarifa za uthamini, kwani kazi zote za uidhinishaji wa taarifa za uthamini zikifanyika kupitia mfumo, mwananchi hatahitajika kufika katika ofisi za ardhi.**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara imepanga kuidhinisha taarifa za uthamini **54,000** ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za uthamini zenye wafidiwa **34,000**. Aidha, malalamiko **100** yatokanayo na uthamini yatashughulikiwa, kukamilisha uandaaji wa vitalu vya thamani ya ardhi kwa mikoa saba (**7**) pamoja na kuimarisha kumbukumbu za uthamini ikiwemo kuendelea na zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa **26**.

**MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA**

51. ***Mheshimiwa* Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216, Wizara ina jukumu la kuanzisha, kusimamia na kuhudumia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi nchini. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kufungua mabaraza mapya **42.** Napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Wizara imeanzisha mabaraza mapya **18** na hivyo kuwa na jumla ya mabaraza **115** yanayofanya kazi. Katika kipindi hicho, Wizara iliahidi kushughulikia mashauri **16,000.** Hadi tarehe 15 Mei, 2025 mashauri **14,090** yalikuwepo na mashauri mapya **12,523** yalifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa **26,613.** Kati ya hayo, mashauri **14,888** yalitolewa uamuzi na mashauri **11,725** yanaendelea kushughulikiwa.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kutoa huduma bora kwa wananchi, katika kipindi cha miaka minne


Wizara imeendelea kusogeza huduma kwa wananchi kwa kuanzisha Mabaraza mapya **67** na hivyo kuwa na jumla ya Mabaraza **115** yanayotoa huduma kati ya Mabaraza **139** yanayohitajika. Kupitia Mabaraza hayo, mashauri mapya **83,529** yalifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa **111,810** ambapo kati ya hayo, mashauri **100,175** yaliamuliwa. Wizara imeendelea kuimarisha Mabaraza kwa kufanya maboresho ya sheria na kuyapatia watumishi na vitendea kazi.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara imepanga kuanzisha Mabaraza mapya **24** ili kukamilisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Wilaya zote **139** nchini. Pia, Wizara itaendelea kushughulikia mashauri **11,725** yaliyobaki na yatakayofunguliwa. Naipongeza Mikoa na Wilaya ambazo zimeendelea kutoa ushirikiano katika uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya nchini. **Natoa wito kwa Mikoa na Wilaya ambazo hazina Mabaraza kuendelea kuwezesha upatikanaji wa majengo ya ofisi na wajumbe ili kuwezesha uanzishwaji wa Mabaraza.**

**HUDUMA ZA TEHAMA**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha miundombinu na mifumo ya TEHAMA kama nyenzo muhimu ya kurahisisha na kuongeza ufanisi katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa taarifa mbalimbali. Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, pamoja na mambo mengine, Wizara imekamilisha usanikishaji wa Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa Huduma za Ardhi (e-Ardhi) ambao ulizinduliwa Jijini Dodoma na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Machi, 2025.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuendelea kuunganisha Mfumo wa e-Ardhi na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidigiti katika maeneo mbalimbali nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeendelea kusambaza Mfumo huu nchini kwa awamu ambapo Mfumo unatumika katika Halmashauri 46 za Mikoa 11 ya Arusha (7), Dodoma (8), Mbeya (7), Shinyanga (2), Mtwara (1), Pwani (1), Tanga (11), Mwanza (6), Ruvuma (1), Kigoma (1) na Tabora (1) ambako kazi ya kubadili nyaraka za taarifa za kijiografia na umiliki wa ardhi kutoka analojia kwenda kidijiti imekamilika.




*Muonekano wa Ukurasa wa Mfumo wa e-Ardhi, 2025*

56. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha upatikanaji na ufanisi wa huduma za TEHAMA, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu wezeshi ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuimarisha Kituo cha Taifa cha Kutunza Kumbukumbu za Ardhi (NLIC) na Kituo cha Kujikinga na Majanga katika mifumo ya TEHAMA. Aidha, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Ofisi za Makao Makuu ya Wizara na Ofisi za Ardhi za mikoa yote **26** na Halmashauri **184** umefanyika. Vilevile, usimamizi wa usalama wa mtandao, elimu na msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mifumo na huduma za TEHAMA vimeendelea kutolewa ili kuongeza uwezo na ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi, taasisi na watumishi.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kusambaza Mfumo wa e-Ardhi katika Halmashauri **18**

za mikoa ya Pwani (**8**) na Morogoro (**10**) pamoja na kuendelea kusafisha na kubadili taarifa za kijiografia na majalada ya umiliki wa ardhi kutoka katika muundo wa analojia kwenda kidijiti ambayo ni hatua muhimu ya usambazaji wa Mfumo huu katika mikoa hiyo. Vilevile, Wizara itakamilisha zoezi la kusafisha na kubadili taarifa za kijiografia na majalada ya umiliki, kusambaza Mfumo wa e-Ardhi, kutoa elimu na kuwajengea uwezo watumiaji na kusimika miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri zote zilizosalia ifikapo mwezi Juni, 2027.

## UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za uwekaji wa alama za msingi; upimaji ardhi wa nchi kavu na ndani ya maji; na utayarishaji wa ramani za msingi, ramani za mipaka ya kiutawala na ramani za matumizi mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya Serikali na shughuli za maendeleo. Wizara imeendelea kutoa miongozo ya upimaji ardhi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu hayo.

### Uwekaji Alama za Msingi za Upimaji Ardhi

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Alama za Msingi za Upimaji (Control Points) na Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji (Continuously Operating Reference Stations - CORS) ni miongoni mwa miundombinu muhimu katika kazi za upimaji ardhi. Wizara inaendelea kuratibu na kuongeza alama za msingi za upimaji na vituo vya kieletroniki vya upimaji katika maeneo mbalimbali nchini ili kurahisisha kazi za upimaji kwa kupunguza muda na gharama za upimaji.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kujenga Alama mpya za Msingi za Upimaji **150** katika Halmashauri mbalimbali nchini pamoja na kuwekeza zaidi kwenye usimikaji wa vituo vya kielektroniki vya upimaji. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, alama za msingi za upimaji **122** sawa na asilimia **81.3** ya lengo zimewekwa katika katika mikoa ya Iringa (**15**), Ruvuma (**13**), Tabora (**10**), Geita (**22**), Kilimanjaro (**20**), Pwani (**22**) na Dar es

Salaam (**20**). Aidha, usanifu wa maeneo ya ujenzi na usimikaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji umekamilika. Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali Awamu ya Sita, alama **710** zimesimikwa na hivyo kuwa na jumla ya alama **1,545** katika maeneo mbalimbali nchini.




*Alama ya Msingi ya Upimaji iliyowekwa Chalinze Mkoa wa Pwani*

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara itaongeza Alama za Msingi za Upimaji **438** pamoja na kukamilisha ujenzi na usimikaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **22** katika Mikoa **20** ya Dodoma, Iringa, Pwani, Kagera, Njombe, Mara, Dar es Salaam, Manyara, Rukwa, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Geita, Katavi, Mwanza, Kigoma, Shinyanga, Singida, Morogoro na Tanga.

**Upigaji Picha za Anga**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** picha za anga ni muhimu kwa ajili ya kupata taarifa za msingi zinazotumika kuandaa ramani za msingi na ramani za matumizi maalum kama vile maendelezo ya miji na hifadhi za misitu. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kupiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **1,000** na kuhuisha ramani za msingi pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu

kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara imepiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **123.89** katika mikoa ya Arusha (**36**) na Dodoma (**87.89**). Aidha, ramani za mipaka ya kiutawala **19** za mikoa ya Manyara, Arusha, Dodoma na Morogoro zimeandaliwa na ramani mbili (**2**) za Halmashauri ya Chamwino na Dodoma zimehakikiwa ardhini. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kupiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **1,000** na kuhuisha ramani za msingi pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali nchini.

**Tafsiri ya Matangazo ya Serikali kuhusu Maeneo ya Utawala (GN)**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** tafsiri ya Matangazo ya Serikali (GN) kuhusu maeneo ya utawala na hifadhi ni suala muhimu katika kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi nchini. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) ya maeneo ya utawala na hifadhi. Tafsiri hizo zinawezesha kutatua migogoro ya mipaka kati ya kijiji na kijiji, wilaya na wilaya, mkoa na mkoa pamoja na vijiji na hifadhi. Katika mwaka 2024/25, Wizara iliahidi kutafsiri matangazo ya mapori tengefu kumi (**10**), hifadhi za taifa tano (**5**) na mipaka ya kiutawala kumi (**10**). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imefanya tafsiri ya matangazo ya maeneo ya mapori tengefu matatu (**3**) na mipaka ya kiutawala sita (**6**).

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, matangazo ya Serikali (GN) **53** yalitafsiriwa kwa ajili ya kubainisha mipaka ya utawala na hifadhi (**Jedwali Na. 9**). Katika mwaka 2025/26, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutafsiri matangazo ya Serikali (GN) **10** ili kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi. **Ili kuondoa migongano na migogoro ya mipaka ya kiutawala, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itaendelea kusimamia na kutoa tafsiri sahihi ya maeneo ya utawala.**

**Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

65. **Mheshimiwa Spika,** upimaji wa ardhi huwezesha kuwa na mipaka iliyotambuliwa kisheria na hivyo kuongeza usalama wa milki, thamani ya ardhi na kuepusha migogoro inayohusiana na mipaka ya ardhi. Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na mamlaka za upangaji na sekta binafsi. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuratibu upimaji na uidhinishaji wa viwanja **500,000** na mashamba **500**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2025, jumla ya viwanja **253,429** na mashamba **1,926** yamepimwa na kuidhinishwa sawa na asilimia **50.69** na **385.2** mtawalia (**Jedwali Na. 10**). Katika kipindi cha miaka minne, jumla ya viwanja **1,476,615** na mashamba **12,577** yamepimwa na kuidhinishwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara imepanga kupima na kuidhinisha viwanja **500,000** na mashamba **500**.




*Shamba Na: 1-828 lililopo eneo F Kijiji cha Msomera Wilaya ya Handeni mkoani Tanga*

**Upimaji wa Mipaka ya Vijiji**

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kupima mipaka ya vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mipaka ya kiutawala. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **100**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, mipaka ya vijiji **213** imehakikiwa na kupimwa sawa na asilimia **213** ya lengo (**Jedwali Na. 11**). Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, mipaka ya

vijiji **974** ilihakikiwa na kupimwa katika Wilaya mbalimbali nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na wadau wa maendeleo kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **100** nchini. **Ninaendelea kuzisisitiza mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kuwa Vijiji vinavyoanzishwa vinapimwa mipaka yake kabla ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali ili kudhibiti migogoro ya mipaka.**

## UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia kazi za upangaji wa miji na uendelezaji makazi nchini. Majukumu mengine ni kusimamia na kuidhinisha mipango ya jumla (Mipango Kabambe), kuidhinisha mipangokina, utangazaji wa maeneo yaliyoiva kwa upangaji, udhibiti wa uendelezaji miji, kusimamia urasimishaji na uboreshaji makazi pamoja na usimamizi na uratibu wa uendelezaji wa nyumba. Utekelezaji wa jukumu hilo hufanyika kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayotolewa ili kuchochea maendeleo endelevu ya ukuaji wa miji na makazi nchini.

### Uboreshaji wa Maeneo Chakavu na Yasiyopangwa Mijini

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha muongo mmoja, Tanzania imeendelea kushuhudia ongezeko la watu na kasi kubwa ya ukuaji wa miji na vijiji hapa nchini. Ongezeko hili linajidhihirisha katika takwimu za Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ambapo kati ya mwaka 2012 na 2022, wakazi wa mijini waliongezeka kutoka watu **13,305,004** hadi **21,539,695** sawa na ongezeko la asilimia **61.8**. Ongezeko hili linaweza kuwa na matokeo hasi iwapo wadau hawatawekeza ipasavyo katika kuhakikisha kunakuwa na ukuaji endelevu wa miji na makazi nchini. Suala la ukuaji wa miji endelevu ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia hilo Serikali inaendelea kuwekeza katika ustawi wa miji kwa kuhakikisha inapangwa na kusimamiwa ipasavyo ili kunufaika na fursa za ongezeko la idadi ya watu.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** kasi ya ongezeko la idadi ya watu mijini imechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa makazi yasiyopangwa ambayo kwa mujibu wa Sensa ya Majengo ya mwaka 2022, makazi yasiyopangwa ni asilimia **67.1**. Hivyo, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 Toleo la mwaka 2023 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 zimehimiza uboreshaji wa makazi chakavu au yasiyopangwa katika maeneo ya miji kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma na miundombinu; kuboresha mandhari ya miji; na kuongeza fursa za kiuchumi na mchango wa maeneo hayo katika pato la Taifa. Kwa kuzingatia takwa hilo la kisera, Wizara inaandaa Programu Maalum ya Uendelezaji Upya wa Maeneo Chakavu katika miji mbalimbali nchini.







*Makangira, Msasani Dar es Salaam. Picha ya chini kushoto inaonesha hali ilivyo sasa uwandani na kulia ni majengo yatakavyokuwa baada ya mradi kukamilika.*

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kasi ya ongezeko la idadi ya watu mijini imechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa makazi yasiyopangwa ambayo kwa mujibu wa Sensa ya Majengo ya mwaka 2022, yamefikia asilimia **67.1**. Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Toleo la mwaka 2023 imehimiza uboreshaji wa maeneo chakavu na yasiyopangwa katika maeneo ya miji. Kwa kuzingatia takwa hilo la kisera, Wizara inaandaa **Programu Maalum ya Uendelezaji Upya wa Maeneo Chakavu** katika miji mbalimbali nchini. Kupitia Programu hii, jumla ya maeneo **111** yenye ukubwa wa hekta **24,309.3** yameainishwa katika mikoa **24** kwa ajili ya kupangwa na kuendelezwa upya ili kuyafanya kuwa na tija kiuchumi na kijamii.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara itatekeleza Programu kwa kuendeleza eneo chakavu moja **(1)** la Makangira lililopo Msasani Dar es Salaam kama eneo la mfano.

**Natoa wito kwa wadau kushiriki kikamilifu katika kufanikisha utekelezaji wa Programu hii ili kuleta mabadiliko ya taswira na mandhari ya miji yetu na manufaa endelevu kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.**

**Urasimishaji Makazi Yasiyopangwa**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** urasimishaji makazi nchini unahusisha kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo yaliyoendelezwa bila kupangwa. Lengo la urasimishaji makazi yasiyopangwa ni kuhakikisha usalama wa milki, kutatua changamoto za migogoro ya ardhi na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya huduma za kijamii na miundombinu ya msingi kwa njia shirikishi. Katika mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi ilipanga kuendelea na zoezi la kurasimisha makazi **500,000** kwa kuyafikia maeneo ambayo yameendelezwa bila kupangwa. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, makazi **190,774** yalirasimishwa katika mikoa **26** (**Jedwali Na. 12**). Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara ilitambua na kurasimisha makazi **1,710,920** katika Halmashauri **169** nchini. Kwa mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia zoezi la urasimishaji wa makazi **200,000** katika Halmashauri mbalimbali nchini.



*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakiwa katika picha ya pamoja na wananchi wa jimbo la Ukonga baada ya kukabidhiwa Hati Milki za Ardhi wakati wa utekelezaji zoezi la ukwamuaji wa urasimishaji katika Mkoa wa Dar es Salaam*

**Uandaaji wa Mipango ya Jumla**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura 355, miji yote inapaswa kuwa na Mipango ya Jumla ili kutoa mwongozo wa ukuaji wa miji hiyo na kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ili kudhibiti uendelezaji holela. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kusimamia na kufuatilia uandaaji wa Mipango ya Jumla ya miji mitano (**5**). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maandalizi ya Mipango ya Jumla minne (**4**) ya Manispaa ya Kahama, Mji wa Mafinga, Mji wa Vwawa (Mbozi) na Kwala (Kibaha) ipo katika hatua mbalimbali. **Natoa wito kwa mamlaka za upangaji kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji na utekelezaji wa mipango ya jumla nchini ili miji yetu iweze kusimamiwa katika uendelezwaji wake na kuleta tija katika matumizi ya ardhi nchini.**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara iliratibu uandaaji na uidhinishaji wa Mipango ya Jumla saba (**7**) katika miji saba (**7**) ya Majiji ya Mbeya na Tanga; Manispaa za Lindi, Morogoro, Mpanda na Moshi; na Mji wa Bagamoyo. Katika mwaka 2025/26 Wizara itaendelea kuratibu, kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalam kwenye Mamlaka za Upangaji kuhusu uandaaji wa Mipango ya Jumla.


**Uandaaji wa Mipangokina**

75. ***Mheshimiwa Spika,*** mipangokina huandaliwa na mamlaka za upangaji kwa lengo la kuelekeza ukuaji na uboreshaji wa makazi, kuhifadhi mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutenga maeneo ya matumizi mbalimbali ikiwemo ya uwekezaji. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, michoro ya Mipangomiji **3,626** yenye jumla ya viwanja **384,312** iliidhinishwa sawa na asilimia **181.3** ya lengo (**Jedwali Na. 13**). Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara ilipokea na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **10,192**

yenye jumla ya viwanja **1,516,309** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha makazi kwenye maeneo kongwe katikati ya miji pamoja na kuwezesha uendelezaji wa maeneo ya fukwe, Wizara ilipanga kuziwezesha Mamlaka za Upangaji kuandaa mipango ya uendelezaji upya maeneo (Re-development Schemes and urban renew) katika maeneo matano (**5**) na mipango kina **25** ya kuendeleza fukwe na visiwa. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 mipangokina **41** imeandaliwa sawa na asilimia **164** ya lengo ili kuwezesha uendelezaji wa fukwe nchini. Vilevile, Wizara imeratibu uandaaji wa mpango wa uendelezaji upya wa eneo la Sinza katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira pamoja na kuendana na miongozo ya kimataifa inayosisitiza uzingatiaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika upangaji miji na ustahimilivu wa miji (urban resilience), Wizara imehuisha Mwongozo wa Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Uendelezaji wa Miji wa mwaka 2007 na kutoa Mwongozo mpya wa mwaka 2025. Mwongozo huo umezingatia mahitaji muhimu katika masuala ya kimazingira, viwango vya upangaji, aina mbalimbali za mipangokina, Mipango ya Jumla na mapendekezo ya namna bora ya kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali inayoibuliwa katika Mipango ya Jumla na mipangokina nchini. **Nazielekeza Mamlaka za Upangaji kutekeleza majukumu ya upangaji na usanifu wa miji nchini kwa kuzingatia Mwongozo ili kuboresha usanifu wa miji yetu.**




*Mpango wa Jumla wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan) wa miaka 20 wa Jiji la Dodoma kuanzia mwaka 2019 - 2039*

**Utangazaji wa Maeneo ya Upangaji Miji**

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutangaza maeneo ya vijiji yanayokua na kufikia sifa ya kupangwa na kuendelezwa kimji kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji, Sura 355. Vigezo vya chini vya kutangaza maeneo hayo ni pamoja na eneo husika kuwa na idadi ya watu wasiopungua **10,000**, uwepo wa huduma za msingi za kijamii kama vile zahanati au kituo cha afya, shule ya msingi, huduma za kiuchumi ikiwemo soko na maduka yasiyopungua matano (**5**). Aidha, eneo lolote linaweza kutangazwa kuwa la upangaji maalum iwapo lina sifa za kipekee au umuhimu wa kiuchumi, kimaendeleo au kimazingira.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 jumla ya maeneo **44** yametangazwa kuiva kwa ajili ya kuendelezwa kimji (**Jedwali Na. 14**). Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Awamu ya Sita, Wizara ilipokea na kutangaza maeneo **462** kuwa maeneo ya upangaji na urasimishaji makazi kutoka katika mamlaka za upangaji. Maeneo hayo yamepandishwa kutoka hadhi ya vijiji na kuwa maeneo ya mipangomiji na yanaendelea kuandaliwa mipangokina kwa ajili ya kuchochea ukuaji endelevu. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipangomiji.

**Usimamizi na Udhibiti wa Uendelezaji wa Miji**

80. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji ni suala mtambuka linalotekelezwa na Wizara kwa kushirikisha mamlaka za upangaji. Kutokana na ongezeko la idadi ya watu nchini, ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, na kukua kwa teknolojia; miji hubadilika na kuhitaji usimamizi katika uendelezaji wake hususan mabadiliko ya matumizi ya ardhi ambayo huidhinishwa na Wizara.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kukagua na kuidhinisha maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka katika Mamlaka za Upangaji **184**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 Wizara ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **423** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka kwa Mamlaka za Upangaji sawa na asilimia **141** ya lengo. Hata hivyo, kumekuwepo na ongezeko la maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwa maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya matumizi ya wazi na umma, jambo ambalo linakinzana na Ibara ya 4.3.9 ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na Kifungu 7(5) (s) cha Sheria ya Mipangomiji, Sura 355 inayozuia kubadilishwa matumizi kwa maeneo ya wazi na maeneo hatarishi. Aidha, Sera hiyo imezuia umilikishaji wa maeneo hayo. Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara ilipokea na kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi **2,070**. Mabadiliko hayo yamewezesha uwekezaji kwenye shughuli za

kiuchumi, upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii, ongezeko la pato la Taifa na uboreshwaji wa taswira ya miji nchini.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka 2025/26, Wizara imepanga kuratibu uidhinishaji wa maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi. **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kusimamia, kutunza na kulinda maeneo hayo kama ilivyoanishwa katika kifungu cha 7(5) (s) cha Sheria ya Mipangomiji, Sura 355 kinachowataka Mamlaka za Upangaji zote nchini kutunza na kuhifadhi maeneo hayo kwa maslahi mapana ya umma na kuchochea ukuaji endelevu wa miji nchini.**

**Usimamizi na Uratibu wa Uendelezaji Nyumba**

83. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba nchini ni jukumu muhimu la Wizara katika kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na makazi bora. Uendelezaji wa nyumba hufanywa na taasisi za umma na sekta binafsi. Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ubunifu na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu; na utoaji wa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Awamu ya Sita, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeweza kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Mathalan, benki za biashara zinazotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zimefikia **31** ambapo zimetoa mikopo ya ujenzi wa nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni **659.3** (**Jedwali Na. 15**). Vilevile, kupitia Tanzania Mortage Refinance Company (TMRC) Serikali imeendelea kuziwezesha taasisi za fedha nchini ili kuweza kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba kwa wananchi na kuwezesha viwango vya riba kwa mikopo ya nyumba kupungua kutoka kati ya asilimia **21 - 24** hadi kufikia kati ya asilimia **15–19.**

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali. Katika mwaka

2024/25, Serikali ilipanga kuwawezesha watumishi wa Serikali **100** kupata mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni **2.2.** Hadi tarehe 15 Mei, 2025, watumishi watano (**5**) walipatiwa mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi milioni **41.5**. Aidha, jumla ya shilingi **519,290,826.34** zimekusanywa kama marejesho kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo. Vilevile, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **1.98** imetolewa kwa watumishi wa Serikali **166**. Aidha, Serikali kwa kutambua umuhimu wa watumishi wa umma kuwa na nyumba, imeongeza kiwango cha mkopo kinachotolewa na Mfuko kutoka shilingi milioni **20** hadi shilingi milioni **40** ili kukidhi ongezeko la gharama za ujenzi wa Nyumba na uhalisia wa sasa wa bei za vifaa vya ujenzi. Kwa mwaka 2025/26, Wizara inatarajia kutoa mikopo kwa watumishi **137** yenye thamani ya shillingi billioni **2.6.**

**Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa katika Uendelezaji Miji na Makazi**

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa yenye lengo la kujenga mahusiano na kubadilishana uzoefu katika usimamizi na uendelezaji miji na makazi. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kusimamia na kuratibu ushirikiano wa taasisi mbalimbali katika uendelezaji wa makazi nchini. Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo:

i) Mkutano kuhusu huduma za jamii, Serikali za Mitaa na Maendeleo ya Miji;

ii) Mkutano kuhusu ubunifu katika ufumbuzi wa changamoto za miji ya baadae;

iii) Kongamano kuhusu kuharakisha utekelezaji wa Agenda Mpya za Miji na Maendeleo endelevu; na

iv) Jukwaa la Miji Afrika kuhusu Agenda ya Afrika (2063) (Afrika Tunayoitaka); na na Mkutano kuhusu Kujenga Miji Stahimilivu na Endelevu (Building Resilient and Sustainable Cities).

87. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imeshiriki katika mikutano **24** ya kimataifa. Mikutano hiyo iliwezesha kujenga uwezo wa kitaalam katika masuala mbalimbali ya uendelezaji miji ikiwemo kuimarisha uwezo wa wataalam katika utekelezaji wa Agenda Mpya za Miji na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Aidha, kufuatia Serikali ya Awamu ya Sita kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, Wizara ilifanikiwa kuingia makubaliano na Shirika la Makazi Duniani ambayo yatawezesha Shirika hilo kuijengea uwezo Tanzania katika masuala ya uendelezaji wa miji na makazi pamoja na kuanzisha ofisi zake hapa nchini ili kurahisisha uratibu wa majukumu yake.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa Tanzania kwenye mikutano hii licha ya kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi nyingine duniani, umekuwa ni jukwaa la kujifunza na kupata uzoefu katika kutekeleza Agenda Mpya ya Miji (New Urban Agenda) ambayo inatekelezwa na nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kusimamia na kushiriki mikutano ya kimataifa ikiwemo shughuli za Shirika la Makazi Duniani kwa lengo la kuimarisha Diplomasia katika sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi nchini.

## USIMAMIZI NA URATIBU WA SEKTA YA MILKI

89. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia, kuratibu, na kukuza Sekta ya Milki nchini kwa lengo la kuhakikisha soko la milki linakuwa imara na lenye uwazi ili kulinda maslahi ya wadau, ikiwa ni pamoja na wamiliki, wawekezaji na watumiaji. Kwa mujibu wa Taarifa ya Ukuaji wa Uchumi iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwezi Januari 2025, Sekta ya Milki nchini imekuwa kwa asilimia **4.3** na imechangia asilimia **2.7** katika pato la taifa kwa mwaka 2024.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usimamizi wa sekta ya milki, katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kukamilisha uandaaji wa Sheria na kanuni za kusimamia Sekta ya Milki, kutoa elimu kwa wadau na kuandaa kanzidata ya waendelezaji milki pamoja na mawakala wa Milki. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, jumla ya Mawakala

wa Milki **147** wamejisajili katika kanzidata ya Wizara. Vilevile, Wizara iliratibu mikutano mitatu (**3**) ya wadau wa Sekta ya Milki iliyofanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha ikiwa na lengo la kuwatambua na kutoa elimu kuhusu uanzishwaji wa vyama vya mawakala wa milki na kujadili namna bora ya utekelezaji wa shughuli zao.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imeanzisha na kuboresha Kitengo cha Milki ili kiweze kusimamia kikamilifu sekta ya milki. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilisha andiko la mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki; kutoa ushauri wa kitaalam kwa wadau mbalimbali wa sekta ya milki; kutoa elimu kwa umma kupitia mikutano sita (**6**) ya wadau na maonyesho mbalimbali ya kitaifa; na kuratibu uanzishwaji wa vyama vya mawakala wa milki katika mikoa mitatu (**3**). Aidha, Wizara imeshiriki mikutano mitano (**5**) ya kikanda na kimataifa inayolenga kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ya milki nchini.



*Afisa Mthamini Mwandamizi kutoka Kitengo cha Milki Wilson Waitara akitoa elimu kwa wadau kuhusu utambuzi na usajili wa wadau wa Sekta ya Milki nchini*

92. ***Mheshimiwa Spika,*** mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki yameandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka ya uamuzi.

Mapendekezo haya yanalenga kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Milki (Real Estate Regulatory Authority) ambayo pamoja na mambo mengine, itakuwa na jukumu la kuunda mfumo madhubuti wa usimamizi wa sekta ya milki; wataalam na wadau wa sekta ya milki; kutoa taarifa sahihi za wadau na soko la milki; kuongeza ufanisi wa wataalam wa sekta; na kudhibiti uhalifu wa utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara imepanga kuratibu ukamilishaji wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki; kukamilisha kanuni na miongozo ya uendelezaji milki; kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya milki; na kuhuisha kanzidata ya mawakala wa milki na waendelezaji milki nchini. **Natoa wito kwa wadau wote wa sekta ya milki kuhakikisha kuwa wanatambuliwa na Serikali ili kuimarisha ushirikiano na ukuaji endelevu wa sekta kiuchumi.**

## MAPITIO YA SHERIA ZA SEKTA YA ARDHI

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya Sheria na Kanuni mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi. Katika kutekeleza maelekezo ya Serikali kuwa sheria zote ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili, Wizara imefanya mapitio ya sheria **14** za sekta ya ardhi na kuandaa rasimu za tafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216 na Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Sura 426 zilifanyiwa marekebisho. Lengo la marekebisho hayo ni kuzifanya sheria kueleweka kwa wananchi wengi; kuruhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa mashauri, uandishi wa hukumu na kumbukumbu za mashauri; kuongeza wigo wa madaraja na sifa za usajili kwa wataalam wa mipangomiji; na kuboresha mfumo wa ajira za Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutoka ajira za mkataba kuwa ajira za kudumu hivyo kuboresha utendaji, kuongeza uwajibikaji, kuwezesha wananchi kupata huduma kwa wakati na kupunguza gharama.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza gharama za umilikishaji wa ardhi na kuwawezesha wananchi kuwa na milki salama za ardhi, Kanuni za Ada ya Ardhi (The Land (Fees) (Amendment) Regulations, 2023) zilifanyiwa marekebisho kwa kupunguza Tozo ya Malipo ya Mbele (Premium) kwa asilimia **50** kutoka asilimia **0.5** hadi asilimia **0.25** ya thamani ya ardhi; gharama ya maombi ya Hatimiliki kwa asilimia 75 kutoka shilingi **20,000** hadi shilingi **5,000;** na gharama ya maombi ya kuandaa Hatimiliki kwa asilimia **50** kutoka shilingi **50,000** hadi shilingi **25,000**. Aidha, Kanuni za Usajili wa Ardhi (The Land Registration (Amendment) Rules, 2023) zilifanyiwa marekebisho ambapo Ada ya Usajili wa Hatimiliki imepunguzwa kutoka asilimia **20** hadi asilimia **10** na Kanuni za Ujumla za Upimaji Ardhi (The Land Survey (General) (Amendment) Regulations, 2023) zilifanyiwa marekebisho kwa kufuta Ada ya Ramani ya Hatimiliki (Deed Plan) ambayo kabla ya marekebisho ilikuwa ni shilingi **20,000**. Marekebisho hayo yamechangia kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi na wigo wa makusanyo yanayotokana na sekta ya ardhi.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa Serikali inakusanya madeni yanayotokana na kodi ya pango la ardhi, Wizara iliandaa Kanuni za Msamaha wa Riba ya Malimbikizo ya Kodi ya Pango la Ardhi. Kanuni hizi zimewezesha madeni ya msingi ya kodi ya pango la ardhi kukusanywa hivyo kuongeza mapato ya Serikali. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kufanya marekebisho ya sheria za sekta ya ardhi kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) na mahitaji ya kisiasa, kijamii, kimazingira na kiuchumi.

## MIRADI YA MAENDELEO

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP); Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI); na Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa.

**Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

98. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi lengo likiwa ni kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini. Katika mwaka 2024/25 jumla ya viwanja **12,303** vimepangwa na kupimwa katika Halmashauri **10** nchini. Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imepokea shilingi bilioni **64.5** kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika Halmashauri **131** ikiwemo shilingi bilioni **50** zilizokopeshwa kwenye Halmashauri **57** kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund (PDRF). Kati ya Halmashauri hizo, Halmashauri **24** na Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa zimekamilisha marejesho na Halmashauri **33** hazijakamilisha **(Jedwali Na. 16)**. Fedha hizo zimewezesha upangaji na upimaji wa viwanja **556,191**. Katika Mwaka 2025/26 Wizara itapanga na kupima viwanja 15,000 kupitia Programu ya KKK.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara iliahidi kubuni na kusanifu miji ya pembezoni (Satellite Cities) miwili katika majiji ya Dodoma (Msalato) na Arusha (Samia Afcon City) ili kuwa na miji nadhifu na kudhibiti makazi holela. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imekamilisha usanifu wa eneo la Mradi wa *Samia Afcon City* uliopo katika Jiji la Arusha wenye ukubwa wa ekari **4,555**. Aidha, Wizara inaendelea na uthamini wa ardhi na mali katika Mradi wa Msalato awamu ya Pili ambapo zoezi la uthamini litakapokamilika, usanifu utafanyika ili kuwa na mji ambao ni nadhifu wenye kuakisi mahitaji halisi ya Jiji la Dodoma. Katika mwaka 2025/26, Programu ya KKK itawezesha utekelezaji wa miradi inayohusisha utwaaji wa maeneo na uboreshaji wa miji iliyochakaa katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya.




*Mpango Kina wa eneo la Mradi wa Samia Afcon City uliopo katika Jiji la Arusha*

100. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na uendelevu wa Programu ya KKK, Serikali ya Awamu ya Sita ilihuisha Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund - PDRF) ambapo vyanzo vya fedha za Mfuko vinatokana na marejesho ya fedha za mkopo zilizotolewa kwa Halmashauri mbalimbali nchini na mauzo ya viwanja kupitia miradi ya KKK inayotekelezwa. Aidha, katika kuhakikisha kuwa Mfuko wa PDRF unasimamiwa ipasavyo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Usimamizi na Utekelezaji wa Mfuko ambao unabainisha vigezo vya ukopeshaji na urejeshaji. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mfuko na kuhakikisha unatumika kwenye miradi yenye tija. **Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 50 kwa ajili ya Mfuko wa PDRF ambao umeendelea kuwezesha ongezeko la kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini.**

**Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)**

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara kupitia mradi wa uboreshaji usalama wa Miliki za Ardhi ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji, kutoa vyeti vya vijiji na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **1,000**. Aidha, Wizara kupitia Mradi huu ilipanga kuandaa mipangokina ya vijiji **100** na kuandaa Hati za Hakimiliki za Kimila **300,000**. Vilevile, Wizara ilipanga

kurasimisha makazi **500,000** kupitia wataalam wa Serikali na kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji nchini, kusanifu na kusimika Vituo vya kieletroniki vya upimaji (CORs) 22, kujenga majengo ya ofisi za ardhi katika mikoa **25** na madarasa manne (**4**) katika vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro. Pia, Wizara ilipanga kuwezesha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kupunguza mrundikano wa mashauri **5,000** kati ya mashauri **14,090** yaliyokuwepo, kuwezesha ukamilishaji wa baadhi ya sera, sheria na kanuni, kukamilisha ununuzi wa magari **52** na kukwamua urasimishaji wa makazi katika Jiji la Dar es Salaam.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa vituo **22** vya kielektroniki vya upimaji ardhi ambapo usanifu umekamilika na ujenzi wa vituo unaendelea, kukwamua urasimishaji katika Jiji la Dar es Salaam (makazi **29,685**) na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali (makazi **27,051**); kukusanya taarifa za thamani za ardhi na kuandaa vitalu vya thamani ya ardhi kwa nchi nzima; kubadili kumbukumbu za ardhi kutoka mfumo wa analojia kwenda mfumo wa kidijiti; kukamilisha kazi za urasimishaji maeneo mbalimbali mijini na vijijini; ununuzi wa magari **52**, samani na vitendea kazi vya ofisi; pamoja na marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sheria na Kanuni mbalimbali. Aidha, mradi umewezesha usikilizaji na utolewaji wa maamuzi ya mashauri **3,435** ya muda mrefu yaliyokuwepo katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kati ya mashauri **5,000** yaliyopangwa kusikilizwa.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara kupitia mradi huu imefanikisha uhakiki wa mipaka ya vijiji **871** na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **846** katika Halmashauri **21** (**Jedwali Na. 17**). Aidha, jumla ya vipande vya ardhi **583,734** vimehakikiwa na vimepandishwa katika mfumo wa e-Ardhi. Vilevile, Hati za Hakimiliki za Kimila **318,868** zimesajiliwa katika vijiji **236** vya Wilaya sita (**6**) za Songwe (**66,631**), Chamwino (**47,514**), Mufindi (**52,497**), Mbinga (**67,805**), Maswa (**58,560**) na Tanganyika (**25,861**). Mradi huu pia umewezesha urasimishaji wa makazi **192,865** katika Jiji la Dar es Salaam (makazi **29,685**) na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali (makazi **27,051**), Halmashauri za Jiji la Dodoma (**7,587**); Wilaya za Chalinze (**24,730**), Songea

(**18,840**); Manispaa za Kahama (**21,519**), Shinyanga (**25,768**), Kigoma (**6,171**) na Mtwara (**11,905**); na Mji wa Nzega (**19,609**); uwekaji wa Alama za Msingi za Upimaji **427** katika Halmashauri **35**; kuanza ujenzi wa vituo **22** vya kielekroniki vya upimaji ardhi na uandaaji wa mfumo wa kidijiti wa vitalu vya thamani nchini. Vilevile, Mradi umewezesha Halmashauri **13** kutumia mfumo wa e-Ardhi, hivyo kuboresha usimamizi wa taarifa za ardhi na utoaji huduma kwa njia ya kidijiti. Pia, Mradi umewezesha upatikanaji wa vitendea kazi yakiwemo magari **70** kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za ardhi.



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndejembi (kulia) akimkabidhi magari Mhe. Deogratius, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya utoaji huduma za Sekta ya Ardhi nchini*

Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani

104. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeiwezesha Wizara kupata Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI) wenye thamani ya Dola za kimarekani milioni **65**. Mradi huu unalenga kuimarisha miundombinu ya upimaji na ramani kwa kujenga Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **30**; kununua ndege maalum ya upigaji wa picha za anga; na ununuzi wa vifaa vya upimaji. Utekelezaji wa mradi huu utaongeza kasi ya upangaji na upimaji ardhi sambamba na kuimarisha matumizi ya ramani hizo katika utekelezaji wa miradi ya Serikali. Ramani za msingi zitaandaliwa kwa uwiano wa **1:2,500** katika miji mikuu ya mikoa na uwiano wa **1:25,000** kwa nchi nzima.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa LDI kwa kukamilisha ununuzi wa vifaa na kuanza uandaaji wa ramani za msingi za uwiano wa 1:2,500 kwa miji mikuu ya mikoa na uwiano wa 1:25,000 kwa nchi nzima. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara imempata mshauri elekezi ambaye ameshirikiana na wataalam wa ndani kukamilisha kazi za usanifu wa mradi, kuandaa viwango vya makadirio ya gharama za mradi pamoja na kuandaa zabuni za ununuzi wa ndege maalum ya kupiga picha za anga na zabuni ya mkandarasi wa kutekeleza mradi. Hatua hii itaiwezesha Wizara kukamilisha kazi ya ununuzi wa vifaa na kumpata Mkandarasi wa uwekaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji na uandaaji wa Ramani za Msingi. Katika mwaka 2025/26, Wizara itakamilisha ununuzi wa vifaa pamoja na kumpata mkandarasi wa kuanza uwekaji wa vituo vya kielektroniki na kuanza uandaaji wa ramani za msingi za uwiano wa 1:2,500 kwa miji mikuu ya mikoa na uandaaji wa Ramani za Msingi za uwiano wa 1:25,000 kwa nchi nzima.




*Mtaalam wa kurusha ndege kwa ajili ya kupiga picha za anga akijiandaa kurusha ndege kuchukua taarifa za kijiografia kwa ajili ya kuchakata na kuandaa ramani*

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mradi huu unatekelezwa ipasavyo, Wizara imeanzisha Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mafunzo ya Teknolojia ya Taarifa za Kijiografia (TNGC) kwa ajili ya kujenga uwezo katika matumizi ya teknolojia ya

mifumo ya taarifa za kijiografia na kumbukumbu za ardhi. Kituo hicho kitaongeza uwezo wa wataalamu wa ndani kutekeleza miradi ya sekta ya ardhi na hivyo kuokoa matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuajiri wataalam kutoka nje ya nchi. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, watalaam **10** wamepata mafunzo ya ukurufunzi nchini Tanzania na Korea Kusini. Aidha, kwa kutumia wakufunzi wa ndani, jumla ya wataalam **31** kutoka Halmashauri za Wilaya za Chamwino, Bahi, Mafia, Jiji la Dodoma, Ofisi za Ardhi Mkoa wa Dodoma, na taasisi nyingine za Serikali ikiwemo TARURA na NBS wamepata mafunzo ya kujengewa uwezo katika kuchukua taarifa za kijiografia kwa kutumia ndege zisizo na rubani, kuchakata na kuandaa ramani. Katika mwaka 2025/26, Kituo cha TNGC kitaanza kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Mifumo ya Kijiografia (GIS) na mafunzo ya kozi za muda mfupi katika matumizi ya ndege zisizokuwa na rubani (drones) kwa ajili ya uchukuaji wa taarifa za kijiografia.





*Wadau wa Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI) walipotembelea Kituo cha Ubunifu na Mafunzo ya Kijiografia (TGNC) kilichopo eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wakati wa semina ya wadau hao iliyofanyika jijini Dodoma*

**Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa**

107. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya kimataifa kwa kujenga na kuongeza alama, kuzipima, kukarabati zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa makubaliano ya uimarishaji wa mipaka. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuimarisha sehemu ya mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita **100** pamoja na mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilomita **100**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara iliendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya kwa kufanya ukokotozi wa vipimo kwa ajili ya kupata majira nukta ya mpaka kwa kipande cha kilomita **110** kutoka Namanga hadi Tarakea, kufanya ukaguzi wa mpaka wa Tanzania na Zambia, mpaka wa Tanzania na Burundi pamoja na kuandaa mpango kazi wa uimarishaji wa mipaka hiyo.



*Kamati ya Pamoja ya Wataalamu ya Uimarishaji Mpaka wa Tanzania na Burundi (JTC) wakikagua eneo la Mto Malagarasi ambao ni sehemu ya mpaka wa nchi hizo*

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, jumla ya kilometa **268** zimeimarishwa na kufanya jumla ya kilomita zilizoimarishwa kufikia **458** kati ya kilomita **758** za nchi kavu katika mpaka kati ya Tanzania na Kenya kwa kuweka alama, vipimo na kuandaa ramani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uimarishaji mipaka imefanya ukaguzi wa mpaka wa Tanzania na Kenya, Tanzania na Zambia, Tanzania na Burundi na Tanzania na Msumbiji. Katika mwaka 2025/26, Wizara imepanga kuendelea kuimarisha sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **100** kutoka Tarakea Wilaya ya Rombo hadi Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi Wilaya ya Mwanga na sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita **100** kutoka Kijiji cha Kagunga Wilaya ya Kigoma hadi Manyovu Wilaya ya Buhigwe Mkoa wa Kigoma.

## USHIRIKI WA WIZARA KATIKA MIRADI YA KIMKAKATI NA MATUKIO YA KITAIFA

109. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imeshiriki katika miradi ya kimkakati ambayo ni ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga Tanzania na ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR). Vilevile, Wizara ilishiriki kwenye matukio mbalimbali ya

kitaifa ikiwemo utwaaji, uthamini, upangaji upimaji na umilikishaji wa ardhi kwa ajili ya waathirika wa maporomoko ya mlima Hanang' mkoani Manyara na wananchi wanaohama kwa hiari kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwenda wilayani Handeni na Kilindi mkoani Tanga na Simanjiro mkoani Manyara.

**Upangaji na Upimaji wa Viwanja Mbadala kwa Ajili ya Waathirika wa Maporomoko ya Mlima Hanang'**

110. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na maafa ya maporomoko ya sehemu ya Mlima Hanang', katika Wilaya ya Hanang' yaliyotokea tarehe 3 Desemba, 2023, Wizara ilishiriki katika kupanga na kupima viwanja mbadala kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za waathirika wa maporomoko hayo. Jumla ya viwanja **269** vilipangwa, kupimwa na kumilikishwa kwa ajili ya matumizi ya makazi (**235**), makazi na biashara (**15**), biashara (**7**) na huduma za jamii (**12**).



*Mhe. Geophrey Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi akikagua eneo ambalo Wizara ilishiriki katika zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa waathiriwa wa maporomoko ya udongo wa Mlima Hanang' mkoani Manyara*



*Makazi mapya ya waathiriwa wa maporomoko ya udongo wa Mlima Hanang' mkoani Manyara baada ya ujenzi kukamilika*

**Uhamaji wa Hiari wa Wananchi Kutoka katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika zoezi la wananchi kuhama kwa hiari kutoka Hifadhi ya Ngorongoro, Wizara ilishiriki kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa ajili ya makazi, kilimo na ufugaji. Kazi hii imefanyika katika vijiji vya Msomera (Handeni) na Saunyi na Lengusero (Kilindi) katika Mkoa wa Tanga na Kitwai B (Simanjiro) Mkoa wa Manyara ambapo mashamba **8,581** na viwanja **5,570** vimepimwa. Aidha, eneo la malisho lenye ukubwa wa takriban hekta **22,000** lililopo katika Wilaya za Handeni na Kilindi limebainishwa.

**Uthamini wa Mali za Wananchi katika Maeneo ya Miradi ya Kimkakati**

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshiriki kufanya uthamini wa mali za wananchi katika maeneo ya miradi mikubwa ya kimkakati. Miradi hiyo inajumuisha Miradi ya Reli ya Kati kwa Kiwango cha

Kimataifa (SGR) awamu ya Tatu hadi awamu ya Sita, miradi ya umeme kwa ajili ya Reli ya Kisasa (SGR), miradi ya Barabara, miradi ya Umeme, miradi ya maji na uthamini wa mali za wananchi wanaohama kwa hiari kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera na Mradi wa *Samia Afcon City*, Arusha. Katika Miradi hiyo jumla ya wananchi **65,332** wamefanyiwa uthamini wa mali zao zenye thamani ya shilingi bilioni **673.6**.

## USIMAMIZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA


113. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa majukumu ya Wizara ni kuratibu na kusimamia shughuli za taasisi zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini, Baraza la Taifa la Wapima Ardhi na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

### Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeendelea kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini; kufanya tafiti zinazohusiana na matumizi ya ardhi; na kufanya ufuatiliaji, tathmini na uzingatiaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Majukumu yote hufanywa kwa kuzingatia Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura 116; Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Taifa (20132033); na Mpango Mkakati wa Tume (2021/22 – 2025/26).

115. ***Mheshimiwa Spika,*** upangaji wa matumizi ya ardhi ni muhimu kwa ajili ya matumizi endelevu ya rasilimali ardhi kwa kuzingatia ongezeko la watu, mifugo na mahitaji mbalimbali kama ardhi ya kilimo, malisho na makazi; usalama wa milki za ardhi; na kudhibiti migogoro ya ardhi nchini. Mipango hii huwezesha utengaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji, uwekezaji na makazi ili kuepuka muingiliano wa kimatumizi yakiwemo maeneo ya shoroba na maeneo ya mazalia ya wanyamapori, vyanzo vya maji, misitu ya

hifadhi, mapori tengefu na mapori ya akiba, Ardhi ya uwekezaji na malisho ambayo huandaliwa katika ngazi mbalimbali za Taifa, Kanda, Mikoa, Wilaya na Vijiji.




*Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa kijiji cha Msomera, Handeni Mkoa wa Tanga unaoonesha matumizi mbalimbali ya ardhi*

116. ***Mheshimiwa Spika,*** uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji hutanguliwa na uhakiki wa mipaka na utatuzi wa migogoro katika vijiji husika. Katika mwaka 2024/25, Tume ilipanga kuhakiki mipaka ya vijiji **240** na kutatua migogoro ya mipaka pale inapojitokeza. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 migogoro ya mipaka ya vijiji **242** imetatuliwa katika Halmashauri za Wilaya **23** ambazo ni;- Busokelo (**8**), Mbarali (**11**), Nzega (**19**), Kaliua (**2**), Urambo (**2**), Sikonge (**4**), Mlele (**6**), Rombo (**23**), Buhigwe (**5**), Nyasa (**12**), Morogoro (**11**), Mbogwe (**25**), Sumbawanga (**6**), Kibiti (**4**), Kilolo (**7**), Korogwe (**16**), Kilindi (**20**), Ushetu (**9**), Manyoni (**5**), Mpimbwe (**16**), Ukerewe (**11**) Mtwara (**18**) na Bahi (**2**). Chanzo cha migogoro hiyo ilibainika kuwa ni mwingiliano wa matumizi ya ardhi na uvamizi wa wananchi katika maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori; vyanzo vya maji na maeneo ya Misitu ya Hifadhi, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu; na mgawanyiko wa Vijiji (**Jedwali Na.18**). Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Tume imehakiki mipaka ya kiutawala na kutatua migogoro katika

vijiji **514**. Kwa mwaka 2025/26, Tume itaendelea kutatua migogoro ya ardhi kwa kushirikiana na wananchi, wadau wa kimkakati na Mamlaka za Upangaji.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Tume ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **422**, wilaya tano (**5**), mikoa mitatu (**3**) na kanda moja (**1**) kwa kushirikiana na wadau. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2025, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **220** katika Halmashauri za Wilaya **20** nchini imeandaliwa. Aidha, kutokana na umuhimu wa mipango ya matumizi ya ardhi, Serikali iliongeza bajeti ya shilingi bilioni tano (**5**) kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **333** katika Halmashauri **21**. Ongezeko hili la bajeti, limewezesha vijiji **114** kupangwa na kufanya jumla ya vijiji vilivyopangwa hadi tarehe 15 Mei, 2025 kufikia **334** (**Jedwali Na. 19**). Vilevile, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **219** inaendelea kuandaliwa na itakamilika Juni, 2025, hivyo kuwa na jumla ya vijiji **4,679** vilivyopangwa nchini kati ya Vijiji **12,333**. **Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa maoni na ushauri ambao umewezesha kuongezeka kwa kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini.**

118. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji, mpango wa matumizi ya ardhi wa wilaya moja **(1)**, mikoa mitatu (**3**) pamoja na mpango wa ukanda mmoja (**1**) iliandaliwa. Mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji iliyoandaliwa imewezesha utengaji wa maeneo yenye ukubwa wa hekta **1,255,487.1** kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo (hekta **717,303**), uwekezaji (hekta **6,485.1**), Hifadhi ya Misitu ya Kijiji (hekta **87,402.9**), makazi (hekta **109,340**), vyanzo vya maji (hekta **34,008.1**) na malisho (hekta **61,113.6**). Aidha, matumizi mengine yaliyotengwa ni hifadhi za barabara, umeme na reli, huduma za jamii, bomba la gesi, ardhi oevu, maeneo ya usimamizi wa wanyamapori, makazi na kilimo yenye jumla ya hekta **239,834.40**.



*Mhandisi Anthony Sanga, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (wa nne kushoto) akipata maelezo kuhusu zoezi la upimaji wa mipaka ya vijiji na mashamba kwa kutumia Vifaa vya Kisasa katika Mkoa wa Njombe*

119. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, idadi ya mipango ya matumizi ya ardhi imeongezeka kutoka vijiji **2,088** hadi vijiji **4,679.** Ongezeko hili limetokana na jitihada za Serikali na mwitikio wa wadau uliochangiwa na mazingira wezeshi yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita hususan kuendelea kuimarika kwa uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya kiuchumi. Aidha, mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya **11**, mikoa mitatu (**3**) pamoja na mpango wa ukanda mmoja (**1**) iliandaliwa. Mipango iliyoandaliwa imewezesha utengaji wa maeneo yenye ukubwa wa hekta **528,438.1** kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo kilimo (hekta **379,437**), uwekezaji (hekta **5,578.2**), Hifadhi ya Misitu ya Kijiji (hekta **39,982.3**), makazi (hekta **66,582.2**), vyanzo vya maji (hekta **15,470.7**) na malisho (hekta **21,387.7**). Mipango hii imewezesha kuibua fursa zinazotokana na shughuli za utalii, kilimo, mifugo, viwanda na uwekezaji. Vilevile, imewezesha uhifadhi wa mazingira, vyanzo vya maji na uimarishaji wa miundombinu mikubwa ikiwemo viwanja vya ndege, usafiri wa majini na reli ya kisasa inayounganisha miji ya kibiashara na maeneo ya utalii. Katika mwaka 2025/26, Tume itaendelea kuratibu na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **240** kwa kushirikiana na wadau nchini. **Natoa Rai kwa wananchi kuzingatia kikamilifu mipango ya matumizi ya ardhi iliyoandaliwa katika maeneo yao. Aidha, nazihimiza Halmashauri**

**za Wilaya kutenga fedha za uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi**.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea na jukumu la kuwezesha uandaaji wa mipangokina ya vitovu vya vijiji na maeneo ya mashamba ili kuwezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila. Katika mwaka 2024/25, Tume ilipanga kuandaa mipangokina **40** ambayo inawezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **8,200** katika maeneo ya makazi na mashamba. Hadi tarehe 15 Mei, 2025 jumla ya mipangokina ya vijiji 11 imeandaliwa kwenye maeneo ya mashamba na makazi katika Halmashauri za Wilaya Nane (**8**) nchini. Kuandaliwa kwa mipangokina hiyo kumewezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **5,499** katika Wilaya za Bahi (**360**), Rombo (**390**), Mlele (**223**), Shinyanga (**429**), Mbarali (**351**), Kilolo (**359**), Mbogwe (**328**) na Songwe (**3,059**). Kwa mwaka 2025/26, Tume itaendelea kuwezesha uandaaji wa mipangokina ya vijiji nane (**8**) katika maeneo ya makazi na mashamba ambayo itawezesha utoaji wa Hati za Hakimilki za Kimila **2,500**.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Tume imewezesha uandaaji wa mipangokina ya vijiji **123** katika Halmashauri za Wilaya **31**. Mipangokina hiyo imewezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **38,243** katika maeneo ya vitovu vya vijiji na maeneo ya mashamba. Hati hizi zimewezesha kuongeza usalama wa milki za ardhi, thamani ya ardhi, kupunguza migogoro ya ardhi, kutumika kama dhamana ya mikopo kwenye taasisi za kifedha, kulinda maeneo ya huduma za jamii na kuimarisha uwekezaji mbalimbali.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Tume ilipanga kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji **422** katika ngazi za Wilaya na Vijiji na kutoa elimu kuhusu sheria za ardhi, miongozo na taratibu za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Vilevile, elimu kuhusu usuluhishi wa migogoro ya ardhi, uhifadhi wa mazingira, maeneo ya mapitio ya wanyamapori, vyanzo vya maji na uzingatiaji wa maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mbalimbali na utunzaji wa misitu ili kusaidia katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Hadi tarehe 15

Mei, 2025, Tume imezijengea uwezo Mamlaka za upangaji **361** ambazo ni Halmashauri za Vijiji **334** na Halmashauri za Wilaya **27** juu ya uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Jumla ya wajumbe **15,345** walijengewa uwezo katika kamati mbalimbali ambazo ni; Kamati ya Usimamizi ya ardhi ya Wilaya (**216**); Hamashauri za Vijiji (**7,682**); Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Vijiji (**2,672**); Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji (**2,338**); Wajumbe wa Kamati za Uhakiki wa Mipaka (**2,338**); na Kamati ya Uhakiki wa Maslahi ya ardhi (**99**).

123. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Tume imezijengea uwezo Mamlaka za Upangaji za Wilaya **99**, Mamlaka za Vijiji **2,591** kwa ajili ya uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Jumla ya wajumbe **118,494** walijengewa uwezo katika kamati mbalimbali ambazo ni Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Wilaya (**792**); Hamashauri za Vijiji (**59,593**); Kamati ya Usimamizi wa ardhi ya Vijiji (**20,728**); Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji (**18,137**); Kamati za Uhakiki wa Mipaka (**18,137**); na Kamati ya Uhakiki wa Maslahi ya Ardhi (**1,107**).

**Tafiti Zinazohusiana na Matumizi ya Ardhi**

124. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, Tume imefanya tafiti mbalimbali zinazohusu usimamizi wa uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi; mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya ardhi na uoto; tathmini ya matumizi ya ardhi na mazingira kwa yaliyokuwa makazi ya wakimbizi ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu katika mikoa ya Katavi na Tabora; na athari za kukua na kupanuka kwa miji na maendeleo ya vijiji. Matokeo ya tafiti hizi yamesaidia kuboresha utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi; uzingatiaji wa athari za mabadiliko ya tabianchi; kuishauri Serikali kuhusu mgawanyo wa rasilimali za ardhi; uhuishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi; maboresho ya kisera, kisheria, kimiongozo na kimkakati. Aidha, tafiti zimesaidia kujenga uelewa wa wadau kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi.

## Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

125. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Tume imeendelea kufanya ufuatiliaji, tathmini na ukaguzi wa uzingatiaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **120** katika Halmashauri za Wilaya 15 za Uyui (**8**), Buhigwe (**8**), Misungwi (**8**), Muheza (**8**), Kilosa (**8**), Mpwapwa (**8**), Mbarali (**8**), Makete (**8**) Bukoba (**8**), Shinyanga (**8**), Mufindi (**8**) Rufiji (**8**), Meatu (**8**), Iramba (**8**) na Tunduru (**8**). Lengo lilikuwa ni kukagua uzingatiaji wa matumizi kwa maeneo yaliyotengwa.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yalionesha kuwa mipango ya matumizi ya ardhi imesaidia kutatua migogoro ya ardhi kwa asilimia **69.1**; utunzaji wa mazingira katika kuchochea agenda ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa asilimia **71.9**; na uendelezaji wa maeneo yaliyotengwa kwa asilimia **80** hususan kwenye maeneo ya huduma za jamii, makazi, kilimo na miundombinu katika maeneo yaliyopitiwa na miradi ya kimkakati ya SGR, EACOP na Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP). Aidha, jitihada zaidi zitaendelea kufanyika katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho na misitu ya hifadhi ya vijiji ili yaweze kuendelezwa kama yalivyopangwa. Katika mwaka 2025/26, Tume itaendelea kufanya ufuatiliaji, tathmini na ukaguzi wa uzingatiaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **60** katika maeneo mbalimbali nchini.

## SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika lina jukumu la kujenga nyumba za makazi na majengo mengine kwa ajili ya kuuza na kupangisha; kujenga majengo kulingana na mipango iliyoidhinishwa na Serikali; kuzalisha na kuwezesha uzalishaji wa vifaa vya ujenzi; kusimamia milki za majengo; kufanya ukarabati wa nyumba; kukusanya kodi ya pango la nyumba za Shirika; kutoa huduma ya ushauri elekezi; na upangaji wa maeneo na ukandarasi wa majengo. Majukumu hayo yanatekelezwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka 11 (2015/16 – 2025/26).

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba nchini. Katika kipindi cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Shirika limejenga nyumba **5,399** zenye thamani ya shilingi bilioni **659.48** kwa ajili ya kuuza na kupangisha ambapo nyumba **3,217** ujenzi wake umekamilika na nyumba **2,182** ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2026. Aidha, kati ya nyumba zilizokamilika nyumba **852** ni kwa ajili ya ofisi na biashara, nyumba **1,317** kwa ajili ya makazi na biashara na nyumba **1,048** ni za makazi pekee.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia mwaka 2018, miradi mikubwa mitatu (3) iliyoko katika Jiji la Dar es Salaam yenye jumla ya nyumba **2,633** ilisimama kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Shirika kuchelewa kupata kibali cha kukopa. Ili kukwamua miradi hiyo, mwaka 2023, Serikali ya Awamu ya Sita ilitoa kibali kwa Shirika kukopa shillingi bilioni **174** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo. Fedha hizo zimewezesha kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo ambapo Mradi wa Morocco Square wenye thamani ya shilingi bilioni **137** umekamilika na nyumba zote **100** zimeuzwa na maeneo mengine ya biashara na ofisi yamepangishwa. Ujenzi wa Mradi wa Kawe **711** wenye thamani ya shilingi bilioni **169** umefikia asilimia **70** na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26. Aidha, Mradi wa Golden Premier Residence wenye thamani ya shilingi bilioni **71** uliopo Kawe, mazungumzo kati ya mkandarasi na Shirika ya kuwezesha mkandarasi kuendelea na ujenzi yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2025. **Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa kupata kibali cha kukopa fedha ambazo zimesaidia kuendelea na ukamilishaji wa miradi hii iliyokuwa imesimama kwa muda mrefu.**

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuenzi kazi nzuri ya kuimarisha upatikanaji wa makazi bora kwa watanzania inayoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, mwaka 2023/24 Shirika lilibuni na kuanza utekelezaji wa Programu ya Ujenzi wa nyumba **5,000** za mradi wa "Samia Housing Scheme". Programu hii

itatekelezwa kwa awamu katika maeneo mbalimbali nchini ambapo asilimia **50** ya nyumba hizo zitajengwa Mkoa wa Dar es Salaam, asilimia **30** zitajengwa katika Jiji la Dodoma na asilimia **20** zitajengwa katika mikoa mingine nchini. Mradi huu unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni **466**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, jumla ya nyumba **560** zimejengwa katika eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam na kuuzwa na sasa Shirika lipo katika hatua ya kuanza kukabidhi nyumba hizo kwa wanunuzi. Aidha, awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huu imeanza eneo la Medeli na Iyumbu Jijini Dodoma; na Kawe na Kijichi Jijini Dar es Salaam ambapo nyumba **908** zinajengwa.



*Mradi wa Samia Housing Scheme, Kawe Dar es Salaam*



*Mradi wa Ujenzi wa Nyumba Iyumbu Dodoma*

131. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Shirika lilipanga kuendelea kukamilisha ujenzi wa majengo ya biashara kwa ajili ya kupangisha katika Mkoa wa Shinyanga (Kahama), Mtwara (Masasi na Manispaa ya Mtwara), Moshi (Kilimanjaro), Kibla

(Arusha), Tanga, Tabora, Lindi, Morogoro, Bukoba (Kagera) na Dar es Salaam. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, ujenzi wa Jengo la Biashara Kahama (Shinyanga) umekamilika; Jengo la Biashara Masasi (Mtwara) ujenzi umefikia asilimia **70** na Jengo la Biashara, Morogoro umefikia asilimia **70**. Aidha, ujenzi wa majengo ya biashara eneo la Mount Meru (Arusha); Tabora Commercial Complex (Tabora); Singida Shops (Singida); Kashozi Complex (Kagera); Mkwakwani Plaza (Tanga); Uluguru Plaza (Morogoro); Iringa Commercial Complex (Iringa); Mpwapwa Flats' Shops (Dodoma); Maghala ya biashara (Mtwara) na Maduka ya Biashara Ilala (Dar es Salaam) ujenzi wake umeshaanza.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kufungua uchumi wa nchi na kushirikisha sekta binafsi ambayo ni injini ya maendeleo endelevu, Shirika lilifanya marekebisho ya Sera ya Ubia ambayo ilizinduliwa rasmi Novemba 16, 2022 Jijini Dar es Salaam. Sera hii imechochea ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya matumizi mbalimbali, ambapo jumla ya miradi **21** yenye thamani ya shilingi billioni **351** inaendelea kutekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam (**17**), Mwanza (**3**) na Iringa (**1**). Aidha, maombi ya miradi **61** yenye thamani ya shilingi bilioni **607** imepitishwa na Bodi ya Shirika ambapo uchambuzi wa maombi hayo ili kujua uwezo wa wabia hao unaendelea. Aidha, Shirika limeendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya ubia **24** iliyokuwa imesimama kwa muda mrefu ambapo ujenzi wa miradi saba (**7**) umekamilika; miradi minne (**4**) imetwaliwa na Shirika na inaendelezwa; wabia wa miradi sita (**6**) wamepewa ilani ya kutwaliwa majengo hayo endapo hawatazingatia masharti ya mikataba na miradi saba (**7**) inaendelea kujengwa na wabia na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025. Utekelezaji wa miradi hii una manufaa makubwa ikiwemo kuongeza upatikanaji wa nyumba bora za makazi na biashara, kuongezeka kwa ajira kwa watanzania na kupendezesha mandhari ya miji yetu na wigo wa kodi na mapato ya Serikali.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Shirika limetekeleza miradi **67** ya ukandarasi yenye thamani ya bilioni **458.2** ambapo ujenzi wa miradi **57**

umekamilika na miradi **10** ujenzi wake upo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Miradi iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wizara nane (**8**) za Serikali eneo la Mtumba; Soko la Kimataifa la Madini ya Tanzanite MireraniManyara; Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI); ghala la chakula Masasi Vijijini na miundombinu kwa ajili ya tanuru (incinerator) la Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) eneo la Nala Jijini Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo mengine unaendelea yakiwemo Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo ujenzi wake umefikia asilimia **90**; Ofisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Temeke Dar es Salaam ambapo ujenzi wake umefikia asilimia **65**; na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Jijini Dodoma umefikia asilimia **40** na Zanzibar umefikia asilimia **20**.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Shirika lilipanga kuendelea kutekeleza mikakati ya kukusanya madeni ya kodi ya pango la nyumba, miradi ya ukandarasi, uuzaji wa nyumba, viwanja na madeni mengineyo. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 15 Mei, 2025, Shirika limefanikiwa kukusanya madeni ya shilingi bilioni tano (**5**). Kutokana na ukusanyaji huu, madeni ya Shirika yamepungua kutoka shilingi bilion **27** hadi shilingi bilioni **22**. Ili kuwezesha ukusanyaji wa madeni hayo mikakati mbalimbali imewekwa ikiwemo kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhimiza ulipaji wa madeni hayo. Aidha, Shirika limeendelea kuchukua hatua kwa wadaiwa wasiozingatia masharti ya mikataba, ambapo wapangaji 150 wamevunjiwa mikataba yao. Vilevile, Shirika linashirikiana na NIDA, Credit Information Reference Bureau na BRELA ili kuwapata wadaiwa wengine binafsi na kampuni zilizohama kwenye nyumba za Shirika. Naomba kutumia fursa hii kuwataka wadaiwa wote wa Shirika kuhakikisha wanalipa madeni yao kabla ya kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Shirika lilipanga kukarabati majengo **250**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Shirika limekarabati na kuboresha nyumba **3,004** zilizopo kwenye majengo **205**. Aidha, ukarabati wa nyumba **1,546** zilizopo kwenye

majengo **45** unaendelea katika mikoa mbalimbali nchini. Ukarabati huu ni endelevu na nyumba zote za Shirika zinatarajiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa ifikapo 2026/27.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Shirika lilipanga kukamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya Mwashiwawala (Mbeya), Kwala (Pwani) na kufanya mapitio ya Mpango wa Kitovu cha Mji eneo la Kawe. Hadi tarehe 15 Mei 2025, usanifu wa Mipango Kabambe katika miji ya Mwashiwawala na Iwambi (Mbeya) umekamilika na Kwala mkoani Pwani umefikia asilimia **25** na upangaji wa maeneo hayo unaendelea.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **908** kupitia Mradi wa Nyumba **5,000** wa Samia Housing Scheme katika maeneo ya Mtoni Kijichi na Kawe (Dar es Salaam), Medeli awamu ya III na Iyumbu (Dodoma);

ii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **422** katika mradi wa Kawe 711 unaotarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2026, ujenzi wa nyumba **196** katika mradi wa Golden Premium Residence (GPR) na Kiwanja nambari 300 Regent Estate;

iii) Kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa miradi **21** ya ubia yenye thamani ya shilingi billioni **351** na kukaribisha wawekezaji wengine kutoka sekta binafsi ili kufanya uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi kupitia Sera ya Ubia;

iv) Kuendelea na ujenzi wa miradi ya majengo ya biashara katika Mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Meru view shops (Arusha), Tabora Plaza (Tabora), Singida Plaza (Singida), Mkwakwani Plaza (Tanga), Kashozi Commercial Complex (Kagera), Uluguru Plaza (Morogoro), Iringa Commercial Complex (Iringa), Uhuru shopping centre Ilala (Dar es Salaam) na Mpwapwa Flats' Shops (Dodoma);

v) Kuanza ujenzi wa miradi mipya katika Miji na Halmashauri mbalimbali ikiwamo jengo la matumizi mchanganyiko mkoani Ruvuma, Usa River na Ngarenaro mkoani Arusha;

vi) Kuendelea na ujenzi wa maghala tisa (**9**) kwa ajili ya kupangisha katika Manispaa ya Mtwara;

vii) Kuendelea na kuanza upembuzi yakinifu wa ujenzi wa miradi ya vitovu vya miji ikiwamo Iwambi (Mbeya), Mwashiwawala (Songwe), Kwala (Pwani), Urafiki na Salama Creek (Dar es Salaam);

viii) Kuendelea kutekeleza mpango wa ukarabati wa nyumba za Shirika;

ix) Kutekeleza miradi ya ukandarasi na utaalamu elekezi inayoendelea na mingine itakayojitokeza; na

x) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwezesha kujenga nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya mahitaji mbalimbali.

## BODI ZA USAJILI WA WATAALAM WA FANI ZA ARDHI

138. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inasimamia utekelezaji wa shughuli za Bodi mbalimbali za wataalam wa sekta ya ardhi. Bodi hizo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kusimamia maadili ya kitaaluma.

### Bodi ya Usajli wa Wataalam wa Mipangomiji

139. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Bodi iliahidi kuendelea kusajili wataalam na kampuni za mipangomiji ili kuimarisha utendaji kazi. Hadi tarehe 15 Mei 2025, wataalam **27** na kampuni sita (**6**) za mipangomiji zimesajiliwa. Kampuni tano (**5**) zimefutiwa usajili na mtaalam mmoja (**1**) amepewa onyo kwa

kukiuka sheria na maadili. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa kazi za kitaaluma umefanyika katika mikoa mitano ya Geita, Kagera, Mwanza, Shinyanga na Dodoma na kutoa ushauri wa kitaalam.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Bodi imesajili wataalam **202** na kampuni za Mipangomiji **28** na kufanya jumla ya Wataalam **520** na kampuni **116** zilizosajiliwa tangu Bodi ilipoanzishwa mwaka 2009. Aidha, Bodi imeendelea kusimamia maadili na nidhamu ya taaluma kwa wataalam wa mipangomiji na kampuni ambapo hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa. Katika kipindi hicho, jumla ya wataalam **59** na kampuni **45** zilituhumiwa kwa makosa mbalimbali ambapo wataalam watatu (**3**) wametozwa faini, **36** wamefutiwa leseni na, tisa (**9**) wamepewa onyo. Vilevile, kampuni sita (**6**) zimefutiwa usajili, **32** zimetozwa faini na sita (**6**) zimesitishiwa leseni kwa muda kwa makosa mbalimbali ya kimaadili. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na mamlaka za kitaaluma imeandaa Mwongozo wa Utambuzi wa Mitaala (recognition manual) kwa vyuo vinavyotoa taaluma ya mipangomiji ili wahitimu wake waweze kusajiliwa na kuendelea kuimarisha ustawi wa sekta nchini. Chimbuko la mwongozo huu ni kuongezeka kwa vyuo vinavyofundisha taaluma ya mipangomiji ambapo baadhi vilibainika kuwa na mitaala inayotofautiana huku vingine mitaala yake ikikosa kozi za msingi za taaluma ya mipangomiji.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Bodi itaendelea kusajili wataalam na kampuni za mipangomiji zitakazokidhi vigezo ili kuimarisha utendaji kazi. Aidha, usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji kazi na uzingatiaji wa Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Sura 426 katika mikoa utafanyika ili kuimarisha ustawi wa sekta ya mipangomiji.

**Bodi ya Usajili wa Wathamini**

142. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Bodi ya Usajili wa Wathamini ilipanga kusajili wathamini **150** katika ngazi zote, kutengeneza mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya usajili wa wathamini na kufanya mapitio ya mitaala ya mafunzo ya Usajili Kamili, kaguzi za kitaalam, kuendesha mafunzo kwa wathamini na kufanya Mkutano Mkuu wa Mwaka. Hadi tarehe 15 Mei 2025, Bodi

imesajili jumla ya Wathamini **160** sawa na asilimia **106** ya lengo. Kati ya hao, Wathamini **36** katika ngazi ya Usajili Kamili, Wathamini **88** katika ngazi ya Usajili wa Awali na Wathamini **36** wameorodheshwa kama Wathamini Wasaidizi. Aidha, Bodi imesajili Kampuni za Uthamini **16**. Vilevile, Bodi ilipokea jumla ya malalamiko **12** ambapo sita (**6**) ya kinidhamu yakiwemo malalamiko manne (**4**) yanayohusu Wathamini na malalamiko mawili (**2**) yanayohusu kampuni za Uthamini.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Bodi ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi milioni **740.55** kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato. Hadi tarehe 15 Mei 2025, Bodi ilikusanya shilingi milioni **800.7** sawa na asilimia **108** ya lengo.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, Bodi imefanikiwa kujenga mfumo wa kielektroniki wa Usajili wa Wathamini ambapo Wathamini **416** wamesajiliwa katika ngazi ya Usajili Kamili; Wathamini **794** katika ngazi ya Usajili wa Awali; na Wathamini Wasaidizi **181** wameorodheshwa. Aidha, Bodi imefanikiwa kusajili kampuni za Uthamini **90**. Vilevile, Bodi imefanikiwa kusimamia masuala ya nidhamu ya Wathamini kwa kutatua masuala **30** kati ya **50** yaliyowasilishwa kwa ajili ya uamuzi kwa kusimamisha leseni za Wathamini **11**, kutoa onyo kwa Wathamini **13** na kuzifungia Leseni Kampuni sita (**6**). Mashauri **20** yaliyobaki yatahitimishwa katika mwaka 2025/26.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Bodi ya Usajili wa Wathamini imepanga kusajili Wathamini **150** katika ngazi mbalimbali, kampuni za uthamini **10**, kuendelea kusimamia kikamilifu maadili ya kazi za uthamini, kuandaa vitabu vya kiada kwa ajili ya mafunzo na mitihani ya Wathamini kwa ngazi mbalimbali, kuendelea na ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa Wathamini na kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa jengo la ofisi za Bodi Dodoma. Aidha, kwa mwaka 2025/26 Bodi imepanga kukusanya shilingi bilioni **1.7** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.



*Baadhi ya wahitimu wa mafunzo ya umahiri wa Uthamini wakila kiapo cha uadilifu wakati wa mkutano wa tano wa mwaka 2024*

**Baraza la Taifa la Wapima Ardhi**

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza linasajili na kusimamia maadili ya taaluma ya Upimaji Ardhi nchini. katika mwaka 2024/25, Baraza lilipanga kupokea na kusajili Wapima Ardhi **80** na kutoa Leseni kwa kampuni za upimaji **30**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, maombi **75** yamepokolewa na wapima ardhi **75** wamesajiliwa katika makundi mawili ambayo ni Usajili wa Awali (**42**) na Usajili Kamili (**33**) na kufanya jumla ya wapima ardhi waliosajiliwa nchini kufikia **868.** Aidha, kampuni tisa (**9**) zimesajiliwa na kufanya kampuni za upimaji zilizosajiliwa kufikia **128.** Katika mwaka 2025/26, Baraza limepanga kupokea maombi na kusajili wapima ardhi **100** pamoja na kampuni za upimaji ardhi **30**.



*Wajumbe wa Baraza la Taifa la Wapima Ardhi wakijadili maombi ya Leseni za Upimaji*

147. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, Baraza lilipokea maombi **456** ya Wapima Ardhi na kampuni za Upimaji **86** ambapo jumla ya Wapima Ardhi **241** wamesajiliwa. Kati ya hao, Wapima Ardhi 128 wamepata usajili kamili na Wapima Ardhi **113** wamepata usajili wa muda. Aidha, kampuni **75** zimepewa Leseni za Upimaji. Pia, Baraza limeendelea kuchukua hatua kwa wapima ardhi na kampuni za upimaji ardhi kutokana na ukiukaji wa maadili ya taaluma ya upimaji ambapo kampuni tano (**5**) zimepewa onyo na kampuni mbili (**2**) zimefutiwa Leseni za Upimaji.

**VYUO VYA ARDHI (TABORA NA MOROGORO)**

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro ambavyo hutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali za ardhi, kufanya utafiti katika fani za sekta ya ardhi na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala ya ardhi. Katika mwaka 2024/25, Chuo cha Ardhi Tabora na Chuo cha Ardhi Morogoro vilipanga kudahili jumla ya wanafunzi **2,670**, ambapo Chuo cha Ardhi Tabora wanafunzi **1,580** na Chuo cha Ardhi Morogoro wanafunzi **1,090**. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, wanafunzi **1,823** walikuwa wamedahiliwa. **Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuridhia vyuo hivi kuingia katika mpango wa kupewa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hatua hii itachochea udahili wa wanafunzi na hivyo kuongeza idadi ya wataalam wa sekta ya ardhi nchini.**



*Mhe. Geophrey Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, akipata maelezo ya Mpango wa Upanuzi wa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) eneo la mlima Kola Morogoro*



*Mhe. Geophrey Pinda Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, akimkabidhi cheti cha kuhitimu masomo mwanafunzi wa Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) wakati wa Mahafali ya 42 ya chuo hicho yaliyofanyika mkoani Tabora*

149. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita (6), vyuo hivi vimefanikiwa kuongeza kozi nne (**4**) mpya kwa

ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada. Kozi zilizoongezwa ni za fani ya Mipangomiji, Usanifu wa Majengo, Usimamizi wa Mazingira na kozi ya Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS). Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2025, wanafunzi **301** wamedahiliwa katika kozi hizi. Aidha, Wizara imeendelea kuvijengea uwezo vyuo hivi kwa kuvipatia vitendea kazi ikiwemo magari na vifaa vingine muhimu ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi. Chuo cha Ardhi Tabora, kimejengewa maktaba ya kisasa. Maktaba hii ina uwezo wa kuchukua wanafunzi **300** kwa wakati mmoja hivyo imeongeza uwezo wa chuo kudahili wanafunzi. Aidha, ili kuimarisha utunzaji wa rasilimali za chuo na ulinzi, Chuo cha Ardhi Tabora kinaendelea na ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la chuo.







*Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakikagua Mradi wa ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora*

150. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, vyuo vimepanga kudahili jumla ya wanafunzi **2,348** ambapo Chuo cha Ardhi Tabora wanafunzi **1,580** na Chuo cha Ardhi Morogoro wanafunzi **768**. Aidha, Vyuo vitaendelea kuimarisha miundombinu ambapo Chuo cha Ardhi Morogoro kitaanza ujenzi wa vyumba viwili (**2**) vya madarasa, kuimarisha maabara ya kompyuta, kujenga uzio katika eneo la chuo na kufanya ukarabati wa majengo. Vilevile, Chuo cha Ardhi Tabora kitaendelea kujenga sehemu ya uzio yenye urefu wa mita **410**; na kukamilisha ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za mihadhara (Lecture theatres) zenye uwezo wa kubeba wanafunzi **700** kwa wakati mmoja.

## UTAWALA NA RASILIMALIWATU

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Utawala na Rasilimali Watu ni sehemu muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa katika maeneo yanayohusiana na maendeleo ya kitaaluma, usimamizi wa utendaji, ajira na masuala ya ustawi wa watumishi. Katika mwaka 2024/25, Wizara ilipanga kuendelea kuwawezesha watumishi kushiriki mafunzo kwa kuzingatia mpango wa mafunzo wa Wizara ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2025, watumishi **123** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Lengo ni kuwajengea uwezo na kuongeza weledi katika utekelezaji wa majukumu. Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imewezesha mafunzo kwa watumishi **815**.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwasiliana na Mamlaka husika ili kupatiwa watumishi kwa kuzingatia ikama ya Wizara. Katika mwaka 2024/25, Wizara iliomba kibali cha kuajiri watumishi **211** ambapo watumishi **197** wameajiriwa. Juhudi hizi zimewezesha watumishi walioajiriwa katika kada mbalimbali kufikia **273** kwa kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Sita na hivyo kufanya kuwa na jumla ya watumishi **2,447**. Kati ya hao, wanaume ni **1,711** na wanawake ni **736**.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi kufanya kazi katika mazingira bora kwa lengo la kuhakikisha wanakuwa na vitendea kazi katika utoaji wa huduma. Katika kufanikisha lengo hilo hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara imenunua magari **52** ambayo yamegawiwa kwenye Ofisi za Ardhi za Mikoa yote 26 ili kuwezesha utekelezaji wa kazi za Wizara. Vilevile, Wizara iko katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara pamoja na ununuzi wa samani ili lianze kutumika kabla ya mwezi Juni, 2025.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utumishi wa umma. Vilevile, imeendelea kusimamia matumizi ya Mfumo wa Upimaji Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma (PEPMIS), Mfumo wa Kumbukumbu za Kiutumishi na Mishahara (eWatumishi), Mfumo wa Mawasiliano na

Utunzaji wa Kumbukumbu (e-Office), Mfumo wa kupokea mrejesho kutoka kwa wananchi (e-Mrejesho) na matumizi ya kituo cha huduma kwa wateja ili kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na utoaji wa huduma kwa wananchi.



*Jengo jipya la Ofisi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi lililopo Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma*



*Baadhi ya magari ya Wizara ambayo yanasaidia kurahisisha utendaji kazi*

155. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi pamoja na kuwekea mkazo katika uwajibikaji, usimamizi wa misingi ya uadilifu na weledi katika utoaji wa huduma za ardhi nchini. Aidha, Wizara imepanga kuajiri watumishi **319** pamoja na kuendelea kusimamia utendaji kazi wa watumishi kupitia mifumo iliyowekwa ili kuhakikisha watumishi wote wanatekeleza majukumu kulingana na matarajio ya Serikali. Vile vile, Wizara itawawezesha watumishi **150** kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

**HABARI NA ELIMU KWA UMMA**

156. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara iliahidi kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya Sekta ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2025, Wizara imetoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi kupitia maonesho, vipindi vya redio na televisheni, mitandao ya kijamii, Kliniki za Ardhi, vipeperushi, majarida, makala katika magazeti na mikutano ya hadhara. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia Tovuti ya Wizara (www.lands.go.tz) ambapo zaidi ya watu **175,822** walitembelea tovuti hii. Aidha, zaidi ya watu **303,600** walipata elimu kupitia kurasa rasmi za Wizara katika mitandao ya kijamii.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia Makala mbalimbali ikiwemo kipindi cha Televisheni cha 'Maisha ni Nyumba' kinachorushwa na Televisheni ya ITV kinachoratibiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na makala iliyoratibiwa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kupitia kipindi cha Kishindo cha Awamu ya Sita kupitia Televisheni ya Taifa (TBC) kinachorushwa mara mbili kwa wiki. Katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi kwa kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali, kushiriki makongamano na mikutano inayoandaliwa na taasisi nyingine, kuendelea kushirikiana na wahariri wa vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, mikutano ya hadhara na maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) na matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Huduma za Ardhi (e-Ardhi).

## SHUKRANI

158. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nawashukuru Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb), Naibu Waziri; Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu; na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya kusimamia sekta hii muhimu. Aidha, nawashukuru Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi; Bw. Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa; Bw. Joseph Constantine Mafuru, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Bi. Evelyne Baruti Mugasha, Mthamini Mkuu; na Bi. Stella Chaggi Tullo, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Pia, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi; na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa bidii na maarifa na hivyo kuleta ufanisi katika kufikia malengo ya Wizara.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya EXIM ya Korea Kusini, UN-HABITAT, *Shelter Afrique, African Union Boarder Program, Regional Centre for Mapping of Resources for Development (RCMRD)*, Benki ya Maendeleo Afrika, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), *Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC)*, *Watumishi Housing Company*, Taasisi za fedha za ndani, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mzuri waliotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi. Kwa hakika, wanahabari wameiwezesha Wizara kuwafikia wadau wengi zaidi kwa namna mbalimbali.

## HITIMISHO

160. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara katika mwaka 2025/26, itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya

Sekta ya Ardhi kwa kuboresha huduma zinazotolewa. Ili kutekeleza azma hiyo, Wizara itazingatia vipaumbele kama vilivyoainishwa hapo awali.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2025/26**

161. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kama ifuatavyo:-

Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

| AINA | MAPATO | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | 265,000,000,000 |
| | **MAKISIO YA MATUMIZI** | |
| B | **Matumizi ya Kawaida** | |
| | Matumizi ya Mishahara (PE) | 53,820,915,000 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 37,559,123,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **91,380,038,000** |
| C | **Matumizi ya Maendeleo** | |
| | Fedha za Ndani | 5,732,469,000 |
| | Fedha za Nje | 56,325,360,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **62,057,829,000** |
| | **JUMLA KUU (B+C)** | **153,437,867,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo shilingi **153,437,867,000/=.**

Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

| AINA | AINA YA MATUMIZI | FEDHA ZINAZOOMBWA |
|---|---|---|
| A | Mapato ya Tume | 18,000,000 |
| | **MAKISIO YA MATUMIZI** | |
| B | **Matumizi ya Kawaida** | |
| | Matumizi ya Mishahara (PE) | 4,712,143,000 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | 3,475,426,000 |
| | **Jumla Ndogo (B)** | **8,187,569,000** |
| C | **Matumizi ya Maendeleo** | |
| | Matumizi ya Maendeleo | 2,520,616,000 |
| | **Jumla (B+C)** | **10,708,185,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi **10,708,185,000/=.**

162. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zote zinazoombwa kwa Wizara (Fungu 48 na Fungu 03) ili muweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi **164,146,052,000/=.**

163. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii, yameambatishwa majedwali ambayo yanafafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni www.lands.go.tz.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa ahsante sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati, kwa niaba Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Kwanza

kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiyo muweza wa kila jambo katika ulimwengu huu. Pia, ninaomba kabla sijasoma taarifa yangu, taarifa yote ya Kamati kama ilivyo iiingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ya Kanuni za Bunge ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa za Kamati zinazowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ndiyo hiyo ya utangulizi ambayo nimeisoma; sehemu ya pili inahusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa 2024/2025; sehemu ya tatu, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; sehemu ya nne inahusu maoni na ushauri; na ya mwisho ni hitimisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025: wakati Bunge lilipojadili Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 tarehe 24 na 27 Mei, 2024 Kamati ilitoa ushauri katika mambo saba kwa Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa maeneo mahsusi mawili kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - Fungu 03.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kulijulisha Bunge lako kuwa maeneo hayo yamefanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa na maeneo mengine yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni ushauri uliozingatiwa ni suala la kuongeza watumishi wa sekta ya ardhi nchini kwa lengo la kupunguza uhaba wa watumishi katika sekta hiyo. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilifanikiwa kuajiri watumishi 197 wa kada mbalimbali katika sekta za ardhi nchini. Aidha, katika mwaka 2024/2025 Wizara imepata kibali cha kuajiri watumishi 34 ambapo Kamati imetaka Wizara kuajiri wakaguzi wa majengo kwa ajili ya kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kudhibiti ujenzi holela nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, kuna maeneo ambayo utekelezaji wa ushauri wa Kamati haukuridhisha sana ikiwa ni pamoja na ukusanyaji hafifu wa madeni ya pango la nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Wizara inaonesha kuwa Shirika limekusanya takribani shilingi milioni 300 ikiwa ni 14.3% ya madeni yote inayodai. Kamati imebaini kuwa Shirika halina mpango madhubuti wa ufuatiliaji wa madeni ya kodi ya pango la nyumba. Hali hii inaweza kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa ufanisi kwani fedha hizi ni moja ya chanzo kikuu cha mapato kwa shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, tarehe 12 hadi 19 Machi, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu inayotekelezwa katika mikoa miwili ambayo ni Manyara na Kilimanjaro. Miradi hiyo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha shilingi 70,656,510,000/= kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taarifa kuhusu miradi hiyo inapatikana ukurasa wa 6 hadi 12 wa taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Wizara. Tarehe 20 Machi, 2025 Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya

Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanikiwa kufanya baadhi ya shughuli ili kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea. Baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na kufanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 (Toleo la Mwaka 2023). Zoezi hilo, limekamilika na kuzinduliwa rasmi tarehe 17 Machi, 2025; Upimaji wa maeneo pia kwa kutumia picha za anga katika maeneo ya Ndachi na Chamwino Mkoani Dodoma na uwanja wa michezo *AFCON* 2027 Jijini Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuanza Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na; pia, kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya vijiji 280 katika maeneo yaliyopitiwa na miradi ya kimkakati na maeneo ya vijiji vya mpakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa Fungu 48 ya Wizara ya Ardhi. Uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 48 hadi kufikia mwezi Februari, 2025 umeonesha mambo yafuatayo: -

(i) Fedha za matumizi ya kawaida zilipatikana kwa 54% ikiwa ni upungufu wa fedha zilizotakiwa katika kipindi kama hicho kwa 12.7%. Pia, katika kiasi hicho cha fedha za kawaida fedha za matumizi mengineyo *(OC)* zilikuwa 47% ya fedha zote huku mshahara ikiwa imepatikana kwa 60%.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa 76% ya bajeti na katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilifikia 91% na fedha za nje 63%. Hata hivyo, katika fedha za ndani 77.5% ilikuwa ni fedha ya kulipia madeni mbalimbali ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Fungu 03 - Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Tume ya Taifa ya Mipango ya

Matumizi ya Ardhi uchambuzi na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2025 ulionesha mambo yafuatayo: -

(i) Tume ilipokea 58.8% ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo; na

(ii) Fedha za matumizi ya Kawaida zilizopokelewa kwa 55.46% ya bajeti yote. Katika kiasi hicho cha fedha za matumizi mengineyo *(OC)* zilipokelewa kwa 50.3%; huku mishahara ikiwa imepokelewa kwa 59.7%; na fedha za miradi ya maendeleo zilipokelewa kwa 63.59%. Huku fedha zote zikiwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa upatakinaji wa fedha hauridhishi sana kwa kuwa kiasi kilichopelekwa ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotakiwa kupelekwa kwenye Tume kutoka Serikalini katika kipindi hicho. Hali hii inaweza kupelekea Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio na mapato kwa fedha 2025/2026. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48). Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inakadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 265,000,000,000. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio hayo yameongezeka kwa shilingi 15,000,000,000 sawa asilimia sita ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo, maoni ya jumla: -

(i) Wizara iongeze jitahada ya kuweza kupima na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vyote ili kuondoa migogoro ya ardhi nchini;

(ii) Wizara ihakikishe inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama yalivyopangwa kwenye bajeti; na

(iii) Wizara ihakikishe inasambaza Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa huduma za Ardhi *(e-Ardhi)* katika Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati kwenye ukusanyaji wa maduhuli. Kamati inashauri kuwa:

(i) Serikali iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwani Wizara hii imekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji.

(ii) Irejeshe utaratibu wa Kodi ya Pango la Ardhi *(Land Rent)* kukusanywa na Wizara ambayo ndiyo ina nyenzo za kisheria na mifumo ya ukusanyaji wa kodi hiyo; na

(iii) Ihakikishe inatengeneza mipango na mbinu za kufuatilia wadaiwa wa Pango la Ardhi ili kuweza kuongeza mapato ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfumo wa Uunganishi wa Kieletroniki wa Huduma za Ardhi. Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali ihakikishe inaongeze kasi ya kusambaza Mfumo wa *e-Ardhi* kwenye halmasahuri zote nchini ili shughuli zote za ardhi zifanyike kwenye mifumo;

(ii) Ihakikishe inafanya maboresho ya Mfumo ili uwe rafiki kwa watumiaji; na

(iii) Ihakikishe inatoa elimu kwa Maafisa Ardhi na kwa wananchi wote kuhusu Mfumo wa utoaji huduma katika usimamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto ya ukosefu wa wakaguzi majengo nchini, Kamati inashauri Serikali kuwa

ihakikishe inaajiri wakaguzi majengo katika Halmashauri zote ili kuzuia ujenzi holela nchini. Hata hivyo, kuhusu uchelewaji wa fidia ya ardhi katika maeneo yaliyofanyiwa uthamini Kamati inashauri Serikali ihakikishe inakuwa na fedha kabla ya kuanza zoezi la kufanya uthamini na mchakato wa utwaaji wa ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pia ifanye marekebisho ya sheria kwa ajili ya kuufanya Mfuko wa Fidia ya Ardhi nchini kuwa chini ya Mthamini Mkuu wa Serikali. Hali itakayomfanya Mthamini Mkuu wa Serikali kujua uwezo wa Mfuko kabla ya kwenda kufanya uthamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya ardhi nchini, Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe kuwa inakuwa na kanzidata ya maeneo yote yaliyopangwa na kupimwa ili kuwezesha wananchi kufanya ujenzi wa makazi kwenye maeneo rasmi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ihakikishe inaandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuondoa migogoro inayojitokeza hapa nchini. Pia, ihakikishe *Clinic* za Ardhi zinakuwa endelevu na zifanye kazi kwa mikoa yote ili kuendelea kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wakubwa katika sekta ya ardhi ambao hawajaendeleza maeneo yao Kamati inashauri Serikali ihakikishe inafanya tathmini ya wawekezaji katika sekta ya ardhi nchini ili kutambua hali ya uendelezaji wa maeneo hayo, lakini pia ichukue hatua kwa wawekezaji ambao wameshindwa kuendeleza maeneo yao kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufinyu wa bajeti katika Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi, Kamati inashauri Serikali kuwa iongeze fedha za maendeleo ili kuiwezesha Tume kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji vingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa niaba ya Kamati ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Spika mwenyewe kwa kazi

kubwa anayofanya, Naibu Spika wewe mwenyewe lakini Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu katika kulisimamia na kuliwezesha Bunge letu kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, ninawapongeza na kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi mahiri kabisa wa Mwenyekiti wetu wa Kamati Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava. Ninaomba majina yote ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru Watendaji wote wa Wizara nchini chini ya Katibu Mkuu, Mhandisi Anthony Sanga; na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Lucy Kabyemela kwa ushirikiano mkubwa walioupatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninaomba nimalize kwa kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge wakiwemo Ndugu Eunice Shirima, na Ndugu Charles Wanyancha ambao ni Makatibu wetu wa Kamati pamoja na Makatibu wote wa Kamati zote kwa uongozi wao mzuri chini ya uongozi thabiti kabisa wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa hoja, ninaomba nitumie fursa hii kuushukuru Uongozi wa Chama cha Mapinduzi kuanzia ngazi ya Taifa hadi matawi lakini pia jumuiya zote tatu ikiwemo jumuiya yangu ya wazazi, jumuiya ya akina mama

Tanzania, pamoja na jumuiya ya umoja wa vijana kwa namna ambavyo wanashirikiana na mimi katika kazi zangu. Wao ndio wameniwezesha kuwa jasiri na kufanya kazi zangu. Bila ya wao, na Mwenyezi Mungu, kazi yangu isingekuwa rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa Wajumbe wote wa Mikutano yetu ya ndani ya chama ambao wameongeza wigo wao kuongeza demokrasia ndani ya chama wataweza kufanya maamuzi sahihi na kuwarudisha viongozi ambao wataweza kusaidiana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Ninaamini kabisa Wajumbe wangu wa wazazi wananiamini na wataendelea kuniamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

#### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari,2023 {Kanuni za Bunge}, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu

Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha
2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (5) kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa, Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inahusu Uchambuzi wa tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya tatu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iv) Sehemu ya nne inayohusu Maoni Ushauri; na

(v) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

**1.2 Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii umejengwa katika Masharti ya Kanuni za Bunge ambapo Kifungu cha 6(8)(a)(b) kikisomwa kwa Pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari,2023, kinaitambua Kamati hii kuwa na wajibu wa kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa

Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.Katika hatua hiyo Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

1.3 Mawanda ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo: -
(i) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;
(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa fedha 2025/2026;
(iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

**Mheshimiwa Spika**, mambo yaliyochambuliwa yalijitokeza katika randama ya Mpango na Bajeti ya **Fungu 48** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na randama ya Mpango na Bajeti ya **Fungu 03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.Wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia na uwiano. Aidha, njia iliyotumika ni tathmini ya Jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali ambapo mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo ilizitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, tarehe 20 – 21 Machi, 2025, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo ilijumuisha Mpango na Bajeti ya Wizara **Fungu 48** pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu 03.**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;
(ii) Ukaguzi wa Miradi;
(iii) Utekelezaji wa Vipaumbele;
(iv) Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli; na
(v) Hali ya upatikanaji wa Fedha.

**2.1.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lilipojadili Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 tarehe 24 na 27 Mei,2024, Kamati ilitoa ushauri katika mambo saba (07) kwa **Fungu 48** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa maeneo mahsusi mawili (2) kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **(Fungu 03).** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa baadhi ya maeneo ushauri wa Kamati umezingatiwa huku maeneo mengine utekelezaji wa ushauri wa kamati haujafanyiwa kwa kiwango cha kuridhisha

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu kuongeza watumishi wa sekta ya ardhi nchini ili kupunguza uhaba wa watumishi katika sekta hiyo. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilifanikiwa kuajiri watumishi 197 wa kada mbalimbali katika sekta za ardhi nchini. Aidha, katika mwaka 2024/2025 Wizara imepata kibali cha kuajiri watumishi 34 ambapo Kamati inaitaka Wizara kuajiri wakaguzi wa majengo (**inspector building**) kwa ajili ya kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kudhibiti ujenzi holela nchini.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika urejeshwaji wa fedha za mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK), Kamati inapenda kulijulisha Bunge kuwa utekelezaji wa azimio hili unaendelea kufanyiwa kazi. Hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2025 fedha zilizorejeshwa ni shilingi **bilioni 29.1** kutoka shilingi **bilioni 22.4** zilizokuwa zimekusanywa katika kipindi cha Machi, 2024 ikiwa ni ongezeko la takribani **asilimia 30** ya marejesho. Aidha, Halmashauri zilizomaliza marejesho zimeongezeka kutoka Halmashauri **12** hadi kufikia Halmashauri **20**. Kamati inaitaka Wizara kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa na kufanya mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi nchini kuwa endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, kuna maeneo ambayo utekelezaji wa ushauri wa Kamati hauridhishi ikiwa ni pamoja na ukusanyaji hafifu wa madeni ya pango la nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Taarifa ya Wizara inaonyesha kuwa Shirika limekusanya takribani Shilingi **milioni 300** ikiwa ni **asilimia 14.3** ya madeni yote inayodai. Kamati imebaini kuwa Shirika halina mpango madhubuti wa ufuatiliaji wa madeni ya kodi ya pango la nyumba. Hali hii inaweza kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa ufanisi kwani fedha hizi ni moja ya chanzo kikuu cha mapato kwa shirika.

### 2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya miradi ya maendeleo hupitishwa na Bunge kwa lengo la kuimarisha sekta inayohusika ili kutoa mchango katika kukuza Uchumi na kuleta ustawi wa maendeleo ya wananchi. Kwa vile Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kujiridhisha na hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoidhinishiwa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, tarehe 12 hadi tarehe 19 Machi, 2025, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu (03) inayotekelezwa katika mikoa miwili ambayo ni Manyara na Kilimanjaro. Miradi hiyo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha **Shilingi 70,656,510,000** kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Naomba kubainisha na kufafanua miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo: -

**(a) Mradi Namba 2326: Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) katika halmashauri ya Mji wa Babati**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa uratibu wa Wizara rya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kutoa mikopo ya fedha isiyo na riba kwa halmashauri nchini. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi **cha Shilingi 4,026,000,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwenye halmashauri mbalimbali nchini. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezji wa mradi wa **KKK** kwenye mitaa ya Sawe na Nangara katika Halmashauri ya Mji wa Babati Mkoani Manyara.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Mji babati ilipatiwa na Wizara mkopo usio na riba kiasi **cha Shilingi 250,000,000/=.** Halmashauri ilitekeleza mradi huu kupitia kampuni mbili za upimaji ambazo ni Land General Planning Co.LTD na Kampuni ya Millenium Surveyors na kufanikiwa kupima viwanja **3969** kwa ajili makazi, biashara, viwanda, huduma na miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** na halmashauri inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 476,280,000/=** kupitia mradi huu. Aidha, mradi huu utainufaisha halmashauri kwa kuingizia mapato kiasi cha **Shilingi 226,280,000** kama faida baada ya kurejesha fedha za mkopo kiasi cha **Shilingi 250,000,000/=** ambazo zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kamati inatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu tarehe 12 Machi, 2025, halmashauri ilikuwa imefanikiwa kukusanya na kurejesha kiasi cha **Shilingi 103,717,091/=** sawa na **asilimia 41** ya fedha inayotakiwa kurejeshwa. Hata hivyo, Kamati ilitarifiwa kuwa zoezi la uuzaji wa viwanja na kutolewa kwa hati linaendelea miongoni mwa wananchi na halmashauri imepanga kutumia sehemu ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni liliobakia.

(b) **Mradi Namba 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Tume iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 5,041,232,000/=** kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa kuandaa matumizi ya ardhi katika vijiji 24 kati ya vijiji 68 kwenye Halmashauri ya Willaya ya Rombo tarehe 15 Machi, 2025. Mradi huu ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 ukurasa wa 120 ambapo katika Ibara ya 74, inataka Serikali kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji vilivyo katika wilaya za mipakani.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** ambapo Kamati ilishiriki katika utoaji wa Hati Miliki za Kimila ishirini na moja **(21)** kwenye kijiji cha Kisale Msaranga. Aidha, Kamati ilishuhudia hatua mbalimbali katika utatuzi wa migogoro ikiwa ni matokeo ya utekelezaji wa zoezi la upangaji wa matumizi ya ardhi katika kijiji eneo la mradi.

(c) **Mradi wa Kandarasi ya Ujenzi wa Soko la Madini Unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Wilaya ya Simanjiro**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linatekeleza Kandarasi ya ujenzi wa Soko la Madini katika Wilaya ya Simanjiro. Aidha, mteja katika mradi huo ni Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro na unatekelezwa kwa kiasi cha **Shilingi 5,494,724,533.28.** Katika mkataba wa awali, mkandarasi alitakiwa kufanya usanifu na kujenga (design and build) sakafu 3 yaani (G plus 2). Hata hivyo, kufuatia mahitaji ya soko hilo kuwa makubwa, mkataba ulibadilishwa na Shirika kuongezewa kazi ya kujenga jengo la sakafu 5 yaani (G plus 4).

**Mhemiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua mradi huo ambapo ilibaini kuwa mradi umefikia **asilimia 98** kwa mkataba wa

awali. Changamoto kubwa katika utekelezaji wa mradi huu ni upatikanaji wa fedha kwa wakati kwani uwezo wa halmashauri katika kufanya malipo ni mdogo. Kamati inalitaka Shirika kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kufanikisha malipo kwa ajili ya kumalizia sehemu ya utekelezaji wa mradi.

**Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa za utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa pamoja na hali halisi iliyobainika wakati wa ziara, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati imefikia hatua nzuri na hali inayoonesha kuwa miradi hiyo itakamilika kwa wakati na mengine ikiwa imefikia asilimia 100;

(ii) Wakati wa utekelezaji wa miradi, Wizara na Tume ziliwashirikisha wadau na wanachi ambao ni wanufaika wa miradi husika; na

(iii) Kasi ndogo ya wananchi katika kulipia viwanja hati ya viwanja vilivyopimwa kupitia mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK).

**Mheshimwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Wizara kwa miradi iliyokamilika ianze kutoa huduma na kwa ile ambayo haijakamilika Wizara iongeze usimamizi.

**2.1.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 20 Machi, 2025 Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka wa Fedha 2024/2025. Wakati wa uchambuzi wake Kamati ilizingatia vipaumbele vya wizara ambavyo ni: -

(i) Kukamilisha kanuni na miongozo ya uendelezaji wa milki;
(ii) Kutoa elimu ya sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa uendelezaji miji katika Ofisi za ardhi;
(iii) Kufanya tafiti kuhusu makzi yasiyo rasmi;
(iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya urasimishaji na kuzuia makazi yasiyo rasmi;
(v) Kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya ardhi katika mikoa 26 kuhusu matumizi ya Mfumo unganishi wa Taarifa za Ardhi (e-Ardhi);
(vi) Kuratibu na kusimamia mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni katika sekta ya ardhi nchini;
(vii) Kufanya Ukaguzi wa uzingativu wa Mipango ya matumizi ya Ardhi iliyoandaliwa katika vijiji;
(viii) Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi; na
(ix) Kufanya tafiti kuhusu makazi yasiyo rasmi

**Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kufanya baadhi ya shughuli ili kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea. Baadhi ya Shughuli hizo ni pamoja na: -

(i) Kufanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 (Toleo la Mwaka 2023). Zoezi hilo limekamilika na kuzinduliwa rasmi tarehe 17 Machi,2025;
(ii) Upimaji wa maeneo kwa kutumia picha za anga katika maeneo ya Ndachi na Chamwino mkoani Dodoma na uwanja wa michezo AFCON 2027 Jijini Arusha;
(iii) Kuanza Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000;
(iv) Kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya vijiji 280 katika maeneo yaliyopitiwa na miradi ya kimkakati na maeneo ya vijiji vya mpakani.

**2.1.4 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** kama sehemu ya msingi katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara, Kamati ilipokea taarifa ya Serikali kuhusu hali ya

ukusanyaji wa maduhuli kwa **Fungu 48 na Fungu 03**. Katika uchambuzi wake, Kamati ililenga kulisaidia Bunge kupata uhalisia na taswira kamili kuhusu uwezo wa Wizara katika ukusanyaji maduhuli. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo: -

(i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo; na

(ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Fungu 48** ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 250,000,000,000/=.** Hadi kufikia Februari, 2025 wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 110,322,568,159.57** sawa na **asilimia 44.13** tu ya lengo la makadirio ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti ambao ni **asilimia 66.7.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, uwezekano wa Wizara kufikia lengo la ukusanyaji ni mdogo kwani katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo makusanyo ya wizara yamekuwa chini asilimia 60 ya lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **(fungu 03**) ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 1,018,000,000/=**. Hadi kufikia Februari,2025, Tume ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 497,755,055/=** sawa na **asilimia 48.90** tu ya lengo ikilinganishwa na muda wa utekelezaji wa bajeti ambao umefikia **asilimia 66.7**. Kamati inaitaka Wizara kuongeza usimamizi kwenye Tume ili iweze kufikia malengo ya makusanyo kama ilivyotarajiwa.

**Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2025**

| Fungu | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Wizara(48) | 250,000,000,000.00 | 110,322,568,159 | 44.13 |
| Tume(03) | 1,018,000,000.00 | 497,755,055 | 48.90 |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara, 2025 ana Usanifu wa Kamati*

### 2.1.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara unategemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 48 na Fungu 03 kutoka hazina kama ifuatavyo: -

**(a) Fungu 48: Wizara ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 48 hadi kufikia mwezi Februari, 2025 umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Fedha za matumizi ya kawaida zilipatikana kwa **asilimia 54** ikiwa ni upungufu wa fedha zilizotakiwa katika kipindi kama hicho kwa **asilimia 12.7**

(ii) Katika kiasi hicho cha fedha za kawaida fedha za matumizi mengineyo **(OC)** zilikuwa **asilimia 47** ya fedha zote huku mshahara ikiwa imepatikana kwa **asilimia 60;**

(iii) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa **asilimia 76** ya bajeti; na

(iv) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, fedha za Ndani zilifikia **asilimia 91** na fedha za nje **asilimia 63**. Hata hivyo, katika fedha za ndani **asilimia 77.5** ilikuwa ni fedha ya kulipia madeni mbalimbali ya Wizara.

**Kielelezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 48**

| AINAYA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mshahara | 50,155,528,000 | 29,897,974,318 | 59.61 |
| Matumizi Mengineyo | 36,643,047,000 | 17,402,708,975 | 47.49 |
| JUMLA (A) | 86,798,575,000 | 47,300,683,293 | 54.49 |
| Miradi ya maendeleo | 70,656,510,000 | 48,491,806,442 | 68.63 |
| Kulipa madeni ya Serikali | 36,508,813,000 | 36,508,813,000 | 100 |
| JUMLA | 107,165,323,000 | 85,000,619,442 | 79.32 |

**Mheshimiwa Spika,** kupitia kielelezo **Na. 2** ni wazi kuwa Wizara imepokea fedha za kutosha katika utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye vipaumbele vyake. Kamati inaitaka Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwani Serikali imetoa fedha kwa wakati na kuzingatia umuhimu wa shughuli za Wizara.

**a) Fungu 03: Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**), uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2025 ulionesha mambo yafuatayo: -

(i) Tume ilipokea **asilimia 58.8** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo;

(ii) Fedha za matumizi ya Kawaida zilizopokelewa zilikuwa **asilimia 55.46** ya bajeti yote;

(iii) Katika kiasi hicho cha fedha za matumizi ya kawaida, Fedha za matumizi mengineyo **(OC)** zilipokelewa kwa **asilimia 50.3** na huku mishahara ikiwa imepokelewa kwa **asilimia 59.7;**

(iv) Fedha za miradi ya Maendeleo zilipokelewa kwa **asilimia 63.59** huku fedha zote zikiwa fedha za ndani. Taswira halisi ya mwenendo wa fedha inaonekana katika **Kielelezo Na.03.**

**Kielelezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha (Fungu 03)**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 3,887,780,000 | 2,321,089,000 | 59.7 |
| Matumizi Mengineyo (0C) | 3,244,318,000 | 1,634,467,833 | 50.3 |
| Mradi wa Maendeleo | 5,041,232,000 | 3,205,722,500 | 63.59 |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizar ana usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa upatakinaji wa fedha hauridhishi kwani kiasi kilichopokelewa ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotakiwa kupelekwa kwenye Tume toka Serikalini katika kipindi hicho. Hali hii inaweza kupelekea Tume kushindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyotarajiwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia masharti ya kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026;
(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na
(iii) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi.

### 3.1 Makadirio ya Mapato

**a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa kuhusu lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi ulijikita zaidi kwa kuangalia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inakadiriwa kukusanya maduhuli ya Shilingi **265,000,000,000/=**. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makadirio hayo yameongezeka kwa **shilingi 15,000,000,000** sawa **asilimia 6** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa pamoja na kuongezeka kwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli ni dhahiri kuwa malengo hayo hayawezi kufikiwa. Hii inatokana na ukweli kuwa mwenendo wa makusanyo kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo unaonesha kuwa, Wizara ilishindwa kufikia hata **asilimia 50** ya ukusanyaji wa maduhuli yaliyoidhinishwa.

**b) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu 03** inakadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,018,000,000**.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa lengo la makusanyo katika mwaka wa fedha 2025/2026 linalingana na lile la mwaka wa fedha 2024/2025.

**Kielelezo Na. 4: Mchanganuo wa makadirio ya Maduhuli**

| FUNGU | Mwaka 2024/2024 | Mwaka 2025/2026 | Ongezeko/ punguzo | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wizara (48) | 250,000,000 | 265,000,000,000 | 15,000,000,000 | 6 |
| Tume (03) | 1,018,000,000 | 1,018,000,000 | 0 | 0 |

### 3.2 Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo: -

**a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu - 48)**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 153,437,867,000** ili kuimarisha sekta za ardhi na nyumba nchini. Matokeo ya uchambuzi katika makadirio ya matumizi ya fedha hizo yanaonyesha kuwa: -

(i) Jumla ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeshuka kwa **asilimia 2.6** ikilinganishwa na ya mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Shilingi 4,581,463,000** sawa na **asilimia 5.3** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeshuka kwa kiasi cha **Shilingi 8,598,681,000** sawa na **asilimia 12.2** ikilinganishwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taswira ya makadirio ya matumizi kwa **Fungu 48** wizara inaonekana katika **Kielelezo Na. 5**

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwaka 2025/2026 - Fungu 48**

| AINA YA MATUMIZI | MWAKA 2024/2025 | MWAKA 2025/2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 50,155,528,000 | 53,820,915,000 | 6 |
| Matumizi mengineyo | 36,643,047,000 | 37,559,123,000 | 2.5 |
| **JUMLA** | **86,798,575,000** | **91,380,038,000** | **5.3** |
| Miradi ya Maendeleo | 70,656,510,000 | 62,057,829,000 | 12.2 |
| **JUMLA KUU** | **157,455,085,000** | **153,437,867,000** | **2.6** |

**b) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu – 3).**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Tume,** inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 10,708,185,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ili kuleta ustawi wa wananchi katika matumizi bora ya ardhi nchini. Kamati imechambua na kubaini kuwa: -

(i) Jumla ya bajeti kwa Fungu 03 imepungua kwa kiasi cha **Shilingi 1,465,145,000** sawa na **asilimia 12 .04** kwa waka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **Shilingi 1,055,471,000** sawa na **asilimia 14.8** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imepungua kwa kiasi cha **Shilingi 2,520,616,000** sawa na **asilimia 50** ikilinganishwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taswira ya makadirio ya matumizi kwa **Fungu 03** Tume ya matumizi ya ardhi inaonekana katika **Kielelezo Na. 6**

**Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka 2025/2026 - Fungu 03**

| AINA YA MATUMIZI | MWAKA 2024/2025 | MWAKA 2025/2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 3,887,780,000 | 4,712,143,000 | 21 |
| Matumizi Mengineyo | 3,244,318,000 | 3,475,426,000 | 7 |
| **JUMLA** | **7,132,098,000** | **8,187,569,000** | **14.8** |
| Miradi ya Maendeleo | 5,041,232,000 | 2,520,616,000 | 50 |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizara ya Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitika kuona kuwa matumizi ya fedha za maendeleo yamepungua kwa takribani asilimia 50 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2024/2025. Hali hii inatoa tasfiri kuwa, katika mwaka ujao wa fedha, Tume inatarajiwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo machache zaidi. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza fedha za maendeleo ili kuiwezesha Tume kutekeleza zoezi la kuandaa Mipango ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo mengi zaidi.

### 3.3 Mambo muhimu yanayogusa Sekta ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kujadili mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilibaini mambo muhimu yanayogusa Wizara hii kama ifuatavyo: -

(a) **Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya Serikali kuhusu mradi huu ambapo ilibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilipanga kutekeleza Programu hii kwa kutumia Mfuko wa Plot Development Revolving Fund (PDRF). Katika program hii Wizara ilipanga kupima na kutoa Hati za Kumiliki Ardhi **100,000** (CRO) za viwanja vipya na vya Urasimishaji ifikapo Juni, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepima viwanja **8,049** katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, taarifa ya Wizara kuhusu mradi huu inaonesha kuwa Vifaa vya kuandalia hati vimenunuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, kasi ya utekelezaji wa mradi wa KKK ni ndogo sana kulinganisha na lengo lililokusudiwa. Wizara imeweza kupima **asilimia 8.05** tu ya viwanja vilivyopangwa hadi kufikia Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inaongeza kasi katika utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi ili kuweza kufikia lengo walilokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025

(b) **Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).**

Ibara ya 76 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 iliitaka Serikali Kuendelea kuboresha na kuimarisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Pamoja na majukumu mengine, Shirika lilitakiwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za majengo makubwa ikiwemo Morocco Square, Kawe 711, Golden Premier Residence na Mradi wa Kiwanja Na. 300 Regent Estate katika jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea na ujenzi wa nyumba 422 katika mradi wa Kawe 711 unaotarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2026. Vilevile, Shirika lipo katika mchakato wa kufanya upembuzi yakinifu na manunuzi katika ujenzi wa nyumba 196 katika mradi wa Golden Premium Residence (GPR) na Kiwanja namba 300 Regent Estate ambapo ujenzi wake unategemea kuanza ndani ya mwaka ujao wa fedha. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inashughulikia changamoto ya wakandarasi na Shirika ili miradi hiyo itekelezwe kwa ufanisi.

(c) **Migogoro ya Ardhi Nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi katika nchi yetu haswa ya wanachi kumavamia maeneo ya Taasisi za Serikali, mashamba ya Serikali na hata ya maeneo ya watu

binafsi. Hali hii inapelekea kuzalisha migogoro kati ya Serikali na *wananchi, na wananchi na wananchi.*

**Mheshimiwa Spika,** kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali katika kutatua migogoro hiyo hata hivyo kamati inaishauri Wizara kuweka mpango madhubuti wa kukabiliana na migogoro hiyo ili isiwe ya kujirudia na kuepusha madhara yanayotokana na migogoro hiyo ikiwa ni uvunjifu wa amani na kukwamisha shughuli za uzalishaji.

(d) **Ulipaji wa Fidia ya Ardhi kwenye maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya Miradi ya Serikali na Uwekezaji.**

**Mheshimiwa Spika,** Fidia ni malipo yanayotolewa kwa mtu au taasisi kama mbadala wa mali yake au kutokana na kuondolewa kwenye eneo lake linalotwaliwa kwa manufaa ya umma au kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa. Ili kukadiria kiasi cha fidia kitakacholipwa kwa mwananchi ambaye mali zake zimetwaliwa kwa manufaa ya umma, sheria inaelekeza kuwa thamani ya mali hizo zinapaswa kukadiriwa na mthamini aliyesajiliwa na bodi ya wathamini.

**Mheshimiwa Spika,** katika ulipaji wa fidia hiyo, Kamati imebaini kuwa kuna changamoto ya ucheleweshaji wa malipo ya fidia kwenye maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili matumizi mbadala. Uchelewashaji wa malipo ya fidia unatokana na zoezi la uhakiki (financial verification) kuwa la muda mrefu na kukosekana kwa fedha katika mfuko wa Fidia ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuondoa changamoto hii. Aidha, Serikali ihakikishe kabla ya kufanya uthamini wa ardhi inakuwa na fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi watakaokuwa wametwaliwa maeneo yao.

**SEHEMU YA NNE**

# 4.0 MAONI YA USHAURI

## 4.1 Maoni ya Jumla

(i) Wizara iongeze jitahada za kuweza kupima na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vyote ili kuondoa migogoro ya ardhi nchini;

(ii) Wizara ihakikishe inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama yalivyopangwa kwenye bajeti; na

(iii) Wizara ihakikishe inasambaza Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa huduma za Ardhi (e-ardhi) katika Mikoa yote nchini.

## 4.2 Ushauri wa Kamati

### 4.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwani Wizara hii imekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji;

(ii) Irejeshe utaratibu wa kodi ya pango la ardhi (Land Rent) kukusanywa na Wizara ambayo ndio ina nyenzo za kisheria na mifumo ya ukusanyaji wa kodi hiyo; na

(iii) Iihakikishe inatengeneza mipango na mbinu za kufuatilia wadaiwa wa pango la ardhi ili kuweza kuongeza mapato ya Wizara.

### 4.2.2 Mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi (KKK)

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Iongeze kasi ya Kupanga na kupima ili kufikia lengo la viwanja 100,000 hadi kufikia Juni, 2025;

(ii) Ihakikishe Wizara inashirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhimiza wakurugenzi wa halmashauri ambazo hazijarejesha fedha hizo kurejesha fedha hizo ili kufanya proramu ya KKK kuwa endelevu katika halmashauri zote nchini;

(iii) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu manufaa ya kumiliki ardhi kwa njia rasmi hali itakayochochea wananchi wengi kulipia hati za umiliki wa maeneo yaliyopimwa kupitia mradi wa KKK; na

(iv) Iongeze idadi ya wasimamizi wa mradi ili kuongeza ufanisi wa programu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

### 4.2.3 Mfumo Unganishi wa Kielekroniki wa Huduma za Ardhi (e-Ardhi)

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe inaongeza kasi ya kusambaza Mfumo wa eArdhi kwenye halmasahuri zote nchini ili shughuli zote za Ardhi zifanyike kwenye mifumo;

(ii) Ihakikishe inafanya maboresho ya mfumo ili uwe rafiki kwa watumiaji; na

(iii) Ihakikishe inatoa elimu kwa Maafisa ardhi na wananchi wote kuhusu Mfumo wa utoaji huduma katika usimamizi wa Ardhi.

### 4.2.4 Changamoto ya Ukosefu wa wakaguzi majengo nchini

Kamati inashauri Serikali kuwa ihakikishe inaajiri wakaguzi majengo katika Halmashauri zote ili kuzuia ujenzi holela nchini;

**4.2.5 Ucheleweshaji wa Fidia ya Ardhi katika Maeneo yaliyofanyiwa Uthamini**

Kamati ianashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe inakuwa na fedha kabla ya kuanza zoezi la kufanya uthamini na mchakato wa utwaaji wa ardhi ya wananchi;

(ii) Ifanye marekebisho ya Sheria kwa ajili ya kuufanya mfuko wa fidia ya ardhi nchini kuwa chini ya mthamini Mkuu wa Serikali.Hali itakayomfanya mthamini mkuu wa Serikali kujua uwezo wa mfuko kabla ya kwenda kufanya uthamini.

**4.2.6 Migogoro ya Ardhi Nchini**

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe kuwa inakuwa na kanzidata ya maeneo yote yaliyopangwa na kupimwa ili kuwezesha wananchi kufanya ujenzi wa makazi kwenye maeneo rasmi nchini;

(ii) Ihakikishe inaandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuondaoa migogoro inayojitokeza hapa nchini; na

(iii) Ihakikishe Clinic za Ardhi zinakuwa endelevu na zifanyike kwa mikoa yote ili kuendelea kupunguza migogoro ya ardhi.

**4.2.7 Wawekezaji wakubwa katika Sekta ya Ardhi ambao Hawajaendeleza Maeneo yao**

Kamati inasahuri kuwa, Serikali: -

(i) Ihakikishe inafanya tathimini ya wawekezaji katika sekta ya ardhi nchini ili kutambua hali ya uendelezaji wa maeneo hayo; na

(ii) Ichukue hatua kwa wawekezaji ambao wameshindwa kuendeleza maeneo yao kwa kuzingatia Sheria.

**4.2.8 Ufinyu wa Bajeti katika Tume ya Taifa ya mipango ya ardhi**
Kamati inashauri Serikali kuwa, iongeze fedha za maendeleo ili kuiwezesha Tume kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji vingi nchini.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya kamati napenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu katika kulisimamia na kuliwezesha Bunge letu kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza na kumshukuru sana **Mhe Deogratius John Ndejembi (Mb),** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mhe.Geophrey M. Pinda (Mb) Naibu Waziri kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara chini ya Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu Ndg.Lucy Kabyemela kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na usimamizi mzuri wa majukumu ya wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee nawapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa waliofanya hadi taarifa hii inaingia Bungeni. Majina ya wajumbe hao yameorodheshwa katika taarifa hii ila kwa sababu ya changamoto ya muda naomba majina yao yaingie kwenye taarifa rasmi za Bunge yaani Hansard.
Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Timotheo P. Mnzava, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb - Mjumbe

4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Askofu Josephat M. Gwajima, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Neema William Mgaya, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Innocent Bilakwate, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Dkt Florence G. Samizi, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Shaban Omari Shekilindi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Asha Juma Abdallah, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, naomba nimalize kwa kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Timotheo P. Mnzava, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

29 Mei, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, ambao ni Kamati ya Utawala za Mitaa, Makazi na Masuala ya Uongozi kutoka Bunge la Zambia. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Twambo Mutita, Mwenyekiti; Mheshimiwa Anthony Kasandwe, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Imelda Munashambatu, Mjumbe; Mheshimiwa Paul Chala; Mheshimiwa Christopher Kagombe; Mheshimiwa Henry Sikazwe; Mheshimiwa Kenisia Chisumo; Mheshimiwa Kabaso Kampampi; Mheshimiwa George Kendafuru; Mheshimiwa Timothy Rumba ni Katibu wa Kamati. *Welcome to the Parliament of Tanzania and ulibwanji. (Makofi)*

Mheshimiwa Matiko ana mgeni wake Ndugu *CEO* wa Jona Jovan, *Business Solution Limited* (Kampuni ya Ushauri Masuala ya Rasilimali Watu). Karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaanza michango. Mheshimiwa Mnzava, Mheshimiwa Kunambi na Mheshimiwa Chege wajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango kwenye Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujaalia uzima, lakini anaendelea kutuwezesha kuendelea kuwa kwenye nyumba hii, kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya yeye na timu yake pale Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa ufafanuzi wa

mambo yote makubwa na ya msingi ambayo Watanzania wa nchi hii wanatamani kuyasikia kwenye eneo la sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hotuba hii, ni matumaini yangu kama ambavyo taarifa ya Kamati yetu imeunga mkono Hoja ya Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge tutaungana pamoja kuipitisha Hoja ya Mheshimiwa Waziri na kuiunga mkono, ili wakaendelee kufanya kazi ya kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hizi nzuri tunasema Mheshimiwa Waziri na timu yake wanafanya Wizarani. Nina mchango kwenye maeneo manne madogo sana ambayo ni ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza; wakati wa kujadili Bajeti ya Hotuba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nilisema kidogo. Nchi yetu kwenye miaka ya 1990 tuliamua kuingia kwenye mfumo tukaleta sera mpya ya ugatuaji wa madaraka kwa maana ya *D* by *D*. *(Decentralization by Devolution)*. Lengo letu kubwa lilikuwa ni kusukuma madaraka kwa wananchi kule chini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa Hotuba ya Bajeti ya TAMISEMI tuliwashauri wenzetu TAMISEMI na tunashukuru walituikia na wakatuahidi kufanyia kazi. Kwamba, umefika wakati sasa wa kufanya mapitio ya sera ya ugatuaji wa madaraka ili kuona ufanisi wake na kuona changamoto zake na kuona namna gani ya kuhangaika nazo, ili kuboresha mfumo wa utawala kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona TAMISEMI wenyewe walipoona barabara ujenzi unasuasua walianzisha *TARURA,* lakini upande wa maji tulipoona mambo yanasuasua tulikuja na *RUWASA*. Baadaye tuliona Serikali imechukua hatua ya kuwahamisha watumishi wa ardhi kutoka kuitika moja kwa moja halmashauri na kusimamiwa moja kwa moja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni zuri, lakini bado tunayo changamoto. Kumekuwa na makanganyiko wa utendaji na kimajukumu kule kwenye halmashauri zetu. Zipo baadhi ya halmashauri ambazo zimedhani kwamba Maafisa Ardhi kwa sasa siyo sehemu ya utendaji kazi wa halmashauri kwa sababu tu wanasimamiwa kinidhamu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hiyo, kuna changamoto nyingine, ukisoma taarifa ya Kamati yetu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo nyuma, Wizara ya Ardhi haijawahi kufikia 80% ya malengo ya makusanyo yake. Ukifanya uchunguzi wa kina sababu haiwezi kuwa ni uzembe, zipo sababu nyingi za kimfumo, kisheria ambazo zinafanya Wizara hii ishindwe kufikia malengo kwenye ukusanyaji. Moja ya sababu hiyo ni mkanganyiko wa kisheria, kiutendaji kati ya halmashauri na Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili nimekusikia Mheshimiwa Waziri umesema na Mheshimiwa Rais wakati mnazindua Maboresho ya Sera ya Ardhi alitoa maelekezo. Tunaomba jambo hili wakaliwekee mkakati madhubuti, wakalifanye. Tuleteeni Kamisheni ya Ardhi, tuwe na chombo maalum na mahsusi cha kusimamia ardhi kwenye nchi yetu kuanzia juu mpaka chini. Kusiwe na mifumo mingi, sheria nyingi na mamlaka nyingi. Tuleteeni Kamisheni ya Ardhi kwenye nchi hii tuwe na mfumo mmoja ambao unaeleweka wa kusimamia sekta ya ardhi kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; tafiti duniani zinaonesha kwamba moja ya njia bora za kuondoa changamoto ya migogoro ya ardhi hasa kwa maeneo ya vijijini ni kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji. Jambo hili ni kubwa sana, kupanga mipango lakini na kwenda kuisimamia. Katika vijiji zaidi ya 12,000 tulivyonavyo kwenye nchi hii mpaka mwaka wa fedha 2021/2022 tulikuwa tumetengeneza mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji kwenye vijiji 2,600 na kidogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka hii miwili tuipongeze Serikali tumefika vijiji 4,822. Hatua hii ni kubwa kwa sababu tumeongeza vijiji zaidi ya nusu au mara mbili ya tulivyokuwa tumefanya mpango wa matumizi bora ya ardhi ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili halipaswi kuachwa, linapaswa kuwa endelevu. Ili jambo hili liweze kuwa endelevu ni lazima Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi itengewe fedha za kutosha kwa ajili ya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kwenye Taarifa yetu ya Kamati; pamoja na kazi nzuri ambayo Kamati na Bunge tunatambua kwamba Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inafanya, bado kumekuwa na changamoto ya kupata fedha za kugharamia miradi ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti anayoomba Mheshimiwa Waziri fedha za maendeleo kwa Tume zimepungua kwa zaidi ya 50% ukilinganisha na fedha zilizokuwa zimetengwa mwaka jana yaani mwaka wa fedha 2024/2025. Mwaka wa fedha unaokwisha Juni, 30 mwaka huu 2025. Tume walitengewa fedha za maendeleo bilioni tano. Mwaka huu wa fedha yaani 2025/2024 tunaoenda kuuanza au bajeti inayoombwa Tume imetengewa bilioni 2.5 ni zaidi ya 50% ya fedha zimepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira kama hayo Tume hii haiwezi kufanya kazi vizuri. Haiwezi kuleta matokeo tunayoyatarajia kwa sababu Tume hii haina fedha. Tunajua bado bajeti hii haijakwisha, mchakato wa bajeti unaendelea mpaka siku utakapopitisha sheria ya matumizi ndani ya Bunge hili. Ni wakati wa Serikali kwenda kuangalia upya, tuone namna ya kuiongezea Tume ya Mipango fedha, ili ifanye jukumu lake la kutengeneza mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ninalotaka kushauri ni kwa upande wa Shirika la Nyumba la Taifa. Shirika letu la Nyumba la Taifa linafanya kazi kubwa na nzuri sana na tunaridhika na kazi wanayofanya. Miradi yote ya kimkakati ambayo ilikuwa imesimama kwa muda mrefu, kwa busara na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, miradi ile imeamika na sasa hivi kazi zinaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo uligusia awali na Mheshimiwa Rais siku ya kuzindua maboresho ya sera alisema; kiu ya Watanzania wa nchi hii ni kupata nyumba au makazi kwa bei nafuu zaidi, kupata makazi kwa gharama ambayo ni nafuu. Pamoja na jtihada za Shirika la Nyumba la Taifa kujenga nyumba za gharama nafuu, lakini bado hazijawa nyumba za gharama nafuu kwa kiwango ambacho wanaweza kukimudu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika letu linafanya shughuli za kibiashara, lakini ni ukweli kwamba siyo kwamba hawapendi tu kujenga nyumba za gharama nafuu, yapo mambo mengine humu ndani ikiwemo sera zetu za kikodi ambazo zinasababisha bei ya nyumba hizi iwe juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati sahihi sasa Mheshimiwa Waziri, Shirika la Nyumba na Wizara wafanye tathmini ya kina ili tupate nyumba na makazi ya gharama nafuu kwa Watanzania. Kuna changamoto na vikwazo gani vya kikodi, kibiashara na kisheria, ili tuipelekee Serikali iamue kufunga mkanda, tukubali kupunguza baadhi ya maeneo, tukubali kusamehe baadhi ya kodi ili tuliwezeshe Shirika la Nyumba la Taifa kutengeneza makazi ya gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kufanya hivyo ni jambo gumu. Shirika hili linajenga kama anavyojenga mtu mwingine binafsi, linanunua vifaa kama anavyonunua mtu mwingine binafsi, wanakatwa kodi kama wanavyokatwa mashirika mengine. Ni ngumu kupata nyumba za gharama nafuu bila kuangalia sana mfumo wa kikodi ili kuwezesha Shirika hili liweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho nililokuwa ninataka nishauri; nimpongeze sana Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia.

**MHE. TIMOTHEO PAUL MNZAVA:** Amefanya kazi kubwa kwenye kubatilisha miliki na mashamba makubwa ambayo yalikuwa hayajaendelezwa na ninaipongeza Wizara inafanya kazi kubwa sana. Kama Mheshimiwa Rais alivyotoa maelekezo, endeleeni kufanya tathmini juu ya maeneo haya, ili tuwasaidie Watanzania waweze kupata ardhi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji ili maisha yao yaendelee kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono Hoja ya Mheshimiwa Waziri na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuiunge mkono. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kunambi, wajiandae Mheshimiwa Chege na Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuwa sehemu ya wachangiaji katika Hotuba ya Bajeti hii ya Wizara ya Ardhi. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, ni Rais anayefanya mabadiliko katika sekta mbalimbali ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aya ardhi kaka yangu Deodatus Ndejembi. Nieleze haiba kidogo ya Mheshimiwa Waziri, ninadhani pia na Waheshimiwa Wabunge wataniunga mkono. Mheshimiwa Deo Ndejembi, ni Waziri kijana na siyo tu kijana ni Waziri ambaye ana *fresh mind in a changing world.* Ni kijana ambaye ana fikra mpya katika ulimwengu unaobadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akiwa Naibu Waziri, Wizara ya Utumishi na Utawala Bora alikuwa anamsaidia mama yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama. Nilisimama hapa Bungeni na hoja ya kueleza mapungufu ya *OPRAS*. Bila shaka alimshauri Waziri wake wakafanya mabadiliko katika usimamizi wa Sekta ya Utumishi wa Umma, wakaja na Mifumo miwili ya *PEPMIS* na *PIPMIS, OPRAS* wakaachana nayo. Ndiyo maana nikasema leo sishangai haya yanayotokea kwenye Wizara ya Ardhi, kwa sababu ndiyo haiba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nimefika kwenye Bunge hili niimekuwa nikijenga hoja kwa habari ya ardhi na kwa nini leo hii ninampongeza Waziri? Ninampongeza kwa sababu amekwenda kumheshimisha Mheshimiwa Rais, kwenye hotuba yake. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuja na utashi wa kisiasa wa kuona sasa ana kusudi la kwenda kutatua migogoro ya ardhi kwa suluhisho la kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa migogoro ya ardhi inatatuliwa kwa njia kuu mbili; ya kwanza, ni njia ya mahakama; na ya pili, ni njia ya utawala kwa mujibu wa sheria za nchi, lakini njia za utawala ni njia za *temporary* siyo za kudumu. Sasa, leo hii tunaona Mheshimiwa Rais ameelekeza na Waziri unatuletea hapa Bungeni, wanakwenda kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Matumizi Bora ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa ninaomba nieleze kidogo. Kamisheni ya matumizi bora ya ardhi ndiyo inayokwenda kutatua migogoro ya ardhi nchini kwa suluhisho la kudumu. Sasa, nieleze kwa nini inakwenda kutatua? Kamisheni hii inakwenda kuwa kama chombo cha kusimamia sekta ya ardhi. Nami nishauri na katika hitimisho ninadhani utasema kidogo. Hii Kamisheni ni lazima iwe na *instrument: instrument* ya Kamisheni hii ni *National Land Use Master Plan.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, ndiyo utakaosaidia kusimamia mipango kabambe yote kwenye halmashauri. Kwenye halmashauri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ni lazima twende na kasi ya

Wizara ya Ardhi kwenye kupanga na matumizi bora ya ardhi ya nchi yetu, kwa sababu wewe ni mdau muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Matumizi Bora ya Mipango Miji Na.8 ya mwaka 2007, halmashauri ndiyo mamlaka za upangaji. Sasa, ni lazima halmashauri nazo ziwe na *Land Use Master Plan* na *Infrastructures Master Plan* (Mipamgo Kabambe ya Matumizi Bora ya Ardhi na Mipango Kabambe ya Miundombinu), maana yake nini? Hii *National Land Use Master Plan* itasimamia katika halmashauri mipango kabambe ya matumizi bora ya ardhi na *infrastructures.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, hayo ndiyo majukumu ya Kamisheni sasa iende ikafanye. Kwa mfano, yapo maeneo yameshapangwa, lakini tunaona bado kuna ujenzi holela. Sasa, Kamisheni hii itatusaidia kupitia, lakini sasa niseme ili kuondoa kuwa na taasisi nyingi kwenye Wizara moja, Kamisheni hii ninashauri iwe chini ya Kamishna Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui watakavyopanga, lakini ninatamani kuona Kamishna Mkuu wa Wizara anakuwa ni sehemu ya Kamisheni. Isipokuwa Kamisheni hii isimamie Tume ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi, pia isimamie *RERA*. Kwa kweli Waziri ninakushukuru *Real Estate* ni sekta muhimu katika uchumi wa nchi yetu, vijana wengi wanafanya huko shughuli zao na kwa kweli imekuwa ikikua kwa kasi sana miaka ya hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spia, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, na nimpongeze Waziri kwa kuja na *RERA (Real Estate Regulatory Authority)*. Mamlaka ya usimamizi wa sekta hii ya *Real Estate* itasaidia kusimamia hawa *stakeholders* (wadau) wa *Real Estate* ambao waliachwa kama watoto yatima leo hii wanakwenda kuwa na chombo cha kuwaratibu. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe tu kusema migogoro ya ardhi mingi imekuwa ikitokea nchini siyo tu kwa sababu. Sababu tuliyokuwa nayo kubwa ni kwa sababu bado hatujakamilisha kupanga na kupima nchi yetu. Nchi hii ikipangwa, ikapimwa vizuri

na wananchi wakamilikishwa ardhi yao, ninadhani hili tatizo la migogoro ya ardhi linakwenda kutatuliwa, kwa sababu tunafahamu katika Taifa letu tuna ardhi za aina tatu. Kuna ardhi ya jumla, ya hifadhi na ardhi za vijiji, sasa maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, unavyofanya *land administration* Waziri wa Ardhi anaposimamia sekta, yeye siyo mtu wa mwisho kwenye kutatua migorogo ya ardhi, mtu wa mwisho ni mahakama na ndiyo maana nikasema migogoro ya ardhi nchini bado haiishi. Kwa hiyo, bado ninaendelea kusema, kupitia Kamisheni itakwenda kutusaidia nchi yetu ipangwe, ipimwe na wananchi wamilikishwe vipande vyao ya ardhi. Hii itaondoa kwa kiwango kikubwa migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapo kidogo, lakini matumizi ya TEHAMA ni muhimiu nayo nikayasema. Kwa hiyo, ninavyosema Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni *transformative leader* maana yangu ni nini? Ni Rais anayepokea na kutaka mabadiliko. Ndugu zangu haya mambo ninayosema leo siyo madogo kwenye sekta ya ardhi. Nchi yetu imekuwa ni nchi ambayo imepata changamoto nyingi sana kwenye sekta ya ardhi hasa hasa migogoro ya ardhi. Wenzetu majirani na nini huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii inayokwenda kufanywa na Mheshimiwa Waziri nimwombee, ikimpendeza Mheshimiwa Rais na Wananchi wa Chamwino, ashinde kuwa Mbunge, lakini Mheshimiwa Rais ampatie tena uwaziri wa Wizara hiyohiyo, ili kusudi haya unayosema yanayopangwa hapa akayasimamie. yeye ni kijana ninasema ni *fresh mind in a changing world. Brother may God bless you.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nieleze kidogo kuna kadhia kwenye halmashauri, kuna ombwe kwenye halmashauri. Sasa, halmashauri wanasema sisi mamlaka za upangaji Sheria Na.8 ya 2007 ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi, inatambua halmashauri zote nchini kama ndiyo mamlaka za upangaji. Sasa, Waziri wa Ardhi anaunda Kamisheni anakwenda kupoka majukumu ya Madiwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nimwombe atoe ufafanuzi kidogo, ili awaeleze wasio na mashaka Kamisheni hii inakwenda kusaidia halmashauri kuimarika katika sekta ya ardhi, wana sehemu yao kama mamlaka ya upangaji. Hiyo sehemu ni muhimu akaitolea ufafanuzi ili Watanzania wajue.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho nihitimishe, Mheshimiwa Waziri nikuombe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungamzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nihitimishe. Waziri ni mtu muungwana sana, nimwombe ikimpendeza Jimbo langu la Mlimba kuna migogoro mingi sana ardhi fanya siku moja ziara walau apite kule na yeye ni rafiki yangu katika hili Mungu atambariki sana na aseme neno moja tu na wananchi wa Mlimba watapona. Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chege, wajiandae Mheshimiwa Lusinde na Mheshimiwa Asenga.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza, nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; kipekee kabisa nichukue nafasi kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo kadhaa, lakini nitataja matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninaingia kwenye Bunge hili mara ya kwanza nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii. Nje ya hivyo nimekuwa niki-*declare interest* mara zote ambazo ninachangia kwenye wizara hii kwamba, mimi ni mdau wa sekta ya ardhi, pia ndiyo *professional* yangu ambayo imenikuza kwa miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo makubwa matatu ambayo yamekuwa yakizungumzwa kwenye taarifa zote za kamati na michango ya Bunge hili. Moja; tumekuwa tukizungumzia sana umuhimu wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995. La pili; tumekuwa tukizungumzia umuhimu wa *RERA (Real Estate Regulatory Authority)*. Pia, tatu; tumekuwa tukizungumzia sana Kamisheni ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nimeanza kutangulia kwa kipekee kabisa kuchukua nafasi kwa moyo wangu wa dhati kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu haya yote matatu ambayo tumekuwa tukisema kwenye Bunge hili kwa miaka minne, kwenye Taarifa zetu za Kamati, kwenye michango ya Wabunge na ndiyo yamekuwa mapendekezo ya Kamati kwa miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona wakati huu wa Mheshimiwa Waziri Ndejembi, yametekelezwa na yamefanyika vizuri sana. Mheshimiwa Ndejembi hongera sana wewe pamoja na Naibu Waziri wako, watumishi wote wa Wizara kwa kweli wametufikisha vizuri sana. Hili si tu kwamba wamekosha Bunge lakini mmekidhi haja ya wadau wa sekta ya ardhi nchini. Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995, tumekuwa tukiisemea sana ifanyiwe mabadiliko ili iendane na kasi ya ukuaji wa uchumi na sekta ya ardhi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 tumekuwa tukiisemea sana ifanyiwe mabadiliko ili iendane na kasi ya ukuaji wa uchumi, iendane na kasi ya ukuaji wa Sekta ya Ardhi nchini, lakini maeneo mengine ilikuwa inamwacha mwanamke katika sekta ya umiliki wa ardhi hasa sehemu ya mirathi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwenye Sera ya Taifa ya Ardhi tumeona inakwenda kumweka mwanamke kutambulika kumiliki ardhi, hata akinamama ambao wanakaa vijijini ambao kimsingi kwenye umiliki wa ardhi hasa maeneo ya mirathi walikuwa wameachwa, walikuwa hawana haki ya kumiliki ardhi, lakini sera hii inakwenda kutambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyasema wakati anazindua sera hii, lakini pia malengo ambayo ameyaainisha kwenye taarifa yake na haya ambayo tumeyasema leo kupitia Bunge hili, nenda ukayafanye ili uweze kuboresha Sera hii ya Taifa ya Ardhi na iweze kufanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningetamani kwenye maeneo hayo ni kutambua mabadiliko ya kanuni na sheria mbalimbali kwenye sekta ya ardhi ambazo zinashabihiana na sekta ya ardhi nchini. Waziri anapofanya mabadiliko ya sera lazima aende akatambue sheria mbalimbali ambazo zinashabihiana na sekta ya ardhi nchini ili na zenyewe ziweze kufanyiwa mabadiliko ziendane na kasi yake na ziendane na dhamira na mwelekeo wa Mheshimiwa Rais nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema pia, lazima iendane na mabadiliko ya sheria na kanuni ya Wizara ya Ardhi peke yake. Kwa sababu zipo sheria, kama tunavyosema kwamba mwanamke sasa anakwenda kumiliki ardhi, tusipofanya mabadiliko ya Sheria ya Mirathi ya Ardhi maana yake itakuwa sera ipo, lakini mwanamke bado atakuwa hatambuliki katika umiliki wa sekta ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba pia Mheshimiwa Waziri tena katika sekta hii kwamba Mamlaka za Upangaji na Upimaji, sheria inasema hivyo, tunatambua sheria inasema kwamba, mwenye mamlaka ya upangaji na upimaji ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, atengeneze *connection* kati ya Wizara ya TAMISEMI na Wizara yake kwa kutambua sera mama ili angalau sera hii iende ikatengeneze usimamizi mahiri, kwenye usimamizi kwa upande wa TAMISEMI, Wakurugenzi waweze kusimamia hili zoezi ambalo linatamkwa kwenye sheria lakini halifanyiki vile ambavyo inapaswa kufanyika kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri lazima atambue kwamba mfumo wa usimamizi wa ardhi nchini siyo rafiki

sana. Mfumo wa usimamizi wa ardhi nchini hauko rasmi kwa sababu hatuna chombo kinachosimamia *Real Estate Regulatory Authority*. Hatuna chombo kinachosimamia watu wa *Real Estate Agent*, hatuna chombo kinachosimamia *Real Estate Developers Consultant*, hawa *brokers* ambao wanafanya kazi zao. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuja na *RERA*. Nimeona sasa wanakwenda kuunda hii taasisi, kuunda mfumo ambao utawaratibu na kuwasimamia hawa watu, hawa watu hawakuwa wanatambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *National Housing* anafanya kazi ya usimamizi wa miliki, lakini zipo *private company* nyingi zinafanya kazi ya usimamizi wa miliki lakini hazitambuliki. Hazina *Regulatory* ambayo inawaongoza namna nzuri ya kwenda na kwa kutokuwa na usimamizi mahiri maana yake Serikali inakosa kodi, wao wanakuwa hawatambuliki na hata wao wanakosa wakati mwingine mikopo kwenye taasisi za Serikali kwa sababu hawaeleweki wako wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri hii *RERA, Real Estate Regulatory Authority* Mheshimiwa Waziri ipe kipaumbele sana kwa sababu watu wengi ambao ni *brokers* na *Real Estate Agent* wanakwama kwa sababu ya ukosefu wa kuwa na sheria ambayo inawasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hili lipo jambo lingine ninaomba nimshauri Waziri. Ni kwenye mkopo wa KKK - kwenye Kupanga, Kupima na Kumilikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha kwa miaka mingi mfululizo. Tumeona alitoa mara ya mwisho bilioni 50 kwenda kwenye Mamlaka za Upangaji na imetumika kwenye kupanga maeneo mengi nchini na kwenye Halmashauri. Ninamwomba tuzingatie mambo mawili. Pamoja na kuwa tumegundua kwamba kuna changamoto kubwa sana fedha hizi namna ya kurudi, baadhi ya Halmashauri hazirudishi fedha ipasavyo. Ninaomba mambo mawili haya angeyafanyia kazi ili angalau hizi fedha ziendelee kuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, wakati mikataba inasainiwa kati ya wakurugenzi na Wizara ya Ardhi, lazima TAMISEMI ihusike. Husisha TAMISEMI kama wasimamizi wa Wakurugenzi wale mnaosaini nao mikataba. Pili, anayetakiwa kuhusika, ni lazima umhusishe *RAS* wa Mkoa ili atambue na akusaidie namna ya kusimamia zile fedha zinazokwenda kwenye taasisi, kwenye maeneo ya Wakurugenzi. Haya mawili Mheshimiwa Waziri akiyafanya, itatusaidia sana kuhakikisha fedha hizi zinarudi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Wizara ya Fedha ihakikishe na yenyewe inahusika kwenye mkataba ule ili kurahisisha kusaidia zile fedha kurudi kwa wakati. Leo tunatoa bilioni 50, lakini Waziri mwenyewe anaona changamoto namna ya fedha hizi zinavyorudi, hii fedha ni *revolving*, inatakiwa irudi ili halmashauri zingine ziweze kupewa fedha, lakini hazirudi kwa wakati. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri hili alione na aone namna ambavyo wanaweza wakalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine Mheshimiwa Waziri nimesema hapa ni *Commission* ya Ardhi Nchini. Kunakuwa hakuna *connection* kati ya Wizara ya Ardhi ambao ndiyo wanasimamia *policy*, TAMISEMI wanaosimamia sheria za utekelezaji wa ardhi, pamoja na watendaji wa maeneo yote mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Commission* hii inakwenda sasa kuwa sehemu ya kusimamia yote mawili, inakwenda kusimamia utendaji wa Wizara ninyi wenyewe kwa yale yote wanayozungumza katika kupanga, kumilikisha ardhi, lakini pia inakwenda kuwa sehemu ya katikati kama *broker* au kuwarahisishia mahusiano yao wao na Wizara ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Kwanza itarahisisha upangaji na upimaji kwenda kwa kasi, itarahisisha *master plan* ambayo tumeizungumza ya sekta ya ardhi nchini itakwenda kwa kasi, pia itawasaidia kuondoa hilo *gap* ambalo

mnalo kati ya sekta ya ardhi kwa maana ya Wizara ya Ardhi na TAMISEMI nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuliona hili, kuanzisha *Commission* ya Ardhi, nimeona hapa anasema anaianzisha, hii iende kwa kasi kwa sababu kuna wakati hawakutani sekta ya ardhi na mipango au usimamizi wa sera na kule wasimamizi wa utekelezaji wanaotekeleza sheria, hawana namna ambavyo wanakutana ili kuhakikisha haya wanayafanya. Akiwa na *Commission* ya Ardhi itamsaidia sana Waziri angalau kufanya *regulation* na kuhakikisha kwamba haya mambo yote yanakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine amelisema Mwenyekiti wa Kamati hii, juu ya utengano wa watumishi wa ardhi, hasa Maafisa Ardhi, *Surveyors*, *Town Planners,* hawa ambao wanaitika wako chini ya Kurugenzi, lakini wanaitika ndani ya Wizara. Huu mkanganyiko kwamba wako chini ya Mkurugenzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini wanawajibika kwenye sekta kwenye Wizara ya Ardhi nchini, kuna mkanganyiko mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mwenyekiti ni kwamba, wakati mwingine Wakurugenzi wanashindwa kuwatambua kama wako chini yao, kuna wakati mwingine wanapata maelekezo kutoka Wizara ya Ardhi juu ya jambo lolote linalotakiwa kufanywa kwenye sekta ya ardhi, hapo hapo anapata maelekezo kwa Mkurugenzi ambaye ndiyo bosi wake kwenye eneo lile la Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ile *contradiction* inawafanya wale watu wanashindwa kuelewa wasimamie lipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba sasa Mheshimiwa Waziri akae na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI waamue hawa watumishi wakae upande upi. Ndiyo maana maeneo mengi hawa watu wanapata lawama kubwa sana, kwamba wanashindwa kutatua migogoro au wanashindwa ku-*meet* ile *objective* ambayo wamewapa ni kwa sababu ya hiyo *contradiction,* anapata maelekezo kwenye Wizara mbili tofauti,

matokeo yake ni kwamba wanashindwa kusimamia na hawajui wasimamie lipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa hili Wakurugenzi wako chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wala hakuna sababu, wawarudishe kama walivyokuwa zamani, warudi kule chini ili wasimame kwenye *command* moja, ikitoka Wizara ya TAMISEMI inashuka mpaka kwa watumishi inakwenda, kuliko hivi ambavyo iko ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa mud awa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie jambo la mwisho kabisa ambalo ni kubwa ninatakiwa kulizungumza ni juu ya kupunguza gharama ya kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wamepunguza kiasi kikubwa sana cha fedha kwa wananchi wanaotaka kumiliki Hati ya Umiliki wa Ardhi nchini, ninamwomba sana hili Kamishna wa Ardhi atoke atoe semina kwa wananchi, ajue namna Mheshimiwa Rais alivyokubali na ameridhia kupunguza bei ya wananchi sasa kumiliki ardhi, zaidi ya asilimia kadhaa kwenye eneo hili ili angalau uweze kuongeza umiliki wa hati na ndiyo sehemu pekee inayoweza kutatua changamoto za ardhi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na naunga mkono hoja. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa nzuri, hongera sana Wizara ya Ardhi pamoja na watumishi wote. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, jiandae Mheshimiwa Asenga, jiandae, Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Jesca, jiandae na Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru wewe mwenyewe kwa uendeshaji bora kabisa wa Bunge letu, umekuwa mhimili mkubwa wa kumsaidia Mheshimiwa Spika na kwa kweli ukikaa hapo Wabunge wengi tunakuwa na morali ya kuchangia. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza kocha, kocha wa timu hii, kocha wa Taifa letu, kocha aliyetengeneza Baraza bora kabisa la Mawaziri, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukiitazama *cabinet* ilivyoundwa, kama ni mtaalam wa kutazama utagundua kwamba Mheshimiwa Rais kuna kitu anataka kutoka kwenye Baraza hili. Kuna Mawaziri wenye umri mkubwa kama Mzee wetu hapa, Mzee George. Katikati hapo amechanganya Mawaziri wa umri wa kati kina Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mheshimiwa Pinda, Mheshimiwa George Simbachawene, lakini akaja akachanganya kundi kubwa la vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimtazama Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, wenzake hao wote hao kina Mheshimiwa Deo, Mheshimiwa Mavunde, Rais anataka *speed* ya ufanyaji kazi. Pamoja na akina Mheshimiwa Mchengerwa mtu kazi, Rais anataka *speed* ya namna ya kutatua kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona namna ambavyo Mheshimiwa Rais anataka. Katika Baraza la Mawaziri umri wa kati upo, umri mkubwa upo. Nimemwona Profesa alikuwa anatabasamu na yeye ninamweka kwenye kundi la umri wa kati, Profesa Waziri wa Elimu namweka kwenye kundi la umri wa kati. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi yuko kwenye kundi la vijana pamoja na akina Mheshimiwa Ridhiwani. Mheshimiwa Rais anataka wafanye kazi na wanafanya, kinachotakiwa hapo ni *speed*. Waongeze *speed* ya kutatua kero za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu *Engineer* Sanga, Kamishna wa Ardhi Methew, tunaona timu nzima ya Wizara yake namna ambavyo inachapa kazi usiku na mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro mikubwa ya ardhi, imeanza kutatuliwa wakati wa Mzee Lukuvi, lakini sasa hivi tunaona utatuzi wake namna ambavyo unakwenda kwa *speed* sana. Katika kutoa haki za watu Mheshimiwa Waziri aendelee na roho hiyo na sura ya ubandidu. Kuna baadhi ya watu ni dhulumati, wanadhulumu watu wa chini. Waendelee kusimamia haki za watu bila kujali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanamtumia *message* wanamtisha, wamepita Mawaziri wengi, sawa utapita, lakini achape kazi aache alama, aache alama! Suala la muda wa kukaa siyo la kwake ni suala la Mheshimiwa Rais, ataamua mwenyewe, lakini wakati huu anaaminiwa na Mheshimiwa Rais, wakati huu Watanzania tunamwombea, apige kazi, asaidie watu kwa haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro baadhi ya maeneo. Kwa mfano, hata kwenye Jimbo letu kwenye Wilaya yake ya Chamwino, kuna mgogoro kati ya mpaka wa Mpwapwa na Chamwino, aende akautatue ule. Pia kuna tatizo vilevile la upimaji na kutambua maeneo. Ninataka wajikite kwenye kupima maeneo ya vijijini na kuyatambua, kutenga maeneo ya wafugaji. Hapo kuna tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua utafiti lazima ufanyike wa kutosha. Kuna baadhi ya wafugaji kwenye maeneo yao hekari chache anaweza kulisha mifugo. Kuna baadhi ya wafugaji maeneo yao ni makame, lazima apate eneo kubwa zaidi ili aweze kulisha mifugo yake. Pia kuna baadhi ya wafugaji wanapewa ardhi ambayo haiwezi kuotesha majani ya kutosha, sasa unaenda kumweka kwenye eneo gumu, eneo la miamba, mfugaji atapataje kulisha mifugo yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vema tukayatambua maeneo tukayapanga, halafu yakaheshimiwa. Maana kupanga jambo lingine, lakini kuyaheshimu ni jambo lingine. Kwa hiyo, ni muhimu sana hii *Commission* inayotaka kuundwa ikatazama maeneo hayo. Hawa wafugaji tunawahamisha kila siku hamia huku, hamia huku, hamia huku, wanakuwa kama siyo Watanzania, kitu ambacho siyo sawa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri hii *Commission* iwahishwe iwekewe sheria, isimamie na haki za walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikutolee mfano, nilikuwa napanga mimi mwenyewe, nilikuwa mpangaji na nilikuwa mlinzi usiku. Ikatokea siku moja mke wangu amejifungua watoto mapacha nimecheleweshа kodi, unajua mwenye nyumba alichofanya? Alileta fundi akaja kung'oa bati. Eeh! akang'oa bati za nyumba yake. Kwa hiyo, Mama Neema ananiuliza vipi? Nikamwambia aah! wewe tulia, tulia tu hamna namna tutafanya, halafu usiku mvua ikanyesha. Kama alikuwa ametumwa yule bwana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaposema *Commission* iundwe, iundwe kusimamia haki za walaji. Kwa sababu sisi wenyewe tumepitia mengi. Kuna baadhi ya wenye nyumba wanaonewa na wapangaji, kuna baadhi ya wapangaji wanaonewa na wenye nyumba. Kwa hiyo, ukiweka *Commission* na sheria nzuri maana yake italinda hata haki za walaji. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa wazo hili, lakini tunaomba *speed* na ubora, ije hiyo sheria Waheshimiwa Wabunge waichambue ili iweze kufanya kazi yake kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uundwaji wa hii *Commission* kusimamia *Real Estate*, hapa pamekuwa na matapeli wengi sana. Ni muhimu sana, kuna baadhi ya watu wanapelekana Mahakamani ardhi siyo yao, yaani wote anayemshtaki mwenzake anajua ardhi siyo yake, anayeshtakiwa anajua ardhi siyo yake. Hukumu ikipatikana wanaitumia ile hukumu kuuza ardhi ya mtu mwingine kabisa, halafu wanagawana kati ya aliyeshinda na aliyeshindwa! Sasa huu ni

utapeli wa kiwango cha juu sana. Kwa hiyo, tunamwomba sana Waziri hili jambo lisimamiwe kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwenye kutetea haki za watu ninarudia tena, hapa tusifanye mzaha. Kwenye sekta miliki hapa tuwamilikishe watu. Lakini hili jambo Mheshimiwa Rais aligusa hivi juzi akaanza kupima ardhi vijijini, ameona namna watu walivyochangamkia ile fursa. Tunaomba tupime mashamba ya watu, watu wapimiwe nyumba zao na tuanze kupanga miji yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Dodoma kadri inavyokua Mji unatakiwa uhamie Mvumi. Mji uhamie kwenye *centre* kubwa kubwa kama Dabalo kule kwa Waziri.  Kama maeneo makubwa ya Itiso, Mpwayungu, Manda na Mlowa barabarani. Maeneo yale yakipimwa yakapangwa vizuri, Haneti pale, ile ni Miji Midogo itakayosababisha Dodoma ipumue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe tuna *state* za pembeni ambazo zimepangwa vizuri, mtu anafanya kazi mjini anaenda kuishi nje kidogo ya mji. Sasa hivi kuna usafiri wa treni ya umeme, watu wanaweza kuwahi kwenda makazini kwa wakati wowote.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, lakini tunaomba na Wizara ya Fedha itoe fedha za kutosha kwenye taasisi za Wizara ya Ardhi ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi, kwa sababu kama hawana pesa, nao vilevile uwezo wa kufanya kazi watakuwa hawana. Kupima nchi yote siyo jambo dogo, wanaweza wakatumia hata wapima binafsi ili waweze kusaidia baadhi ya maeneo kuweza kunyoosha mambo yaweze kwenda vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, Mungu ambariki sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, wajiandae Mheshimiwa Mtemvu na Mheshimiwa Jesca.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia Wizara yetu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nami naanza kwa kuunga mkono hoja mapema kabisa, hoja ya Wizara ya Wizara ya Ardhi, ambayo inaomba takribani shilingi bilioni 164.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema Wabunge wenzangu, ninaanza hapa kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watumishi wote wa Wizara yako, Katibu Mkuu *Eng*. Sanga, Kamishna Methew, Makamishna wote na Watumishi wote wa Idara ya Ardhi na hasa katika Mkoa wetu wa Morogoro na Halmashauri yetu ya Mji wa Ifakara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaombea Mungu awasaidie, maana yake Wizara ya Ardhi na mambo ya ardhi kwa kweli ni changamoto kubwa sana sana. Tunawaombea sana Mungu na hata hapa Dodoma tunaona namna ambavyo mnavyoita majukwaa na mnaleta ma-*tent* yale ya kutatua kero kama hapa Bungeni, tunawapongeza sana, tunawashukuru sana, jambo hili liendelee na limesaidia wananchi wengi sana kwa utatuzi wa kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Morogoro pale tunamshukuru sana Kamishna Frank aliondoka pale na sasa hivi wametuletea Kamishna Kayela, ameanza kufanya kazi vizuri. Hata katika Halmashauri yangu ya Mji wa Ifakara wametuletea Mkuu wa Idara ya Ardhi mpya anaitwa Rajabu Bogwa. ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, nimesikia huyu amefika ana wiki tu anataka kuondoka. Ifakara ina changamoto kubwa za ardhi sana, tunaomba Rajabu abaki Ifakara Halmashauri ya Mji ili aendelee kutatua changamoto kubwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi kama nilivyosema inahitaji kuwaombea Mungu viongozi wetu hawa kwa sababu hata hapa Dodoma ukiangalia sasa hivi wamemleta Kamishna mpya anaitwa Godfrey Mwamsojo, ninamwona anavyokaa pale, nami nilikuwa na migogoro yangu nimeenda pale unaona kabisa mpaka mvi zake zimeanza kuwa za *brown*. Anasikiliza mgogoro mpaka anasinzia, mgogoro unaenda mbele

unarudi nyuma, unazunguka unaanzia mwanzo ulipoanzia, kwa hiyo, kwa kweli tunawaombea Mungu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaona Kamishna Mwamsojo amekaa hivi, unaona mpaka anasinzia namna hii, maana yake mgogoro mwingine unasikilizwa unaenda huku unarudi huku, unarudi huku unaenda huku. Kwa hiyo, hii maana yake narudi pale kwenye hoja ya msingi, Mheshimiwa Waziri ambayo amesema hapa, hii *Land Commission* wakiianzisha itatusaidia kupunguza mambo haya. Wakienda kwenye mambo ya kidigitali watatusaidia kukamilisha mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwambia mimi kwenye Jimbo langu na Halmashauri yangu nilipata ule mpango wa Hati za Kimila, katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Wilaya ya Kilombero. Katika vitu ambavyo vimepunguza migogoro kwa asilimia kubwa ni utoaji wa Hati zile za Kimila, ule mpango kwa sasa haupo kwa sababu sisi ni Halmashauri ya Mji, lakini wananchi kwenye mashamba yao wameenda wamepimiwa mashamba, wamepimiwa nyumba zao wamepimiwa makazi yao, wana hati. Changamoto ikawa kwenye uuzaji tu, lakini kwa kweli kila mtu ana kipande chake cha Hati ya Kimila, kimesaidia sana kupunguza kero kwa kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *Land Commission* hii ikienda ki-*digitalized* ikiwa na vifaa vya kisasa, lazima mu-*invest* katika vifaa vya kisasa, *mobile track* na kadhalika ili muweze kutatua kero kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hapa Mheshimiwa Waziri ni taasisi nyingine wanazoshirikiana nazo. Kwa mfano, nimejifunza Wizara ya Ardhi wanatakiwa washirikiane karibu sana na TAKUKURU, kwa sababu ninyi hawana wataalam wa kujua mikataba *fake*, kujua hati *fake*, kujua watu waliouziana, nani *original* nani siyo *original*. Sasa ni vizuri pia waka-*push* kule upande wa TAKUKURU, wakawawezeshwa vifaa, wakawezeshwa bajeti, wakawezeshwa pesa ili jambo la ardhi linapoenda TAKUKURU lirudi kwa wakati na wananchi waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu Mheshimiwa Waziri amesema atafanya ziara Mkoa wa Morogoro, utatusaidia kutatua migogoro ambayo ipo baina ya mipaka, kwa mfano kule Sanje, Ituli na Kidatu. Nami nimechangia hapa leo Mheshimiwa Waziri kukushukuru wewe, Mheshimiwa Rais alikuja tarehe 4 Agosti, 2024, tulizungumza kuhusu mgogoro wa Ifakara Mjini pale, Kata ya Mrabani, mbele ya Mheshimiwa Rais na Baba Askofu alikuwepo pale, kuna mgogoro mkubwa wa miaka mingi ya historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo Mheshimiwa Waziri akabaki pale akakutana na Baba Askofu, leo ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri ameniambia hapa na Katibu Mkuu amenihakikishia, ziliombwa kama milioni 400 kasoro, wameshaweka shilingi milioni 150 za kukagua mgogoro huo. Hii inathibitisha Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inasikiliza na inafanyia kazi yale ambayo Wabunge tunayasema na Wabunge tunayaombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, kama hizo milioni 150 zimewekwa kwenye bajeti zipatikane kwa wakati kupitia Wizara ya Fedha, ziende kwa wataalam wetu wa ardhi wakapime Kata ya Mrabani. Wananchi wale wakishaona hati zao zipo wako tayari kuchangia ili kumaliza mgogoro huu mkubwa sana katika Halmashauri yetu ya Mji wa Ifakara, ni jambo kubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo kubwa pale la Kanisa limevamiwa na wananchi, wananchi wameshajenga makazi yao ya kudumu, kwa hiyo, wananchi wale wakipimiwa wakimilikishwa fedha zile zitapatikana kwa ajili ya kwenda kumtafutia Baba Askofu eneo lake lingine na hii amekuwa akiifuatilia kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri ninaomba sana hizi fedha ziende kwa wakati ili tuweze kumaliza mgogoro huu, nilimpigia hata juzi nikiwa pale na Mtendaji wa Kata na akaniahidi kwamba analifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuzungumzia kuhusu Shirika letu la Nyumba kidogo, ninaomba kutoa ushauri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri hapa kwamba ni

muhimu sana pia wakajielekeza katika Halmashauri za Mji zinazoendelea na zinazokua kwa kasi kama Halmashauri ya Mji wa Ifakara. Ina mipango pale ina ramani imepanga, Makao Makuu ya wilaya, kila kitu kimepangwa pale, lakini ni vizuri wakaanza kuweka bajeti sasa ya kujenga nyumba nafuu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani sisi kule tunachoma tofali kwa udongo, tofali jekundu, tunajenga kwa tope na wataalam wanakwambia kwa sababu kule kuna maji basi ukijenga kwa tope na zile tofali nyekundu nyumba inadumu zaidi kuliko kujenga kwa simenti. Wakituletea wataalam wa ardhi, wataalam wa nyumba wakaja wakafanya *study* ya kisayansi inawezekana wakapata nyumba rahisi zaidi za kujenga kwa wananchi wetu kuliko kutumia gharama nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tofali inachomwa, udongo unachomwa uleule, shimo la choo ndiyo linatoa udongo, tofali inachomwa inakuwa nyekundu inajengwa kwa tope. Mtu anapandisha mpaka juu, anakazia kasimenti kidogo anapaua. Kwa hiyo, ni mfumo wa nyumba ambao unaweza kusaidia sana Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kusimama hapa kwa unyenyekevu mkubwa. Niliomba dakika hizi chache za kushukuru Wizara hii kwa kumaliza mgogoro wa Mlabani na kuanza kutenga fedha kwenda kumaliza mgogoro wangu wa Ifakara Mjini wa kanisa na wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, wajiandae Mheshimiwa Jesca na Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana kwenye nchi yetu. Kwanza, nitumie nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli kwa jinsi ambavyo katika kila sekta muhimu kwenye nchi yetu ameweza kuigusa na kuitolea maelekezo muhimu ambapo Waheshimiwa Mawaziri hawa (Makamisaa) wetu wameweza kutafsiri maono hayo katika hali ambayo inafaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitoe pongezi sana kwa Wizara. Ndugu yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi kwa kazi anayoifanya pamoja na Naibu Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Pinda pamoja na wataalam wetu ambao wanawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitambue sana uwezo mkubwa wa Mhandisi Antony Sanga pamoja na Naibu Katibu Mkuu, dada yangu Lucy wakisaidiwa na mbobezi sana kwenye Wizara hii, Kamishna wetu Mathew na wataalam wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara kwa kiasi kikubwa ninaifahamu vizuri, lakini hakuna mwaka nimeacha kuichangia na leo nimepata bahati sana kuwaona wachangiaji; ni wale ambao mara nyingi wanachangia kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia pia jinsi gani wanachangia na nimeona ni sehemu kubwa wanakubaliana na ushauri ambao tumewahi kuutoa zaidi ya miaka minne humu, mambo mengi yamekwenda vizuri. Kwa hiyo, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wa kisekta ambao wamewahi kupita hapo, lakini leo mwisho sana jinsi gani Ndugu yangu Ndejembi ameendelea kubeba maono yote na ushauri wote wa Waheshimiwa Wabunge kwenye Bunge hili katika nyakati zote zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatamani kujielekeza katika maeneo machache ambayo na wengine wameyasema, lakini pia yamesemwa kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwenye Hotuba yake ya Bajeti, hasa katika eneo la urasimishaji na migogoro. Pia, jambo lingine dogo sana ni kumalizia hili ambalo limezungumzwa kwenye *page* ya 45 kuhusu upimaji wa viwanja na mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye urasimishaji miaka minne sasa ninasema humu, lakini leo nitoe pongezi sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya maboresho makubwa ya kuona jinsi gani changamoto ya urasimishaji mijini ambayo inaenda sambamba na ile ya huko kwenye nje ya miji kwenye halmashauri zetu ya (KKK).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu huku ni urasimishaji tu. Lugha yetu ni ndogo tu (urasimishaji) lakini ni ukweli katika miji mikubwa kama Dar es Salaam na majiji, hili eneo lilikuwa ni changamoto sana katika muda mrefu. Tunakubali tulianza zaidi ya miaka 10 nyuma kuwa na jambo hili la urasimishaji, lakini katika maeneo ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam katika Wilaya kama ya Ubungo ilikuwa ina changamoto kubwa katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Wizara kwa kuja na mipango kadhaa, lakini kubwa ambalo limetuvusha zaidi ya 50% kwa sasa ni hili la *clinic* ya ardhi. Ninawapongeza, ninawapongeza sana. Ni ukweli imeenda kutupa majibu kwamba changamoto hii siyo tu ya eneo moja kwamba ya Mamlaka ya Upimaji ambayo ni halmashauri zetu, lakini msimamizi wa sera ambayo ni Wizara yetu, mwenye jukumu la kutoa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja kugundua hata wananchi tunaowaongoza pia ni changamoto kwenye sababu ya wao kutopata hati na kufikia yale malengo ya Mheshimiwa Rais kuona kila mwananchi anajiinua kiuchumi kwa kupata hati ambayo inaweza ikamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili limeenda vizuri. *Clinic* za ardhi zimetusaidia. Wale ambao hawana migogoro kwa maana hawajavamia mashamba na hawajavamia maeneo ya watu, hao wanaweza kupata hati vizuri tu kwa sababu michoro itakamilika, lakini mwisho wa siku watalipia ankara zile ambazo wamehitajika kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumebaki na wale ambao wamevamia maeneo ya watu. Wale watu bado wanamiliki hati zao. Watu hao inawezekana wapo ndani ya nchi au nje ya nchi,

lakini unakuta wananchi wameingia, wamekuta mapori makubwa yamekaa muda mrefu, lakini wameyaingilia. Hao ni kweli wanaweza kuikosa hati lakini, mwisho wa siku wanaikosa hati kwa nini? Wanaikosa hati kwa sababu yule mwenye hati amekataa kuirudisha, ku-*surrender* hati husika. Kwa hiyo, hata mchoro pia hauwezi kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza kumwona mwananchi huyu bado ana changamoto, lakini Wizara imeenda vizuri. Imetushauri tukatengeneze timu za kwenda kupiga magoti kwa wahusika waweze ku-*surrender* hati zile kwenye ardhi au na mashamba yao makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia ameenda mbali amesamehe kodi zote ambazo hazijalipiwa katika mashamba ya muda mrefu ili watu hawa wamiliki wapate nafuu ya ku-*surrender* kwa sababu sina gharama nyingine ili wananchi wale waliovamia waweze kuingia na kuweza kukubaliana waweze kupata hati. Hii ninawapongeza sana Serikali, haya ni maono makubwa ya kuwasaidia Watanzania waweze kupata hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli sasa tunavyokwenda hata kule kwangu Wilaya ya Ubungo, Jimbo la Kibamba tunakwenda sasa zaidi ya 50% tunakiri sasa tunaweza tukapata hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa wananchi wenzangu na ninaowaongoza; waende wakatembelee Ofisi za Ardhi watakuta kuna majalada yao yamekamilika wanahitajika wakalipie ankara au *bill* ili waweze kupata hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli, hakuna mtu wa kukudanganya eti anaweza kufuatilia hati yako. Hati ni kama *cheque*. Ni lazima ni wewe mwenyewe unahusika kuifuatilia na ulipie mwenyewe na mwisho wa siku uipate...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu, malizia.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la migogoro. Hata hapa nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Serikali. Mheshimiwa Ndejembi wewe ni mtu anayesikia sana. Leo mdogo wangu Kunambi amesema, (mimi sijawahi kumsikia Kunambi akisifia sana) lakini leo nimemsikia kwa mara ya kwanza akimtakia na uchaguzi ujao ashinde pale Chamwino na pia Mheshimiwa Rais amkumbuke kwenye nafasi hiyo ili aendelee kutuvusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na Mheshimiwa Kunambi, mdogo wangu Mwanamorogoro katika hili, tunakuombea wewe kila la heri. Ukweli kwenye migogoro tumekuwa na migogoro mingi sana na mimi kwenye Wilaya ya Ubungo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu, mengine andika. Ahsante. Mheshimiwa Jesca.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, lakini na kuwatakia kila la heri watumishi wote na Wizara hii. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca. Mheshimiwa Jesca yupo?

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuendelea niwatambue wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni wawili wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Ndugu Charles Saguda, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro na Ndugu Linda Salekwa, Mkuu wa Wilaya ya Mufindi. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ndejembi; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitendo na Maafisa kutoka Wizarani; Wadau wa Sekta ya Ardhi; Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa na Wasajili Wasaidizi; Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Chamwino; Sekretarieti ya Wilaya ya Chamwino; na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Chamwino. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe; Viongozi wa CCM wa Kata Tisa kutoka Jimbo la Kavuu; Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mlele; Waheshimiwa Madiwani wa Kata tisa kutoka Jimbo la Kavuu; Makatibu Tarafa Mpimbwe na Mamba Jimbo la Kavuu; Wadau wa Maendeleo Jimbo la Kavuu; Watendaji wa Kata zote Jimbo la Kavuu; na Watumishi wa Chuo Kikuu cha Kilimo *(SUA)*. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 25 wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Stergomena Tax, Waziri wa Ulinzi ambao ni Kikundi cha Mama Kijani Tawi la Mwanza. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani; Wanachama wa CCM kutoka Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Anatropia Theonest; Ndugu Kaney Angelo, mtoto wake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Walimu nane na wanafunzi 50 kutoka Shule ya Msingi Shree Hindu Mandal ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Nitatambua umashuhuri wake wa kufanya kazi Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pale ambapo watatatua mgogoro kati ya wananchi wa majimbo mawili; Jimbo la Kawe katika Mitaa ya Madale, Mbopo, Mabwepande na Jimbo la Kibamba pale kwa ndugu yangu Mtemvu, Mitaa ya Tegeta A, Msumi A, Msumi B na Kulangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa huu mgogoro, yeye ni Mheshimiwa Waziri wa tatu. Nilianza kueleza hapa Bungeni wakati Mheshimiwa Waziri akiwa Mheshimiwa Dkt. Mabula akashindwa kutatua. Nikaeleza Mheshimiwa Waziri alipokuwa Jerry Silaa, akakwama kutatua na sasa ni Mheshimiwa Waziri wa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sifa anazopewa Mheshimiwa Ndejembi, ninaomba basi sifa hizo wananchi hawa zaidi ya 250,000 ambao wanaathirika kwa maeneo yao yaliyochukuliwa na *DDC* mwaka 1980 kwa kutokufuata utaratibu kwa sababu Serikali ya Kijiji haikushirikishwa, wala haikutoa baraka. Wakaenda kupata hati mezani, hati ilikuwa inawataka kwa maelezo yao wafanye kilimo na ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 50 baadaye, hawajawahi kufuga kuku wala hawajawahi kulima bustani ya mchicha. Wameenda kutaka kuwaondoa wakazi wa asili na ambao wakazi wa asili kwa sheria za ardhi za kipindi kile, walikuwa wana umiliki halali na wao wameuzia wananchi wengine. Kwa hiyo, tunavyozungumza, watu 250,000 tunazungumza raia ambao walikuwepo kipindi kile kama wananchi ama wakazi wa asili na wananchi wengine waliokuja kununua maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana, nimesoma hotuba yake anasema kwenye mwaka huu wa fedha 2025/2026 wanataka kutatua migogoro 3,000. Ninaomba kwa hisani kabisa, eneo hili ama mitaa hii saba niliyomtajia ambayo inaingia kwenye Jimbo la Kawe na Jimbo la Kibamba akatafute ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali za wananchi ni ngumu tunavyozungumza. Ni bahati mbaya viongozi waliopewa dhamana kwenda kuhudumia wananchi, kwenda kuwasikiliza wananchi, kwenda kutatua migogoro kwa busara wamekuwa hawatumii hiyo busara. Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam, Jeshi la Polisi na mitutu ya bunduki linawasumbua raia wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina matangazo mawili. Hili jambo lingeshughulikiwa na Mheshimiwa Dkt. Mabula, hili jambo lingeshughulikiwa na Mheshimiwa Jerry Silaa, haya matangazo mawili yasingetokea. Kuna tangazo la tarehe 10 Februari, 2024 limesainiwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni anasema anaenda kuuza viwanja vya halmashauri Mabwepande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangazo la pili, tarehe 9 Mei, 2025, limesainiwa na Shedrack Maxmillian, anaenda kuuza maeneo na mbaya zaidi, watu wamejenga nyumba zao, watu wana viwanja vyao, viwanja vyenye nyumba na viwanja ambavyo havina nyumba vinauzwa wakati wananchi wapo ndani ya ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni nchi huru. Ardhi ya Tanzania ni mali ya Watanzania. Mheshimiwa Rais amepewa dhamana, tunaomba asaidie kumaliza huu mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ...

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, anayezungumza anazungumza nusu vizuri, nusu haijakaa vizuri na kwa sababu kanishirikisha, ninayo nafasi ya kumpa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi kwenda na huu mgogoro kwa hatua na hatua ya kwanza waliyofanya chini ya Mkoa wa Dar es Salaam maeneo ambayo hayajavamiwa tayari... *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, si ungechangia, acha kunipotezea muda.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo hayajavamiwa katika eneo hilo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imetangaza wananchi waombe, wapewe, lakini maeneo ambayo yamevamiwa Serikali imetoa maelekezo. Tayari

wananchi walipie *per square meter* shilingi 3,000 badala ya yale ambayo hayajavamiwa *square meter* ni shilingi 15,000. Unaweza kuona tofauti hapa Serikali iliyofanya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante. Waheshimiwa tunaendesha Bunge kwa kanuni. Taarifa ni sehemu ya haki ya Mbunge ndani ya Bunge. Msemaji anayepewa taarifa jibu lake ni moja tu, kukubali taarifa au kuikataa anaendelea na shughuli zake. *(Makofi)*

Haina haja ya kutupiana maneno, haina haja ya kugombana, wala haina haja ya jambo lolote; ndiyo kanuni zinavyosema. Mheshimiwa Halima, wewe ni mwanasheria na hizi kanuni tumetunga pamoja; endelea. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei taarifa na ninamshauri Mbunge...

**NAIBU SPIKA:** Ahhaa, acha acha. Hupokei taarifa, endelea na mchango wako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei taarifa, ushauri wangu ni kwamba akasome nyaraka zote za historia ya mgogoro huu, aende shule akajifunze. Mimi ni Mbunge wa mwaka wa 20 sasa, siwezi kusimama bila kuwa na nyaraka ya kuonesha historia ya huu mgogoro ulitoka wapi mpaka tumefika wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu unahusisha maeneo ambayo yana shule zaidi ya 15, yana vituo vya mafunzo vya Serikali, kuna zahanati zaidi ya tatu, kuna viwanda zaidi ya vitano, kuna taasisi za kidini zaidi ya sita, kuna makanisa, kuna ofisi za Serikali, kuna maeneo ya uwekezaji, kuna maeneo ya maziko na kuna vituo vya kulelea watoto yatima. Kwenye eneo ambalo linahusu ekari zaidi ya 5,000; kwa hiyo, nimalizie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wananchi walikuja wakamwona Mheshimiwa Waziri pale Wizarani, amewaahidi wananchi ataenda kwenye maeneo husika kati ya tarehe 2 mpaka tarehe 7 mwezi Juni. Wananchi wameshajitangazia huko

kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi anaenda kuwatembelea. Ninaomba ahadi yake itimie, akatatue mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine, ushauri wa bure kabisa, Mheshimiwa Waziri aende kusikiliza pande zote. Watu ambao wanashiriki kukandamiza wananchi sasa hivi wakijua ana ziara watamuwahi wampotoshe. Mheshimiwa Waziri asikilize upande wa Serikali, asikilize upande wa wananchi upate ukweli, haki itendeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho; tunalalamika hapa na ninaomba Mheshimiwa Waziri atujibu. Tarehe 2 Februari, 2022 Benki ya Dunia iliingia mkataba na Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele yako ya pili ilishapigwa. Mengine mwandikie Waziri na ndiyo utaratibu wa Bunge. Hata mpira ukifika dakika 90 kama umefungwa moja hujarudisha ndiyo basi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninashukuru kwa kunipa nafasi, nilipata udhuru kidogo. Mengine nimeyaweka kwa maandishi, lakini nitakuwa na machache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini ombi langu la kwanza Mheshimiwa Waziri ni *NHC*. Kuna utaratibu umekuja sasa hivi kwamba, mna-*charge key deposit;* sasa unakuta mna wapangaji, wale ambao walishapanga muda mrefu, halafu mmewaletea *demand* walipie *key deposit,* mtu ameshakaa miaka minne, mitano, unamdai sasa hivi alipe *key deposit!* Wakati ile *key deposit* ilikuwa ni kodi ya mwanzo kabla hajaingia, unam-*charge* miezi mitatu, analipa, *then* analipa kodi yake anaendelea. Sasa ni kinyume cha utaratibu na wananchi wanalalamika, tunaomba Mheshimiwa Waziri hilo akalifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, amesema hapa, tuwe na *affordable houses*. Tunaomba kabisa Mheshimiwa Waziri hizi nyumba za *National Housing* kodi zao wasizingatie tu *market*, turudi kule tulipoanzisha shirika tulikuwa na nia gani. Waangalie na jinsi uchumi wa nchi unavyokwenda bila kuangalia tu *market* ya eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri katika kupanga hii miji watusaidie, wasipange miji kwa vipandevipande, kila watu kwenye mamlaka yao waupange mji mzima. Kwa mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa wawe na *masterplan* ya halmashauri yote, wasianze kata hii kata hii; wanapoanza kata hii, kule kata nyingine kumevamiwa. Kwa hiyo, tunaomba kila sehemu yenu ya Idara ya Ardhi, kwenye eneo lao la utawala, wawe na *masterplan* ya eneo lote, ili kuzuia kule mbele kusivamiwe. Wakiweza warejee ile Sheria ya Vijiji vya Ujamaa tulivyokuwa tunafanya sogeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ilikuwa ni kusogeza huduma karibu na wananchi, kuwaweka wananchi pamoja, iwe rahisi kuwahudumia. Leo hii tunalazimika kupeleka umeme sehemu nyingine kwa gharama kubwa kwa sababu tu, hatuku-*plan* ule mji watu wakakae kule. Wakishafika kule watakudai maji, watakudai umeme, watakudai barabara, bajeti ya jimbo zima unakuta inaelekea kwenye kijiji kimoja ambacho watu walienda kuishi mashambani. Sasa watusaidie kupanga hii miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la Dodoma, ni fahari ya Watanzania. Dodoma ni fahari ya Watanzania, lakini siyo fahari ya migogoro ya ardhi kwa Watanzania. Hakuna Jiji lina migogoro ya ardhi kama hili la Dodoma. Ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi, sijui watafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wanadhani kwamba, imeshindikana kwa utaratibu wa kawaida wa ardhi, basi iundwe tume kama, zile za akina Keenja, kama inashindikana basi hizo kamisheni watengeneze. Kwa kweli, watu wa Dodoma wamekuwa *loyal* kwa Serikali hii na Serikali zote za Chama Cha

Mapinduzi, lakini namna ambavyo tunabanana nao, kila siku wanaandamana kwenye Ofisi za Mipango Miji, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wanalalamika. Unakuta akinamama wanalia mle. Mimi mwenyewe, Mbunge, nimefanyiwa *double allocation* Dodoma, wapo wengi tu humu. Walikuja wakatuuzia viwanja kwenye kliniki, kumbe viwanja hewa! Tumepata *double allocation*, kila siku tunapanga foleni, huu ni mwaka wa tano tunakwenda kumaliza Ubunge hatujawahi kupewa viwanja vyetu. Sasa hawa Watanzania wengine na hii fahari yetu iko wapi, Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba iwe fahari yetu, lakini tusinune. Tuujenge mji kwa haraka. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninataka nimpe Taarifa dada yangu, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kwa mchango wake mzuri anaochangia kwamba, ni kweli kabisa kumekuwa na ukiritimba kwenye Ofisi za Ardhi. Mimi mwenyewe hapa nina zaidi ya miezi nane ninasubiri *control number*, ninaambiwa mtandao haufanyi kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kaa inatosha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Inatosha. Mheshimiwa Jesca, Taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokea Taarifa yake na ninaomba sana, tunataka Dodoma iendelee kuwa fahari yetu, lakini wapunguze migogoro ya ardhi,

Wanadodoma wasione kama sisi wageni tumekuja kuwapora. Sisi wageni watukaribishe kwa wema, watupatie viwanja. Kliniki tunaingia na magonjwa, tunatoka na magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne ya kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu, hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii, kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa ni pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia, kutumia fursa hii kumpongeza wewe binafsi, Spika na pia, uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa, *National Competitiveness.* Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Katika kipindi chake akiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kusababisha Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa kwa kuanzisha mikopo inayotolewa, kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha (KKK) ardhi. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni mnufaika wa programu hii na imekopeshwa shilingi 1,857,586,634. Mji Mdogo wa Mbalizi umepimwa viwanja 35,000 kwa gharama ya shilingi 1,273,038,500 na Kijiji cha Mwashoma, Kitongoji cha Inolo, vimepimwa viwanja 565 kwa gharama ya shilingi 584,548,134 na umefanyika kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa na faida itayopatikana kwenye mauzo ya viwanja hivi ipangiwe matumizi yanayolenga kuendeleza ardhi, ikiwemo kuweka miundombinu kwenye maeneo yanayopimwa. Kutokana na mafanikio katika utekelezaji huu wa mwanzo, ninapendekeza Serikali iweke kipaumbele cha kuendeleza programu katika maeneo mengine, hususani yanayolizunguka Jiji la Mbeya, kutokana na mahitaji makubwa ya makazi yaliyopimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza Serikali iendeleze programu hii katika Vijiji vya Swaya, Lupeta, Nsenga, Ifiga,

Nsongwi Mantanji, Nsongwi Juu, Izumbwe, Iwindi, Igoma, Ilembo, Idimi na Haporoto. Upimaji kwenye vijiji ambavyo vinakua haraka kuwa miji, *growing towns,* utawezesha kupunguza na hata kuondoa kabisa makazi holela na pia, kuongeza wigo wa walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na programu ya makazi, Serikali iweke usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo, ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya makazi. Katika kupanga matumizi mazuri ya ardhi, ihusishe Wizara za Kilimo, Wizara za Maji na Wizara inayosimamia mazingira. Kwa vile binadamu tunaongezeka ni muhimu kuhakikisha ulinzi kwa kuhifadhi ardhi inayofaa kwa kilimo na pia, kutenga ardhi, kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza hatua zinazochukuliwa na Serikali kurejesha mahusiano mazuri kati ya *TANAPA,* Hifadhi ya Kitulo na Wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma, Ulenje na Inyala; bado hakuna Suluhu, haijapatikana. Serikali ichukue hatua pia, za kumaliza mgogoro wa miaka mingi wa mpaka kati ya *TFS* na wananchi wa Kijiji cha Mwashoma. Wananchi wa Wilaya ya Mbeya wamekuwa walinzi wazuri wa hifadhi zetu na ni jukumu la Serikali kuhakikisha uendelevu huu na kuondoa migogoro ambayo haina maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua fursa kuwapongeza Wizara kwa mambo mengi mazuri waliyofanya. Hata hivyo, ninaomba mambo haya yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni suala la *NHC* kudai *key deposit* kwa wapangaji wa zamani sasa, kwa *rate* ya sasa na siyo ya upangaji wao walipoingia, siyo sawa kisheria. Jambo hili linaleta malalamiko mengi kwa wapangaji ambao ni wananchi. Utaratibu kwa mujibu wa mikataba yao unahitaji watoe *key deposit* kabla ya kuingia katika nyumba hizo na inatakiwa itozwe kwa wapangaji wapya. Sasa hii ya kuwatoza wapangaji wa

zamani kwa uzembe uliofanywa na shirika lenyewe kutodai au kupoteza kumbukumbu za wateja, sio sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa usumbufu wa migogoro isiyokuwa ya lazima kwa kushtakiwa na wapangaji na kuliingizia shirika hasara zisizo za msingi, basi utaratibu ufuatwe kwa wapangaji wapya na wale wa zamani watozwe kwa kodi waliyoingilia kwenye majengo hayo, iwapo watajiridhisha kuwa haikutolewa. Siyo kwamba, hawaoni kumbukumbu yoyote au wawaache, ila warekebishe kwa wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *issue* ni hoja ya *CAG,* wamwambie kwa sasa wamerekebisha, ndiyo maana amewekwa Mkurugenzi mpya, ili arekebishe. Siyo tena kuharibu zaidi kwa kukiuka taratibu na kuleta migogoro isiyo ya lazima. Mimi pia, ni mpangaji humo, nina uhakika na ninachokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili. Upandishaji wa kodi uzingatie pia, ukuaji wa uchumi wa Taifa, ili kuendelea kuzingatia hasa lengo la uanzishaji wa Shirika la *NHC*. Siyo kushindana kwenye soko tu, bali kusaidia kupatikana kwa makazi ya bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, utatuzi wa migogoro ya ardhi. Tunaomba sana utaratibu madhubuti wa kutatua migogoro ya ardhi, uwekewe mpango mahususi wa kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kipekee katika Mkoa wa Dodoma, tunaomba migogoro itatuliwe, ili iwe kweli, fahari ya Watanzania kwa kujengwa kwake kwa wakati. Tunadai viwanja vilivyofanyiwa *double allocation* kwa zaidi ya miaka mitano sasa na wengine zaidi ya hapo, sasa hii siyo sawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri sasa; kama Wizara wameshindwa kutatua migogoro ya ardhi Dodoma, basi iundwe tume maalum ishughulikie suala hilo, kama ilivyokuwa Tume ya Jiji au Tume ya Keenja, maana kliniki zimekuwa nyingi, lakini matatizo hayaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne; Mipango Miji waandae mipango miji kwa eneo lao lote la utawala, siyo kwa vipande vipande. Hii inasababisha ujenzi holela katika miji. Kwa kuwa, wanaanza kupanga huku, upande mwingine unavamiwa. Ule utaratibu wa vijiji vya ujamaa uangaliwe, ili kupunguza ujenzi holela na kufikisha huduma za jamii kirahisi zaidi. Tutapunguza gharama kubwa ya kupeleka miundombinu kwa gharama kubwa kwa wananchi wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Geophrey Pinda, Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Damian Sanga, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Lucy Kabyemera, wataalam wa Wizara na wadau wengine kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwenye umuhimu wa kutatua matatizo ya ardhi kwa kuwekeza nguvu ya ziada katika teknoloijia ya TEHAMA. Migogoro ya ardhi imekuwa ni changamoto ya muda mrefu sana nchini Tanzania, ikihusisha umiliki wa ardhi, mipaka na haki ya matumizi ya ardhi. Baadhi ya maeneo yanaathiriwa na migogoro ya kijamii kuhusu umiliki wa ardhi. Migogoro hii mara nyingi hutokea kutokana na ukosefu wa mifumo mizuri ya umiliki wa ardhi, michakato mibovu ya usajili wa ardhi pamoja na ukosefu wa taarifa sahihi za umiliki wa ardhi, ambapo husababisha mwingiliano wa madai ya ardhi kwa mmiliki zaidi ya mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii imekuwa ikisababisha ugomvi wa kudumu na mauaji ya wananchi wanaogombea ardhi. Hapa nchini Tanzania, tumejionea migogoro mikubwa kati ya wakulima na wafugaji na kati ya wamiliki wa mbuga za wanyama, maeneo tengefu na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla idadi kubwa ya waathirika wa migogoro ya ardhi ni watu wa kipato cha chini na

wenye uelewa mdogo wa kisheria, ambao wamekuwa wakiporwa ardhi zao na watu wenye kipato kikubwa na mabavu ya kifedha, kupitia kwenye sheria. Migogoro hii, hapa Tanzania, imekuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo, hasa kwenye kutekeleza miradi inayotegemea ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inayo mifumo miwili rasmi ya kumilikisha ardhi. Nchi yetu inatambua mifumo ya umiliki wa ardhi ifuatayo:-

(i) Umiliki kwa njia rasmi ya kupata hati toka Serikalini; na

(ii) Umiliki kwa kutumia hati za kimila; kwa kiasi kikubwa hati za kimila zimechangia migogoro kutokana na kutosomana na mifumo rasmi ya Serikali. Kutokana na tofauti za kiuendeshaji, mifumo hii miwili imetofautiana sana na kusababisha migogoro na kukwamisha juhudi za usimamizi na upangaji wa ardhi. Kwa mfano, mamlaka za vijiji kupitia mifumo ya umiliki wa kienyeji wanaweza kuamua juu ya matumizi au umiliki wa ardhi, lakini mifumo rasmi ya kisheria, mahakama au kamishina wa ardhi au Waziri au Rais, wakatengua maamuzi husika kutoka mamlaka za vijijini. Jambo hili linatakiwa lipatiwe suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo huchochea migogoro ni changamoto katika utawala wa ardhi kutokana na kuwepo rekodi za ardhi zilizopitwa na wakati na kukosekana kwa taarifa sahihi katika usimamizi wa ardhi. Kwa mfano, ardhi zenye hati miliki zilizomaliza muda wake taarifa huwa hazitoki na wamiliki huendelea kutumia maeneo haya kinyume na sheria. Kadhalika, upatikanaji mdogo wa taarifa juu ya umiliki na utumiaji wa ardhi, ambao huambatana na vikwazo vya kupata taarifa za ardhi huchochea ukosefu wa uwazi na kuaminiana katika shughuli za usimamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa hatua mbalimbali ilizochukua kwa kuweka mkazo kwenye kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi

mijini, vijijini na katika maeneo ya kimkakati. Pia, kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa taarifa za ardhi na uthamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza pia Serikali kwa kusudio la Wizara kuanzisha Kamisheni ya Ardhi, *Land Commission,* ambayo pamoja na mambo mengine itaweka mfumo mmoja wa usimamizi na utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi katika ngazi zote, hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya sekta. Ili kufanikisha malengo haya makubwa ya Wizara, ninaishauri Serikali iimarishe mifumo yote ya kimtandao itakayobeba na kushughulikia utoaji wa hati za umiliki wa ardhi. Kupitia mifumo hii, wananchi watapata huduma kirahisi kwani mifumo hii itakuza uwazi na ushiriki wa wadau wenye mamlaka kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha hili, ni vyema yakatolewa mafunzo ya kujenga uelewa na uwezo kwa wadau wote, wa namna ya kufanya kazi kupitia kwenye hii teknolojia ya TEHAMA. Matumizi ya TEHAMA yataleta suluhu ya mageuzi katika kushughulikia michakato mbalimbali ya vibali na hati za ardhi hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na leo tuko kwenye Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Wizara yetu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli, kwa kuniamini na kunipa nafasi ya Naibu Waziri, ambapo katika awamu zote hizi mbili nimefanya kazi katika Wizara mbili, chini ya Mawaziri saba. Ninawashukuru sana

Mawaziri wote ambao nimefanya nao kazi, wamenijengea uwezo mkubwa sana wa kuelewa na kusimamia taratibu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu hapa, ana moto wa ujana na kwa kweli, ananisaidia sana, katika kusimamia shughuli hizi ambazo ananikasimu kila wakati, kwa ajili ya kutekeleza wajibu wa Wizara. Wanachamwino wasifanye makosa, turudishieni kamanda huyu, aweze kupiganisha jeshi la nchi kavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, Wizara hii changamoto zake ni nyingi sana, lakini ukweli toka Mheshimiwa Waziri amefika tunaona kuna mwelekeo na mabadiliko mapya ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kavuu na leo kwa uwakilishi mdogo sana, wameweza kufika Viongozi wa Chama na Serikali, ambao tumemudu kuwaleta, waje wajionee tu mazingira ya kazi ambazo Wizara yetu imekuwa ikifanya kila panapokucha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru familia yangu kwa jinsi ambavyo wamekuwa wavumilivu katika mapito yangu ya kazi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yangu ni machache. Suala la kwanza, ni hizi Kliniki tunazoziendesha katika Wizara ya Ardhi. Ni kweli kabisa changamoto ni kubwa sana na katika uhalisia tumeona ni muhimu tuwe na vikao vya wazi katika kusikiliza matatizo ya Ardhi na ndiyo hizi Kliniki ambazo tumeendelea nazo. Tumeendelea kujifunza na kutekeleza kwa nguvu zote kuhusu suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi na hasa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma hii, chanzo kikubwa kabisa cha migogoro ya ardhi ambacho kimesababisha *double allocation* hapa Dodoma, moja, ilikuwa ni kuhama kutoka kwenye Mfumo wa *CDA* kuja Mfumo wa hizi Halmashauri. Mfumo wa *CDA* ulikuwa umeshajiwekea utaratibu wake, Mfumo wa Halmashauri ulipokuja kukawa hakuna ule uwiano wa

makabidhiano ya kumbukumbu za *CDA* kwenda kwenye Miji na Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake sasa vile viwanja ambavyo vilikuwa na namba tayari, vimeshakuwa *plotted* na vingine vilifikia mpaka hati, kwa wananchi wale waliokuwa wa asili, waliokuwa wameondolewa katika utaratibu wa awali wakarudi na Halmashauri zilishindwa kuzuia ule mwingiliano. Matokeo yake wananchi sasa kwenye kiwanja kimoja ambacho kilikuwa cha *CDA,* kilichokuwa na mtu mmoja, wale wa asili walivyorudi, walirudi watatu, wanne, watano. Hii ndiyo shughuli ambayo tunaendelea nayo. Kwa sasa tunaweza tukakiri kwamba, kazi kubwa imefanyika na tunaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na *double allocation* 3,000 sasa hivi tumebaki tunazungumza na *double allocation* karibu elfu moja, kama na mia mbili hivi, ambazo tunaendelea kuzitatua. Watuvumilie kwa sababu, kujenga ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kawaida migogoro yote ambayo imetajwa na Waheshimiwa Wabunge ni kweli, ipo kwa sababu, Wabunge wanatoka kwenye maeneo hayo na wanakiri kabisa kwamba, usumbufu huu wa migogoro bado umeendelea na hizi kliniki itakuwa ni zoezi na endelevu. Ingawa tunalitafutia dawa, kama tulivyoeleza mwanzo wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba, tukiunda hizi kamisheni zitakwenda kutusaidia kwa maana mfumo wa utendaji nao ilikuwa ni changamoto nyingine, kwamba, unakwenda inafika mahali Wizara inakatika, kule chini kuna watu wengine ambao wanakuwa na sauti na wale Watendaji. Kwa hiyo, kulikuwa kuna mwingiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile kamisheni inayokwenda kusimama sasa itatufikisha mahali ambapo tunatamani mpaka kwenye kijiji tuwe na Afisa Ardhi, kama taasisi nyingine zinavyofanya kazi, ili tuondokane na hii hadithi ya mwingiliano. Sasa hivi tunakwenda kwa kasi kubwa ya kupima, kupanga na kushirikisha katika kutatua hii migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hii Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji, ambayo nayo huko ile ndiyo msingi wa kwanza ambao tunakwenda kuujenga kwenye vile vijiji, kwa ajili ya kwamba, hata ukuaji wake unapokuja unakuta mji upo tayari umeplaniwa *(planned)*. Hata kama tutauhamisha kutoka kwenye *level* ya kijiji kwenda kwenye mji, bado yale maeneo yatakuwa yameshazingatiwa tayari kutoka kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi, kitakachokuwa kinafanywa pale ni kutanuliwa kuelekea kwenye uhitaji wa mji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli, bajeti yetu ikipita, basi shughuli inaendelea. Kwa kweli, nimeona mawazo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa, sisi tutayazingatia, tutakwenda kuyafanyia kazi kwa haraka sana na kama alichokisema dada yangu, Mheshimiwa mama Msambatavangu, jina gumu kabisa la balozi wetu huyu, katika uhalisia tumezingatia yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *National Housing*. Kama watakumbuka vizuri *National Housing* sasa hivi iko kwenye mageuzi makubwa ya kuelekea kwenye suala la kuleta miji mipya katika maeneo mengi sana. Kwa sasa hivi ni kweli, gharama za nyumba ni za juu sana, haziwezi kukidhiwa na watu wa kipato cha kati na kipato cha chini, hili ni jambo ambalo tunakwenda kuanzisha mazungumzo kati ya sisi, Wizara, pamoja na Wizara za wenzetu; Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kuangalia hasa masuala ya kodi, ambayo kimsingi ndiyo yanayopandisha bei za ujenzi kwa sababu, vifaa vyetu hivi tunavyotumia, kwa ajili ya ujenzi vingi vimepanda bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye uhalisia, wakati wa kuuza ni lazima *VAT* ziingie na vitu vingine. Kwa hiyo, tunaendelea na mazungumzo ya awali na Wizara ya Fedha, ili kuona uwezekano wa kuhakikisha kwamba, lengo la *National Housing* liweze kurudi katika mfumo wake wa kawaida, kwamba, wananchi wajengewe nyumba zenye bei nafuu na wanazoweza kumudu kuzinunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yote ambayo yamechangiwa na Wabunge kwenye sekta hizi tunayachukua na mengine atakuja kuhitimisha Mheshimiwa Waziri. Nipende tu kukushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kuongoza Bunge hili siku hii ya leo na kuweza kufikia wakati huu wa kuhitimisha hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninatumia fursa hii tena kuishukuru Kamati yako ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, chini ya uongozi wake Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini. Kwa kweli, Kamati hii imekuwa ikitoa miongozo, ambayo imefanya leo tumefikia mafanikio makubwa sana katika utendaji kazi wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninawashukuru wachangiaji wote waliochangia hoja yetu hii, jumla ya wachangiaji nane wamechangia hoja hii. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, mawazo na ushauri wote walioutoa, sisi kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tunaenda kuufanyia kazi na kuhakikisha kwamba, tunaporejea hapa waone mambo yote waliyoyasema yamefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumzia. Suala la Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, miaka minne hii ya utawala wa Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan, tume hii imefanya kazi kubwa sana. Kwa sababu, tangu tupate uhuru katika vijiji 12,333 tulivyonavyo, amezungumza hapa Mheshimiwa Mnzava, vijiji

vilivyokuwa vimewekewa matumizi bora havizidi 2,600, lakini katika kipindi cha miaka minne tumeona vijiji zaidi ya 4,000 vikiwa vimewekewa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza, kwa ushauri wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, tumefanikiwa kupokea shilingi bilioni tano kutoka Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kwenda kuendeleza upimaji wa vijiji 333 na kuweka matumizi bora. Kazi hiyo imezinduliwa Wilayani Ikungi, Mkoani Singida, wiki kadhaa zilizopita na Kamati yako ya Bunge ilishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawahakikishia kwamba, lengo la Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi wasaidizi wake ni kuhakikisha mipango ya matumizi bora ya ardhi inakuwepo kwenye vijiji vyote 12,333. Hii ndiyo itakwenda kuondoa mzizi wa migogoro ya ardhi, hasa kati ya wakulima na wafugaji. Amezungumza hapa Mheshimiwa Lusinde, ipo migogoro kwa sababu ya maeneo kutokupangwa na kuwekwa, kwa ajili ya ufugaji na kilimo, ama maeneo mengine yanakuwa yamepangwa, ambayo hayako *suitable,* kwa ajili ya kimoja ama kingine. Kwa kupima vijiji vyote hivi, tutahakikisha tunaondokana na changamoto hiyo. Ninalihakikishia Bunge lako kwamba, tunakwenda kutekeleza hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *Plot Development Revolving Fund,* ambapo ndiyo Mradi wa KKK upo. Tangu *Development Fund* hii ianzishwe haikuwahi kuwekewa hata senti moja, lakini katika kipindi cha uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza kuweka shilingi bilioni 50, ambayo fedha hii imekwenda kupima viwanja zaidi ya 12,303.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Chege, amezungumza changamoto ya halmashauri kutorejesha fedha hizi. Tumekaa na wenzetu wa TAMISEMI, tumekaa na wenzetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambayo yeye, Mheshimiwa Chege, ni Makamu Mwenyekiti. Tumekubaliana ya kwamba, kuanzia sasa hakuna maombi yoyote ya halmashauri yataletwa moja kwa moja kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama halmashauri inaona ina uhitaji mkubwa wa kupima viwanja kupitia Mradi huu wa KKK ipitishe maombi yake TAMISEMI; TAMISEMI ione uwezo wa halmashauri ile kurudisha. Kwa sababu, wengine walichukua fedha, walienda kupima katika maeneo ambayo hayauziki na ndiyo maana fedha hii hairejei. Tumeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba, tunalinda fedha hizi shilingi bilioni 50 zilizotolewa na Dkt. Samia Suluhu Hassan na tunahakikisha viwanja zaidi vinaendelea kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumziwa kwa upana wake na Waheshimiwa Wabunge waliochangia; amezungumza Mheshimiwa Mnzava, Mheshimiwa Kunambi, Mheshimiwa Asenga na Waheshimiwa wengine waliopata nafasi ya kuzungumza wamegusia sana suala la Kamisheni ya Ardhi na namna ambavyo inakwenda kutatua changamoto mbalimbali. Ninasema mbele ya Bunge lako Tukufu, tumechelewa sana kuwa na Kamisheni kama hii ya Ardhi na tumechelewa sana kuweka utaratibu madhubuti wa kuhakikisha nchi yetu inakuwa imepimwa na imepangwa vilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuna mwingiliano mkubwa kati ya Mamlaka ya Upimaji na Mamlaka ya Halmashauri, kuna changamoto kubwa. Kwenye *master plan* unakuta kuna eneo, mfano Jimboni kwako pale Kariakoo, *master plan* huenda inasema mwisho ni ghorofa kadhaa, tano au sita, ama jengo lilijengwa kama *apartment*, tumeona changamoto zikijitokeza za maghorofa kudondoka, lakini mabadiliko ya matumizi yanapofanyika Wizara ya Ardhi haihusiki. Mabadiliko ya matumizi kwenda kwenye *commercial* hayapiti katika *entity* nyingine za Serikali kuhakikisha ya kwamba, jengo lile linaweza kuhimili mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwa Dar es Salaam, Masaki na *Oyster Bay*, mpango madhubuti wa maeneo yale uliopitishwa na Baraza la Mawaziri unasema ni *ground plus five, maximum*. Kuna watu wanaojenga *ground plus nine, plus ten,* ni kwa sababu ya mamlaka kuingiliana. Anapokwenda kuomba kibali cha ujenzi, mtu anaomba cha ghorofa 10 anapewa,

hawajui *master plan* iko vipi! Suluhisho la hili na migongano hii inayojitokeza ni kuhakikisha tunakuwa tuna *Land Commission*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawatoa mashaka Waheshimiwa Wabunge, kuwa na *Land Commission* hii haimaanishi kwamba, tunakwenda kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Bado Serikali za Mitaa itakuwa ni kiungo muhimu sana katika utekelezaji wa kazi za Kamisheni hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia ndugu yangu, Mheshimiwa Kunambi, amezungumzia suala la Tume na *RERA* kuwa, chini ya *Commission* hii. Sasa kwa sababu tuko katika *initial stages* za kuanzisha tume hii tunachukua mawazo hayo na kwenda kuyafanyia kazi. Nimemsikia Mheshimiwa Mnzava akisema isiathiri *D by D;* haitoathiri *D by D,* tutahakikisha tunaboresha yale malengo ya *D by D* yaweze kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye suala la kuanzisha *Real Estate Regulator Authority (RERA),* kwenye masuala ya miliki, na lenyewe tumechelewa sana. Kumekuwa kuna uholela mwingi katika Sekta ya *Real Estate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mwananchi wa kawaida anayetaka kununua kiwanja ili aweze kujenga kwa kipato chake anachokipata anaweza akatafuta dalali A akamwonyesha kiwanja, dalali B, akamwonyesha kiwanja kile kile, dalali C, akamwonyesha kile kile; lakini si ajabu hawa watu wote mwenye kiwanja hawafahamu, mwenye kiwanja hawajui, ama hata nyumba ambayo inauzwa; ni kwa sababu kuna uholela mwingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kuweka utaratibu ambao utamlinda Mtanzania katika kuhakikisha tunawafahamu wenye nyumba, tunawafahamu wanaofanya kazi katika sekta ya milki ili mwananchi awe salama, lakini hata mwenye nyumba na yeye awe salama. Kwa hiyo ni jambo ambalo nalo lilichelewa na niwahakikishie tutalileta hapa Bungeni kwa ajili ya kupitisha sheria zake tuweze kuanza kulitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa hapa suala la migogoro ya ardhi. Ni kweli kwamba kuna changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi na migogoro hii ipo ya aina mbalimbali. Kuna migogoro ambayo ni *administrative* ambayo ni jukumu letu kama Wizara, kuna migogoro ambayo ni ya kifamilia, lakini tafsiri ya jamii inaona kama ni wajibu wa sekta ya ardhi kutatua *administratively;* labda mirathi na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna migogoro ambayo imeshatolewa maamuzi na Mahakama. Katika maamuzi hayo sisi kama *administrators* hatuwezi kuingilia Mhimili mwingine; wajibu wa ku-*counter* maamuzi yale ya Mahakamani kukata rufaa katika chombo cha Mahakama ili uamuzi unapotoka, sisi kama *administrators* tuweze kutekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengine lazima nikiri ni migogoro iliyotengenezwa na watumishi wetu wenyewe katika sekta ya ardhi. Mheshimiwa Msambatavangu amezungumzia kuhusu masuala la *double allocation* ambayo yamekuwa kinara katika Jiji letu la Dodoma na maeneo mengine. Nitoe maelekezo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hapa leo mbele ya Bunge lako Tukufu; ni marufuku kuendelea kutumia mfumo mwingine zaidi ya *e-ardhi* katika kutoa au kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *double allocation* ilikuwa inatokeaje; unakuta mtumishi wetu kwa makusudi na kwa kufahamu anakwenda kwenye mfumo ambao hatuutumii tena wa *MORIS* anatoa hati. Anakuja Mheshimiwa Msambatavangu na yeye anataka hati ya kiwanja hicho hicho anaingia kwenye *e-ardhi,* kwa sababu mifumo ile ilikuwa haisomani. Kwa hiyo unakuta eneo moja lina hati mbili. Kuanzia leo ni marufuku kuendelea kutumia mfumo wa zamani. Tutahakikisha nchi nzima mpaka ifikapo mwaka 2027 tunaweka mfumo mzima wa *e-ardhi* ili kuondokana na changamoto hizi za migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Kunambi kuwa nitafika Jimboni kwake. Nimhakikishie Mheshimiwa Asenga kuwa mgogoro ule wa pale kwa Baba Askofu tayari

fedha imekwishapelekwa kwa ajili ya kuanza upimaji na kwenda kutatua. Vile vile Mheshimiwa Halima juzi tumekaa na wazee wale; niwaahidi na Mheshimiwa Mbunge wa jimbo rafiki yangu Mheshimiwa Mtemvu, kuwa tutahakikisha kwamba tunafika kuweza kusikiliza pande zote mbili tuone tutatue changamoto ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, si tu kwa Mheshimiwa Mtemvu, hata kwa Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambapo maeneo haya yameingiliwa. Tayari kuna nyumba zaidi ya laki mbili katika eneo hilo; ninaamini tutapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya Shirika letu la Nyumba na wewe mwenyewe uliligusia wakati unamtambulisha *DG*. Ni kwamba tunaendelea na mradi wa *Samia Scheme;* na tunatafuta njia bora ya kuhakikisha kuwa tunapata nyumba za bei nafuu ambazo Watanzania wengi wataweza ku-*afford* kuzinunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kuwa ililetwa Bungeni hapa kwa ajili ya kuondoa *VAT* katika nyumba ambazo zipo chini ya milioni 50; na sasa tunapoelekea ni kutafuta namna ya kuondoa *VAT* kwenye nyumba amhazo hazizidi milioni 100; na huku tunatafuta teknolojia mpya kwa kuangalia kwa wenzetu nchi mbalimbali wanajenga vipi katika kupunguza gharama ili tupate nyumba ambayo Mtanzania wa kawaida ataweza ku-*afford*. Hii ndiyo njia pekee pia ya kulinda ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi tuliyokuwanayo wakati wa uhuru wetu mwaka 1961 tukiwa Watanzania milioni tisa ni ardhi ile ile na mipaka ile ile ambayo tunayo leo hii ambayo tuko Watanzania milioni 65. Tukiacha tusambae bila mipango, bila kwenda juu na kujenga nyumba za bei nafuu tutajikuta tunamaliza ardhi yote ambapo vizazi vijavyo vitakosa mahali pa kwenda. Ni lazima tujenge kwenda juu, lakini vile vile tuipendezeshe na miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mingine ya Waheshimiwa Wabunge tumeipokea kwa maandishi; niwaahidi tunakwenda kuifanyia kazi. Tutahakikisha kwamba tunaibadili sekta ya ardhi kwa kuweka mifumo madhubuti ya kuhakikisha tunaondokana na migogoro. Niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais katika kipindi changu cha Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ametupa *support* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi majuzi tu ametupatia magari zaidi ya 50 ambayo yanakwenda kuongeza kasi ya utekelezaji wa shughuli zetu katika sekta hii ya ardhi. Hata hili *land commission* ambalo tunalizungumzia ni jambo ambalo yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais alielekeza Siku ya Uzinduzi wa Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995, Toleo la 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara ipo mbioni katika kuandaa sheria mbalimbali zinazotokana na sera ile ili tulete hapa Bungeni; na kanuni mbalimbali, ili tuanze kutekeleza sasa kama vile sera inavyotutaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, ninaomba sasa nitoe hoja mbele ya Bunge lako ili tuweze kupitishiwa bajeti yetu. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 11,776,811,824
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 1,232,475,493
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*.....Sh. 1,102,932,385
Kifungu 1004 - *Management Information System Unit*…………………………………….Sh. 1,653,911,459
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*..................................Sh. 486,078,519
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*……..Sh. 644,503,570
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*.....Sh. 583,613,920
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*...............................Sh. 658,619,032
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*……….Sh. 510,257,733
Kifungu 2001 - *Land Management and Development Department*............Sh. 16,979,276,788
Kifungu 2002 - *Surveys and Mapping Department*…………………………..Sh. 13,249,870,054
Kifungu 2003 - *Registration of Titles Unit*....................Sh. 1,066,174,890
Kifungu 2004 - *Valuation Department*......................Sh. 5,638,508,767
Kifungu 2005 - *Dar es Salaam Land Office*..............Sh. 1,397,732,000
Kifungu 2007 - *Dodoma Land Office*...........................Sh. 940,000,000
Kifungu 2008 - *Tabora Land Office*..............................Sh. 690,000,000
Kifungu 2009 - *Mwanza Land Office*...........................Sh. 924,000,000
Kifungu 2010 - *Kilimanjaro Land Office*........................Sh. 720,000,000
Kifungu 2011 - *Mtwara Land Office*.............................Sh. 610,000,000
Kifungu *2012* - *Mbeya Land Office*..............................Sh. 834,828,000
Kifungu 2013 - *Simiyu Land Office*................................Sh. 600,362,000
Kifungu 2014 - *Arusha Land Office*..............................Sh. 734,716,000
Kifungu 2015 - *Geita Land Office*................................Sh. 620,000,000
Kifungu 2016 - *Njombe Land Office*............................Sh. 620,000,000
Kifungu 2017 - *Katavi Land Office*...............................Sh. 620,000,000

Kifungu 2018 - Coastal Land Office.............................Sh. 744,023,000
Kifungu 2019 - *Iringa Land Office*................................Sh. 540,494,000
Kifungu 2020 - *Kigoma Land Office*.............................Sh. 638,545,000
Kifungu 2021 - *Lindi Land Office*..................................Sh. 620,000,000
Kifungu 2022 - *Mara Land Office*.................................Sh. 735,000,000
Kifungu 2023 - *Morogoro Land Office*..........................Sh. 880,000,000
Kifungu 2024 - *Ruvuma Land Office*............................Sh. 660,000,000
Kifungu 2025 - *Shinyanga Land Office*.........................Sh. 640,000,000
Kifungu 2026 - *Singida Land Office*.............................Sh. 614,000,000
Kifungu 2027 - *Tanga Land Office*...............................Sh. 824,000,000
Kifungu 2028 - *Kagera Land Office*.............................Sh. 690,000,000
Kifungu 2029 - *Rukwa Land Office*..............................Sh. 570,000,000
Kifungu 2030 - *Songwe Land Office*............................Sh. 570,000,000
Kifungu 2031 - *Manyara Land Office*...........................Sh. 619,403,000
Kifungu 3001 - *Human Settlement Development Department*....................................Sh. 10,627,173,028
Kifungu 3002 - *Real Estate Unit*.....................................Sh. 468,877,083
Kifungu 3003 - *District Land and Housing Tribunal Unit*…………………………...Sh. 6,043,850,455

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 003 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001 - *Directorate of Corporate Services*...Sh. 3,090,268,592
Kifungu 1003 - *Procurement and Management Unit*……………………………………...Sh. 223,698,500

Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 181,489,369
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*...............................Sh. 507,430,000
Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Mngment & Coordination Division*…..Sh. 772,340,000
Kifungu 2002 - *Directorate of Research, Compliance & Information*..................Sh. 888,396,208
Kifungu 2003 - *Zonal Offices*.....................................Sh. 2,523,946,331

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## KITABU CHA NNE

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....................Sh. 645,500,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Department*.........................Sh. 0
Kifungu 1004 – *Management Information System Unit*................Sh. 0
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*.................................Sh. 210,000,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 232,000,000
Kifungu 2001 – *Land Management & Development Department*...............Sh. 3,295,969,000
Kifungu 2002 – *Surveys and Mapping Department*…………………………Sh. 57,674,360,000
Kifungu 3001 – *Human Settlement Development Department*....................................Sh. 57,674,360,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 003 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Kifungu 1001 – *Directorate of Corporate Services*.....Sh. 126,010,000
Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Mngment & Coordination Division*...Sh. 2,333,356,000
Kifungu 2002 – *Directorate of Research, Compliance & Information*...............Sh. 2,520,616,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni 123(3)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba sasa Bunge likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumzi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA.** Walioafiki wameshinda. Mheshimiwa Waziri, kwanza nikupongeze sana kwa namna unavyoitendea haki Wizara hii; wewe, Mheshimiwa Naibu wako, Katibu Mkuu wako na taasisi unazoziongoza.

Waheshimiwa Wabunge ninawashukuru kwa michango mizuri, Kamati ya Ardhi kwa ushauri ambao mmeipa Serikali. Hili la

*affordable houses* ni kitu muhimu sana, mpaka sasa hivi mmejenga nyumba nyingi nzuri na ambazo hazina gharama.

*Affordable houses* kuna *bachelor quoters* chumba kimoja kinamtosha. Pamoja na hiyo mmeweka nyumba ambazo watu wanaweza kumudu; kama vile milioni 25, milioni 28, milioni 30, milioni 18. Nchi nyingi zinafanya, lakini muhimu ni lazima muweke sheria ili kuwalinda wale wanaoingia mle ndani na kuzuia mtu mwenye uwezo asiende kwenye kupora haki za watu wa kipato kile cha chini.

Mheshimiwa Waziri, nendeni Malaysia mkatazame *affordable houses* zao walivyozifanya. Wameweka sheria kabisa kwa ajili ya kuzuia mtu mwingine nje ya kiwango kile cha pesa kuingia na kuchukua nyumba nyingi, kuzifanyia biashara na kuwaonea wale ambao walikuwa ni haki yao kuingia pale. Kwa hiyo niombe sana ndugu zangu na hii itakuwa ni *legacy* ya Mheshimiwa Rais, kuwapa wananchi wake makazi bora na salama. *Legacy* yako na Mungu akujalie urudi tena; na kila kitu ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu.

Baada ya maneno haya, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru watendaji wa taasisi mbalimbali za Wizara yako. Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.11 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 30 Mei, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*